# Kuzaliwa Mara ya Pili

# Kuzaliwa Mara ya Pili

EDITORIAL PEREGRINO

Kuzaliwa Mara ya Pili

Editorial Peregrino
Apartado 19
13350 Moral de Calatrava (Ciudad Real)
Uispania

Kuandaliwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiingereza na Christian Focus Publications Ltd mwaka wa 2009 na kuitwa Finally Alive.

© Desiring God Foundation 2009.

Kuandaliwa mara ya kwanza katika lugha ya Kiswahili na Editorial Peregrino, mwaka wa 2011.

Publication under the auspices of Christian Books Worldwide
© 2011 Editorial Peregrino kwa Kiswahili.

Mtafsiri: Sukesh Pabari.

Kuhakikishwa na Ronald Kogo na Paul Musembi

Jalada imetayarishwa na Samuel Cabera Fernandez.

Mistari ya Biblia imenuukuliwa kutoka Holy Bible in Kiswahili, © 2010. Imechapishwa na Biblica – Africa, P.O. Box 60595 – 00200, Nairobi, Kenya.

Kimechapishwa katika nchi ya Uispania.

ISBN: 978-84-96562-75-2
Depósito legal:

Kimechapishwa katika nchi ya Uispania
*Printed in Spain*

# Yaliyomo

**Utangulizi** 11

**Sehemu ya Kwanza: Je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili?**

Sura ya Kwanza, Jambo la kuzaliwa mara ya pili ni jambo muhimu sana 29

Sura ya Pili, Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kupewa maisha mapya kutoka kwa Mungu 34

Sura ya Tatu, Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha haitoshi kujua kwamba Yesu Kristo ni Bwana, bali kupata maisha ya kiroho kutoka kwake 37

Sura ya Nne, Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kuwa kiumbe kipya 42

**Sehemu ya Pili, Je ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili?**

Sura ya Tano, Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu tumekufa katika mambo ya kiroho 55

Sura ya Sita, Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu sisi ni watumwa wa dhambi na shetani 67

Sura ya Saba, Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu tutapata faida nyingi 73

Sura ya Nane, Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ili tuweze kufahamu ni kwa nini Kristo alikuja hapa ulimwenguni 79

Sura ya Tisa, Uhusiano kati ya kuja kwake Kristo na kuzaliwa kwetu mara ya pili 84

**Sehemu ya Tatu, Je, ni namna gani mtu anazaliwa mara ya pili?**

Sura ya Kumi, Ni nini Mungu anafanya ili tuweze kuzaliwa mara ya pili 93

Sura ya Kumi na Moja, Kuzaliwa upya kwa viumbe vyote 105

Sura ya Kumi na Mbili, Mungu anatuzaa mara ya pili kwa kutuosha na kwa kutufanya watu wapya 109

Sura ya Kumi na Tatu, Mungu anatuzaa mara ya pili kupitia kwa imani 116

Sura ya Kumi na Nne, Tunazaliwa mara ya pili kupitia kwa mahubiri ya ujumbe wa Biblia 125

**Sehemu ya Nne, Je, matokeo ya kuzaliwa mara ya pili ni gani?**

Sura ya Kumi na Tano, Yule ambaye amezaliwa mara ya pili ataushinda ulimwengu 133

Sura ya Kumi na Sita, Kuzaliwa mara ya pili, imani na upendo 144

Sura ya Kumi na Saba, Uhuru kutoka kwa tabia ya dhambi 155

Sura ya Kumi na Nane, Kuwapenda wengine na upendo wa Mungu 165

**Sehemu ya Tano, Je, ni namna gani tunaweza kuwasaidia wengine ili wazaliwe mara ya pili?**

Sura ya Kumi na Tisa, Waambieni wote habari njema ya Yesu Kristo 177

Sura ya Ishirini, "Ninawatuma kufungua macho yao" 187

Sura ya Ishirini na Moja, Kuzaliwa Upya na nchi mpya 198

*“Kwa hiyo usishangae ninapokuambia huna budi kuzaliwa mara ya pili. Upepo huvuma po pote upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi ukafahamu utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na Roho”.*

Yohana 3:7-8

# Utangulizi

Yesu Kristo alisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:7). Hii inamaanisha kwamba jambo hili la kuzaliwa mara ya pili ni jambo kuu sana, na kwa hivyo kila mmoja wetu anapaswa kulifahamu vizuri sana jambo hili. Katika kitabu cha Yohana sura ya tatu, Yesu Kristo anafundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili, na wakati tunasoma sura hii, tunaona kwamba sisi wanadamu ni wenye dhambi, na hatuwezi kufanya chochote kujiokoa: "Upepo huvuma po pote upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi ukafahamu utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na Roho" (Yohana 3:8). Yesu Kristo hapa anaongea kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu, na anasema kwamba kazi ya kuokoa watu wa Mungu ni kazi yake Roho Mtakatifu.

Kuna watu wawili katika historia ya dunia ambao maisha yao yanaonyesha wazi kabisa kwamba wokovu ni kazi ya Mungu Roho Mtakatifu mwenyewe. Kwanza, tunasoma kumhusu mtu mmoja ambaye aliitwa Augastine ambaye aliokoka mwaka wa 386, na pili tunasoma kumhusu mtu mwingine ambaye aliitwa C.S. Lewis ambaye aliokoka mwaka wa 1931. Wote wawili walikaa miaka mingi bila wokovu na walipiga vita dhidi ya Mungu miaka mingi kabla ya kuokoka. Lakini Mungu Roho Mtakatifu alitumia njia tofauti kabisa kumwokoa kila mmoja wao.

### Hadithi ya Augustine

Augustine alikuwa na dhambi moja ambayo alipenda sana, na hii ilikuwa dhambi ya uasherati. Kwa miaka 16, yeye alifuata dhambi hii kwa moyo wake wote. Wakati alikuwa miaka 16 aliondoka nyumbani mwake na kuanza kuishi maisha ya dhambi. Lakini mamake Monika alikuwa ameokoka, na yeye alivumilia kumwombea kijana wake. Wakati Augustine alikuwa miaka 32, alianza kuwaza juu ya wokovu. Aliandika, "Nilitafuta njia ya

kupata furaha katika Mungu, na niliona kwamba siwezi kupata furaha katika Mungu bila kumwamini Yesu Kristo."

Siku moja, katika mwaka wa 386, Augustine alikuwa akitembelea rafiki yake mmoja, Alypius. Hawa wawili walikuwa wakiongea kumhusu mtu mmoja ambaye alikuwa mtakatifu sana na aliitwa Antony. Augustine alijua kwamba yeye mwenyewe alikuwa mtumishi wa dhambi na kwamba wale ambao walikuwa wameokoka walikuwa huru katika Kristo. Augustine aliandika, "Nilikuwa katika bustani la nyumba moja wakati niliongea na rafiki yangu. Nilijua kwamba mimi ni mwenye dhambi mkuu mbele za Mungu na nilikuwa na wasiwasi sana moyoni mwangu kwa sababu ya dhambi zangu. Nilijua kwamba katika moyo wangu nilikuwa na vita, na kwa sababu ya vita hivi karibu niwe wazimu! Nilijua kwamba Mungu ananiita niende kwake ili nipate msamaha wa dhambi zangu, na nilitaka sana kwenda kwake. Hii ndiyo sababu nilikuwa na vita moyoni mwangu."

Wakati Augustine alikuwa katika bustani hili alianza kuona kwamba maisha ya dhambi yatamharibu kabisa, na maisha ya wokovu katika Kristo yatamletea faida kubwa sana. Kwa hivyo alikuwa na vita hivi ndani yake: kuendelea kufuata maisha ya dhambi na kujiharibu au kufuata maisha matakatifu katika Kristo na kupata furaha nyingi kwa kuokoka. Augustine aliandika,

> "Vita hivi viliendelea ndani yangu hadi nililia sana. Baada ya muda kidogo, nilisikia sauti ya mtoto mdogo ambaye alicheza mchezo fulani karibu na lile bustani. Mtoto huyu alikuwa akiimba, 'Chukua na usome, chukua na usome!' Kwa hivyo nilichukua Biblia ambayo ilikuwa karibu nami na nilianza kuisoma. Nilifungua Biblia na nilisoma maneno haya: 'Basi na tuenende kwa adabu kama inavyopasa wakati wa mchana, si kwa kufanya karamu za ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali jivikeni Bwana Yesu Kristo, wala msifikiri jinsi mtakavyotimiza tamaa za miili yenu yenye asili ya

> dhambi' (Warumi 13:13-14). Wakati nilimaliza kusoma maneno haya, nuru ya Mungu iliingia moyoni mwangu na giza la dhambi liliondoka."

Hapa tunasoma ni namna gani Augustine aliokoka. Baada ya siku hiyo, yeye hakurudi kwa dhambi zake. Tunaona hapa ni namna gani Roho Mtakatifu alimwokoa. Roho Mtakatifu alitumia sauti ya mtoto mdogo ambaye alicheza katika bustani fulani karibu na Augustine, na pia Roho Mtakatifu alitumia neno la Mungu kuondoa giza kutoka moyoni wake na kuleta nuru ndani yake.

### Hadithi ya C.S. Lewis

Mwaka wa 1925, Lewis alianza kufundisha lugha ya kiingereza katika chuo kikuu katika nchi ya Uingereza. Wakati huo yeye alikuwa hajaokoka. Leo yeye anajulikana sana katika nchi yake kwa sababu yeye ameandika vitabu vingi sana.

Siku moja katika mwezi wa Septemba mwaka wa 1931, Lewis alizungumza na rafiki wawili kuhusu dini ya Ukristo. Tunaweza kuona kwamba Mungu Roho Mtakatifu alianza kazi yake ndani ya Lewis siku hiyo.

Kesho yake, Lewis aliokoka, lakini jambo hili lilikuwa tofauti kabisa na lile la Augustine. Lewis alikuwa ndani ya gari akienda safari fulani. Baada ya kuokoka aliandika hivi:

> "Nilikuwa safarini ndani ya gari wakati niliokoka. Wakati gari lilianza safari yake mimi sikuamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, lakini wakati gari lilimaliza safari yake baada ya masaa machache tu, mimi nilimwamini Kristo. Lakini wakati wa safari hii sikuwa na mawazo kuhusu wokovu au sikuhisi mambo mengi moyoni mwangu. Nilikuwa kama mtu ambaye anazinzia kitandani. Hivi ndivyo ilikuwa wakati mimi nilioko nikiwa safarini siku hiyo."

Tunaona hapa kwamba hawa watu wawili waliokoka, lakini njia ambayo Mungu alitumia kuwaokoa ilikuwa tofauti kabisa. Augustine alikuwa na vita vikubwa sana ndani yake wakati aliokoka, lakini Lewis alikuwa tu safarini na Mungu alimwokoa. Wote wawili baada ya kuokoka waliweza kusema, "Sisi tunajua ya kwamba tumepita kutoka kwa mautini kuingia uzimani" (1 Yohana 3:14). Kitabu hiki kimeandikwa kufundisha kuzaliwa mara ya pili ni nini.

## Kuchanganyikiwa kuhusu kuzaliwa mara ya pili

Kuna watu wengi leo ulimwenguni ambao hawafahamu vizuri kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha nini. Wakati tunaona mambo hapa ulimwenguni, tunaona kwamba kuna wengi leo ambao wanadai wamezaliwa mara ya pili. Lakini wakati tunachunguza maisha yao, tunaona kwamba hakuna tofauti kamwe kati ya maisha yao na maisha ya wale ambao hawajazaliwa mara ya pili. Wakati unachunguza maisha yao kwa nje, wanaonekana kwamba kweli wao wamezaliwa mara ya pili na ni watu wa Mungu. Wao wanasema wamezaliwa mara ya pili, na kila wiki wanaenda kanisani. Pia wao wanadai wanamhudumia Mungu katika makanisa yao: wengine ni waimbaji, na wengine wanahubiri neno la Mungu. Wote wanadai kwamba wanaishi maisha matakatifu ya kumpendeza Mungu.

Lakini wakati tunachunguza maisha yao kwa makini sana, tunaona kwamba ukristo wao ni wa nje tu, ni ukristo wa kuwaonyesha wengine tu, si ukristo wa ukweli. Mioyoni mwao, wao wanapenda pesa na vitu vya dunia na anasa za dunia kama tu wale ambao hawajazaliwa mara ya pili. Wengi wao wanafanya kazi ya kanisa si kwa sababu wanapenda Mungu, bali wanawaza kwamba watapata faida ya pesa na vitu vya dunia. Pia, wakati tunachunguza maisha yao ya siri, tunaona kwamba wao ni wenye dhambi kama tu wale ambao hawadai kwamba wamezaliwa mara ya pili. Kwa nje, wanaonyesha kwamba wao ni watu wa Mungu

na watu watakatifu, lakini mbele za rafiki wao wa karibu sana wao wanaishi maisha ya dhambi na wanapenda dhambi kama tu watu wa dunia.

### Makosa makuu

Sasa, kuna jambo moja kuu sana ambalo sisi sote tunapaswa kufahamu vizuri sana. Tunapaswa kufahamu kwamba, fahamu ya watu wengi kuhusu kuzaliwa mara ya pili ni fahamu ya uongo. Tunapaswa kufahamu kwamba watu wengi sana wanafanya makosa makuu wakati wanawaza juu ya kuzaliwa mara ya pili. Wengi wanawaza kwamba wao wanajua kuzaliwa mara ya pili ni nini na ni namna gani mtu anazaliwa mara ya pili, lakini kwa ukweli wamechanganyikiwa kabisa. Fahamu yao kuhusu kuzaliwa mara ya pili ni tofauti kabisa na yale Biblia inafundisha kuhusu jambo hili.

Leo, mtu akisema, “Nimezaliwa mara ya pili,” watu wengi wa dunia wanamwamini. Wao watasema, “Huyu amesema kwamba yeye amezaliwa mara ya pili na ameokoka, basi, hii ni kweli. Yeye kweli amezaliwa mara ya pili, yeye kweli ameokoka.” Halafu baada ya muda wanaona kwamba mtu huyu anaishi maisha yake kama tu watu wa dunia wanaishi maisha yao. Wanaona kwamba huyu mtu anafanya mambo mabaya mabaya na anapenda sana dunia. Wakati watu wa dunia wanaona hii, wanasema, “Kweli hata wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanaishi maisha yao kama tu watu wa dunia!” Kwa kusema hivi wao wanamaanisha kwamba mtu anaweza kuwa amezaliwa mara ya pili lakini maisha yake yawe hayana mabadiliko hata kidogo. Watasema, “Yeye anaishi maisha yake tu kama watu wa dunia, ingawa amezaliwa mara ya pili. Kwa hivyo kuzaliwa mara ya pili na kuokoka haimaanishi kwamba mtu atakuwa tofauti na wengine. Hata wale ambao wamezaliwa mara ya pili na kuokoka wanaishi tu maisha ya dhambi.”

Hivyo ndivyo watu wa ulimwengu wanawaza wakati wanaona kwamba yule ambaye anadai amezaliwa mara ya pili anaishi maisha ya dhambi. Lakini haya ni makosa makubwa.

**Mafundisho ya Agano Jipya.**

Wakati tunasoma Agano Jipya, tunapata mafundisho ambayo ni tofauti kabisa na yale ambayo wengi leo wanafundishwa. Leo wengi wanafundishwa kwamba mtu akisema kwamba yeye amezaliwa mara ya pili na kuokoka, wote watamwamini na kusema, "Kweli amezaliwa mara ya pili." Halafu wakati mtu ambaye anadai amezaliwa mara ya pili anaishi maisha ya dhambi, wengi wanasema kwamba hakuna tofauti yoyote kati ya wale ambao wameokoka, na watu wa dunia. Wengi leo wanafundishwa haya. Lakini wakati tunasoma Agano Jipya tunapata mafundisho ambayo ni tofauti kabisa na haya.

Agano Jipya linasema kwamba kuzaliwa mara ya pili si kazi ya mwanadamu, bali ni kazi ya Mungu mwenyewe. Pia, Agano Jipya linasema kwamba ikiwa mtu anadai amezaliwa mara ya pili, lakini anaishi maisha ya dhambi kila siku, basi yeye hajazaliwa mara ya pili. Agano Jipya linafundisha kwamba mtu huyu amejidanganya, au yeye anajua kwamba yeye hajazaliwa mara ya pili lakini anataka kuwadanganya wengine ili apate faida fulani, na kwa hivyo anaonyesha kwamba yeye amezaliwa mara ya pili. Agano Jipya linatufundisha kwamba ikiwa mtu amezaliwa mara ya pili, basi maisha yake yatabadilika kabisa na yeye ataanza kuishi maisha matakatifu, na ikiwa maisha yake hayajabadilika, basi yeye hajazaliwa mara ya pili, hata kama anasema kwa mdomo wake kwamba amezaliwa mara ya pili.

Kwa mfano, wakati tunasoma waraka wa 1 Yohana, tunasoma mambo haya wazi kabisa.

- "Kama mkijua kuwa Yeye ni mwenye haki, mwajua kwamba kila atendaye haki amezaliwa na Yeye" (1 Yohana 2:29).

- "Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu" (1 Yohana 3:9).

- "Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu naye anamjua Mungu" (1 Yohana 4:7).

- "Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4).

- "Tunajua ya kuwa yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, bali aliyezaliwa na Mungu hujilinda wala yule mwovu hawezi kumdhuru" (1 Yohana 5:18).

Katika kitabu hiki tutajifunza mistari mingi kama hii ili tuone ni nini Biblia inafundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Tunajua kwamba hakuna yeyote ambaye amekamilika na kwamba hakuna yeyote ambaye hatendi dhambi. Hii tunajua. Lakini pia tunajua kwamba ikiwa mtu anadai amezaliwa mara ya pili, lazima aanze kuacha dhambi zake na kufuata njia ya utakatifu. Mistari kama hii inatuonyesha kwamba kuna wengi leo ambao wamechanganyikiwa kuhusu wokovu. Wengi wanadai kwamba wamezaliwa mara ya pili, lakini kwa ukweli hawajazaliwa mara ya pili. Wengi wanaonekana kwamba wamezaliwa mara ya pili, lakini kwa ukweli wanawadanganya wengine, na hawajazaliwa mara ya pili kamwe. Mungu anajua mambo haya yote, na hii ndiyo sababu waraka wa 1 Yohana uliandikwa. Biblia inatufundisha kwamba wengi ambao hawajazaliwa mara ya pili wameingia kanisani na wameleta kuchanganyikiwa kwingi.

**Ni kwa nini nimeandika kitabu hiki.**

Kitabu hiki kinahusu kuzaliwa mara ya pili. Nina sababu tatu ni kwa nini nimeandika kuhusu kuzaliwa mara ya pili katika kitabu hiki.

1. Kwanza, nimeandika kuhusu kuzaliwa mara ya pili kwa sababu kuna kuchanganyikiwa kwingi duniani leo kuhusu jambo hili la kuzaliwa mara ya pili. Je, ni nini Biblia inatufundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili? Wengi katika dunia leo wamesikia kuhusu kuzaliwa mara ya pili lakini hawajui hata kidogo jambo hili linamaanisha nini. Pia, kuna wengi ambao wanadai kwamba wao wenyewe wamezaliwa mara ya pili, lakini hata hawa hawajui jambo hili linamaanisha nini.

Katika Biblia, jambo hili la kuzaliwa mara ya pili ni jambo kuu sana. Kwa hivyo ni lazima sana tufahamu jambo hili la kuzaliwa mara ya pili linamaanisha nini. Ni lazima tufahamu jambo hili ili tuweze kujua kama kweli sisi tumezaliwa mara ya pili, na pia sisi tuweze kuwasaidia wengine kuzaliwa mara ya pili.

2. Pili, nimeandika kitabu hiki kuhusu kuzaliwa mara ya pili kwa sababu ninataka wale ambao wamezaliwa mara ya pili wafahamu ni nini Mungu amefanya ndani yao. Vile tumeona, kuna wengi ambao wamezaliwa mara ya pili lakini hawafahamu hii inamaanisha nini. Mungu Roho Mtakatifu amefanya kazi kuu sana ndani yao, lakini wao hawaelewi ni nini Mungu amefanya. Kuzaliwa mara ya pili ni jambo kuu sana, na sisi hatuwezi kuelewa kila kitu kuhusu kuzaliwa mara ya pili kwa sababu hii ni kazi kubwa sana ya Mungu. Lakini Biblia inatufundisha mengi kuhusu kuzaliwa mara ya pili na wengi ambao wamezaliwa mara ya pili hawajui ni nini Biblia inafundisha. Hata baada ya kufahamu mengi katika Biblia kuhusu kuzaliwa mara ya pili tunaweza kusema tu, "Tunaona taswira kama ya kwenye kioo" (1 Wakorintho 13:12). Kwa hivyo ni maombi yangu kwamba baada

ya kusoma kitabu hiki wewe utafahamu mengi kuhusu kuzaliwa mara ya pili.

Kuna sababu tatu ni kwa nini ninataka wale ambao wamezaliwa mara ya pili wafahamu ni nini imefanyika ndani yao.

(i) Kwanza, ninataka ufahamu ni nini imefanyika ndani mwako kwa sababu wakati unazaliwa mara ya pili na unapoendelea kukua katika imani yako, utakuwa na uhusiano na Mungu ambao ni mtamu sana, na utakuwa na hakika kwamba kweli Mungu anakupenda na amekuokoa.

(ii) Pili, ikiwa utafahamu vizuri inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili, utaona utukufu wa Mungu na wa Yesu Kristo na wa Roho Mtakatifu na wa neno la Mungu. Utapenda zaidi sana Mungu na neno lake ukifahamu vizuri ni nini Mungu alifanya wakati wewe ulizaliwa mara ya pili.

(iii) Tatu, ikiwa utafahamu ni nini Mungu alifanya ndani mwako wakati wewe ulizaliwa mara ya pili, utaona kwamba hii ilikuwa kazi kuu sana ya Mungu. Wengi leo ambao wamezaliwa mara ya pili hawaelewi kwamba Mungu amefanya kazi kuu sana na kwa hivyo hawa hawaishi maisha ya kufuata utakatifu. Lakini wakati utafahamu kwamba Mungu amefanya kazi kuu sana ndani mwako wakati wewe ulizaliwa mara ya pili, basi utaanza kufuata utakatifu kwa moyo wako wote kwa sababu utafahamu vizuri kazi ya Mungu. Ni maombi yangu kwamba wakristo wote wataishi yale maisha ambayo yanamtukuza Mungu ili watu wa dunia wafahamu vizuri maisha ya ukristo ni ya aina gani.

3. Tatu, nimeandika kitabu hiki kwa sababu kuna mamilioni ya watu hapa ulimwenguni ambao hawajaokoka. Wao hawajazaliwa

mara ya pili na kwa hivyo hawamfuati Bwana wetu Yesu Kristo na kumhudumia. Ni maombi yangu kwamba Mungu atatumia kitabu hiki kuwaonyesha watu hawa njia ya kuokoka, na kwamba Yeye atawaokoa. Kuna wengi ambao wanahudhuria kanisa kila wiki lakini hawajaokoka, na pia kuna wale ambao ni viongozi wa makanisa ambao hawajaokoka. Wao wanawaza kwamba wameokoka kwa sababu walizaliwa katika jamii za ukristo na wamehudhuria kanisa tangu utotoni mwao, lakini haya yote hayamaanishi kwamba wameokoka. Ukristo wao ni wa nje tu, ni wa kuwaonyesha wengine tu kwamba wao ni watu wa Mungu, lakini kwa ukweli hawa hawajaokoka.

Ninataka kuwahudumia watu hawa kwa kuwaeleza ni nini inapaswa kufanywa ndani mwaao ili waokoke. Ninaomba kwamba Mungu Roho Mtakatifu atatumia neno la Mungu kuwaokoa wakati watasoma kitabu hiki. Kuzaliwa mara ya pili si kazi ya mwanadamu. Hakuna yeyote ambaye anaweza kuzaliwa mara ya pili kwa uwezo wake. Hakuna mhubiri yeyote ambaye anaweza kumwezesha mwingine azaliwe mara ya pili. Hii ni kazi ya Mungu pekee, ni Yeye anafanya kazi ndani yetu ili tuzaliwe mara ya pili.

Kila wakati Mungu anafanya kazi yake ili mtu fulani azaliwe mara ya pili, anatumia neno lake. Petro anasema, “Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai...Hili neno lililohubiriwa kwenu” (1 Petro 1:23-25). Kwa hivyo Biblia hapa inatufundisha kwamba ni Mungu mwenyewe anafanya kazi ndani ya mtu ili mtu huyu azaliwe mara ya pili, na kwamba wakati Mungu anafanya kazi hii, anatumia neno lake, yaani injili ambayo sisi tunahubiri. Kwa hivyo ni maombi yangu kwamba Mungu atatumia mafundisho ya kitabu hiki kuwaokoka wale ambao hawajaokoka. Ninataka kufundisha wazi kabisa kuzaliwa mara ya pili inamaanisha nini, ili wote waelewe.

**Mpangilio wa kitabu hiki.**

Kitabu hiki kina sehemu tano, na katika kila sehemu nitauliza na kujibu swali moja.

***Sehemu ya kwanza: Je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili?***

Je, ni nini inafanyika ndani ya mtu wakati yeye anazaliwa mara ya pili? Je, ni nini inabadilika ndani yake wakati yeye anazaliwa mara ya pili? Je, ni maisha gani anaanza kuishi anapozaliwa mara ya pili? Kuzaliwa mara ya pili ni jambo muhimu sana na ni muhimu sana tufahamu vizuri jambo hili. Kwa hivyo katika sehemu hii ya kwanza tutaona majibu ya maswali mengi kama haya:

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu anatuita katika ufalme wake: "Wale aliowaita pia akawahesabia haki" (Warumi 8:30).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili ni kiumbe kipya: "Kwa hiyo mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya" (2 Wakorintho 5:17).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu anatuvuta kwake: "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu kama asipovutwa na Baba aliyenituma" (Yohana 6:44).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu aliwapa watu wake kwa Kristo: "Wale wote anipao Baba watakuja Kwangu" (Yohana 6:37).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu anafungua mioyo yetu: "Bwana akaufungua moyo wake akaupokea ujumbe wa Paulo" (Matendo ya Mitume 16:14).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu ameifanya nuru yake ing'ae mioyoni mwetu: "Yeye ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo" (2 Wakorintho 4:6).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu ataondoa moyo wa jiwe na kuweka moyo wa nyama badala yake: "Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama" (Ezekieli 36:26).

Je, Biblia inamaanisha nini wakati inasema kwamba Mungu atatufanya tuwe hai: "Hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu" (Waefeso 2:5).

Je, ni nini Biblia inamaanisha wakati inasema kwamba Mungu anafanya sisi tuwe watoto wake: "Mlipokea roho ya kufanywa wana, ambaye kwa Yeye twalia, 'Abba, yaani, Baba'" (Warumi 8:15).

***Sehemu ya pili: Je, ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili?***

Yesu Kristo alimwambia Nikodemo, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:7). Yesu hakusema, "Ikiwa unaweza kuzaliwa mara ya pili, basi utapata faida nyingi, lakini usijali sana kuhusu jambo hili." Yeye hakusema kitu kama hicho, bali alisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili." Je, ni kwa nini ni lazima tuzaliwe mara ya pili? Je, ni kwa nini Yesu alisema, "Mtu hawezi kuuona ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3)? Haya ni maswali muhimu sana na tutapata majibu ya maswali haya katika sehumu ya pili ya kitabu hiki.

Kuna wengi ulimwenguni leo ambao hawajazaliwa mara ya pili, na hii ni kwa sababu wao hawafahamu kwamba ni lazima

wazaliwe mara ya pili. Wao wanawaza kwamba hawana taabu kubwa na kwamba wanaweza kuendelea na maisha yao bila kuzaliwa mara ya pili. Wao hawafahamu kwamba mtu hana budi kuzaliwa mara ya pili. Mafundisho ya Biblia kwamba tunahitaji kuzaliwa mara ya pili yanaonyesha kwamba sisi wanadamu tuko na taabu kubwa mioyoni mwetu. Ikiwa mtu anaumwa na mguu na anaenda kwa daktari, na daktari anamwambia kwamba mguu wake unapaswa kukatwa, yeye atafahamu kwamba ako na taabu kubwa. Vile vile Biblia inasema kwamba moyo wetu unahitaji kuondolewa na tunahitaji moyo mpya uwekwe badala yake. Hii inatuonyesha kwamba tuko na taabu kubwa ndani yetu, na hii ndiyo sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili.

***Sehemu ya tatu: Je, ni namna gani mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili?***

Je, ni nini Mungu anafanya wakati anafanya mtu azaliwe mara ya pili? Biblia inatufundisha wazi kwamba ni Mungu pekee ambaye anaweza kufanya sisi tuzaliwe mara ya pili. Je, ni namna gani Mungu anafanya kazi hii? Tutaona majibu ya maswali haya katika sehemu hii ya tatu.

***Sehemu ya nne: Je, ni kwa nini Mungu hutufanya sisi tuzaliwe mara ya pili?***

Wakati Mungu anatufanya sisi tuzaliwe mara ya pili, anatuokoa. Je, ni kwa nini Mungu anatuokoa? Je, ni kwa kusudi gani anafanya kazi hii?

***Sehemu ya tano: Je, ni namna gani tunaweza kuwasaidia wengine wazaliwe mara ya pili?***

Tumeona kwamba ni Mungu pekee ambaye anaweza kutufanya tuzaliwe mara ya pili, lakini je, ni nini sisi tunafaa kufanya ili tuwasaidie wengine wazaliwe mara ya pili?

Hizi ni sehemu tano za kitabu hiki: katika kila sehemu tutauliza swali fulani na kupata majibu lake kutoka kwa Biblia.

**Ni kwa nini unahitaji sana kusoma na kujifunza kitabu hiki.**

Ni lazima sana tufahamu vizuri ni nini Biblia inafundisha kuhusu jambo hili la kuzaliwa mara ya pili. Jambo hili linahusu mbinguni na jahanum. Ni mapenzi ya Mungu kwamba watu wake waishi maisha matakatifu hapa ulimwenguni, na kwa hivyo ni lazima tufahamu vizuri ni nini Biblia inafundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili.

Vile tumeona, kuna wengi leo ambao wanadai wamezaliwa mara ya pili, lakini ukichunguza maisha yao, utaona kwamba wao wanaishi tu kama watu wa dunia. Lakini Biblia inasema kwamba hii haiwezekani: "Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4). Ni maoni yangu kwamba kuna mamilioni ya watu ambao wanadai wamezaliwa mara ya pili na wanahudhuria kanisa kila wiki, lakini kwa ukweli wao hawajazaliwa mara ya pili. Wao wamechanganyikiwa kuhusu ni nini Biblia inafundisha kuhusu jambo hili na kwa hivyo hawaelewi kabisa kuhusu wokovu wao.

Kwa kusema hivi, mimi sisemi kwamba yule ambaye ameokoka hana dhambi yoyote sasa na kwamba yeye amekamilika. Ninajua kwamba dhambi bado iko ndani mwetu, na kwamba hata yule ambaye ameokoka miaka mingi sana bado ana dhambi ndani yake, na anahitaji kila siku kupigana vita dhidi ya dhambi. Pia ninajua kwamba kuna wale ambao wameokoka lakini bado wako na dhambi nyingi sana ndani mwao, na kuna wakati ambapo watu wa dunia wanaonekana kuwa wazuri zaidi kuliko wale ambao wameokoka. Hii ni kwa sababu wale ambao wameokoka mara mingi walikuwa watu wabaya sana na kazi ya Mungu ya kuwakamilisha inaendelea pole pole ndani mwao. Pia hii ni kwa

sababu kuna wale ambao hawajaokoka lakini wanaishi maisha mazuri sana kwa nje, na wanaonekana kuwa watu wazuri sana, ingawa wao ni wauasi dhidi ya Mungu. Hii ndiyo sababu kuna wale ambao hawajaokoka lakini wanaonekana kwamba wanaishi maisha mazuri kuliko wengine ambao wameokoka.

Machoni pa Mungu kuna wale ambao wamezaliwa mara ya pili, na kuna wale ambao hawajazaliwa mara ya pili. Sisi hatuwezi kuona kwa ukweli nani amezaliwa mara ya pili na nani bado, lakini Mungu anaweza kuona haya yote. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili pengine leo anaishi maisha ya dhambi kwa sababu yeye alikuwa mwenye dhambi mkuu sana na ameokoka juzijuzi tu, na pengine yule ambaye hajaokoka anaishi maisha mazuri machoni pa watu wa dunia. Lakini yule ambaye amezaliwa mara ya pili ana Roho Mtakatifu ambaye anakaa ndani yake na yeye anaendelea kubadilika na kuwa kama Yesu Kristo mwenyewe. Ile siku Yesu Kristo atarudi yule ambaye amezaliwa mara ya pili atakuwa kamili na mtakatifu kabisa, kama Yesu Kristo mwenyewe, na yule ambaye hajaokoka, kwa nje anaonekana kwamba yeye ni mtu mzuri, lakini dhambi zake zote za siri zitahukumiwa ile siku kwa sababu yeye hajazaliwa mara ya pili.

Kwa hivyo, jambo hili ya kuzaliwa mara ya pili ni jambo kuu sana. Ni jambo kuu kwa sababu linahusu maisha ya milele na linahusu utukufu wa Yesu Kristo mwenyewe. Ikiwa mtu ataingia mbinguni milele (Yohana 3:3), na pia ikiwa watu wa Mungu hapa ulimwenguni wataishi maisha matakatifu ya kumletea Mungu utukufu (Mathayo 5:16), basi lazima tufahamu kuzaliwa mara ya pili ni nini.

Kazi ya kutufanya tuzaliwe mara ya pili ni kazi ya Mungu, na Mungu ametufundisha wazi katika neno lake kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Hii ni kwa sababu yeye anataka tufahamu vizuri kuzaliwa mara ya pili inamaanisha nini. Wakati Yesu Kristo alimwambia Nikodemo, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili,”

(Yohana 3:7), alimwambia jambo hili kwa sababu alitaka Nikodemo ajue njia ya kupata uzima wa milele. Ni maombi yangu kwamba wale ambao wanasoma kitabu hiki pia watapata kujua njia ya uzima wa milele. Kuokoa mwanadamu ni kazi ya Mungu, lakini Mungu anatumia mafundisho ya neno lake kufanya kazi hii. Ninaomba kwamba Mungu atatumia mafunisho haya ya neno lake kuwaokoa wale ambao watasoma kitabu hiki, ili wao wazaliwe mara ya pili.

# Sehemu ya Kwanza
# Je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili?

Katika sehemu hii ya kwanza, tunaangazia jambo hili: je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili? Tutaona kwamba jambo hili la kuzaliwa mara ya pili linamaanisha mambo mawili. Kwanza, linamaanisha kwamba Mungu anaumba maisha ya kiroho ndani ya yule ambaye amezaliwa mara ya pili. Pili, linamaanisha kwamba yule ambaye ameokoka sasa ni kiumbe kipya.

*"Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu. Nasi ndivyo tulivyo. Sababu kwa nini ulimwengu haututambui, ni kwa kuwa haukumtambua Yeye. Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. Kila mmoja mwenye matumaini haya katika Yeye hujitakasa, kama vile Yeye alivyo mtakatifu.*

*Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala ndani Yake hamna dhambi. Kila mtu akaaye ndani Yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi hakumwona Yeye wala hakumtambua.*

*Watoto wadogo, mtu ye yote na asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki. Yeye atendaye dhambi ni wa Iblisi, kwa sababu Iiblisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi ya Ibilisi. Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu. Kwa jinsi hii tunaweza kujua dhahiri watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi nao. Ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake".*

1 Yohana 3:1-10

# Jambo la kuzaliwa mara ya pili ni jambo muhimu sana

Yesu alimwambia Nikodemo, “Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili” (Yohana 3:3). Maneno haya ya Yesu yako na maana kwa wanadamu wote ulimwenguni, si Nikodemo peke yake. Sisi sote tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ikiwa tunataka kuuona Ufalme wa Mungu. Hii inamaanisha kwamba ikiwa wewe hujazaliwa mara ya pili, wewe hujaokoka na haumo katika jamii ya Mungu na hutaingia mbinguni, bali utaenda jahanum ukifa. Hii ndiyo sababu Yesu alisema, “Ye yote anayemwamini Mwana ana uzima wa milele, lakini yeye asiyemwamini Mwana hatauona uzima, bali ghadhabu ya Mungu itakuwa juu yake” (Yohana 3:36). Hili si jambo la kucheka-cheka, Yesu hapa anafundisha kuhusu mambo muhimu sana. Anafanya hivyo kwa sababu anatupenda na anataka sisi tuelewe ukweli kuhusu kuzaliwa mara ya pili vizuri.

Nikodemo alikuwa mfarisayo. Mafarisayo walikuwa watu wa dini sana na walikuwa viongozi wa watu wa Israeli katika mambo ya dini. Yesu aliwaambia Mafarisayo, “Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, wanafiki! Ninyi mnasafiri baharini na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja agueke na kuwafuata ninyi, lakini baada ya kumpata, mnamfanya mwana wa jehanam mara mbili kuliko ninyi...Ninyi nyoka, ninyi uzao wa nyoka wenye sumu! Mtaiepukaje hukumu ya jehanam?” (Mathayo 23:15;33). Haya maneno yanaoneysha kwamba jambo hili la kuzaliwa mara ya pili ni muhimu sana. Mafarisayo walikuwa watu wa dini sana na kwa nje walionekana kwamba wao ni watu wazuri na watu wa Mungu. Lakini hawa, hawakuwa wamezaliwa mara ya pili na kwa hivyo Yesu Kristo anasema hapa kwamba wao walikuwa waovu kabisa. Yesu Kristo anasema hapa kwamba hata kama mtu ni mtu wa dini sana na anaonekana kuwa mtu wa Mungu kwa nje, haya yote

hayajalishi. Hata yeye anahitaji kuzaliwa mara ya pili. Hadi mtu azaliwe mara ya pili yeye hawezi kuona Ufalme wa Mungu.

**Jambo la kuzaliwa mara ya pili linaweza kuwasumbua watu wengine sana.**

Katika sura hii, tunatafuta jibu la swali hili: Je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili? Kabla ya kuona jibu la swali hili, tunapaswa kufahamu kwamba jambo hili la kuzaliwa mara ya pili linaweza kusumbua watu wengi. Pengine wakati wewe unasoma kitabu hiki, unapata kwamba mafundisho ya kitabu hiki yanakusumbua sana. Kuna sababu tatu ni kwa nini mafundisho haya yanaweza kukusumbua.

1. Kwanza, mafundisho ya Yesu Kristo kuhusu kuzaliwa mara ya pili yanaweza kutusumbua sana kwa sababu mafundisho haya yanatuonyesha kwamba sisi ni wenye dhambi wakuu sana na hakuna chochote ambacho tunaweza kufanya kujiokoa. Kabla ya mtu kuzaliwa mara ya pili, yeye amekufa kiroho. Hii inamaanisha kwamba yeye hujijali tu na hawajali wengine na yeye ni mwuasi dhidi ya Mungu. Pia hii inamaanisha kwamba yeye ana hatia mbele ya sheria ya Mungu, na kwa hivyo yeye ako chini ya hasira na hukumu ya Mungu.

Wakati Yesu Kristo anasema kwamba sisi tunahitaji kuzaliwa mara ya pili, anamaanisha kwamba hali yetu kabla ya kuzaliwa mara ya pili ni mbaya sana. Anamaanisha kwamba sisi hatuna uwezo wa kutii neno la Mungu kwa sababu dhambi imetuharibu kabisa na sisi tuko na hatia mbele zake. Hii ndiyo sababu ya kwanza mafundisho ya Biblia kuhusu kuzaliwa mara ya pili yanasumbua watu wengi.

2. Pili, mafundisho ya Biblia kuhusu kuzaliwa mara ya pili yanasumbua watu wengine kwa sababu hii ni kazi ambayo Mungu anafanya ndani mwetu, si kazi ambayo sisi wenyewe tunaweza

kujifanyia. Biblia inasema, "Hawa watoto wamezaliwa si kwa damu wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu" (Yohana 1:13). Ni Mungu mwenyewe ambaye anatuwezesha kuzaliwa mara ya pili: "Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Kwa rehema zake kuu ametuzaa sisi mara ya pili" (1 Petro 1:3). Sisi hatuwezi kuzaliwa mara ya pili kwa uwezo wetu, hakuna chochote ambacho tunaweza kufanya ili tuzaliwe mara ya pili, ni Mungu pekee ambaye anatuzaa mara ya pili.

Hii inamaanisha kwamba matendo yetu mazuri na kazi zetu za dini haziwezi kutuwezesha kuzaliwa mara ya pili. Mtu anaweza kuenda kanisani kila wiki na kuimba nyimbo nyingi na kuomba maombi mengi na pia kuhubiri sana, lakini haya yote hayawezi kumsaidia kuzaliwa mara ya pili. Ni Mungu peke yake anaweza kufanya kazi hii.

Mafundisho haya yanaweza kusumbua watu wengine kwa sababu yanawafundisha kwamba wao hawana uwezo kabisa katika jambo hili la kuzaliwa mara ya pili. Tunaambiwa kwamba hatuwezi kuona Ufalme wa Mungu bila kuzaliwa mara ya pili, na tunaambiwa kwamba hakuna chochote tunaweza kufanya ili tuzaliwe mara ya pili.

3. Mafundisho haya kuhusu kuzaliwa mara ya pili yanawasumbua watu wengine kwa sababu hakuna chochote tunaweza kufanya kumlazimisha Mungu azae mtu fulani mara ya pili. Biblia inasema kwamba kuzaliwa mara ya pili ni kazi ya Mungu pekee, na ni Mungu pekee anachagua ni nani atamzaa mara ya pili. Yaani hakuna chochote ambacho mtu anaweza kufanya ili Mungu amzae mara ya pili. Biblia inasema kwamba sisi sote tumekufa katika mambo ya kiroho na sisi sote ni wenye dhambi. Pia inatuambia kwamba sisi sote tuko chini ya ghadhabu ya Mungu (Waefeso 2:3). Biblia inatufundisha kwamba kwa sababu sisi sote ni wenye dhambi hatuwezi kuona utukufu wa Kristo katika injili, na hatutaki kumtukuza Kristo (2 Wakorintho 4:4). Haya yote yanamaanisha

kwamba sisi hatuna upendo wa kuzaliwa mara ya pili, hakuna yeyote ambaye anataka kuzaliwa mara ya pili, sisi sote tunapenda tu dhambi zetu. Kwa hivyo ni uamuzi wa Mungu na chaguo la Mungu ni nani atazaliwa mara ya pili, sisi wenye dhambi hatuwezi kumlazimisha Mungu amzae mara ya pili mtu fulani.

**Tumaini langu.**

Tumaini langu katika kitabu hiki ni kufundisha kutoka kwa Biblia kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha nini. Mimi ninajua kwamba kuna wale ambao wamezaliwa mara ya pili ambao wanasoma kitabu hiki. Ninataka kuwafundisha vizuri ni nini Mungu amefanya ndani mwao ili wao waweze kufurahia katika wokovu wao na pia kumhudumia Mungu kwa mioyo yao yote. Pia ninajua kwamba kuna wale ambao hawajazaliwa mara ya pili ambao wanasoma kitabu hiki. Pengine wao wamechanganyikiwa kwamba wamezaliwa mara ya pili, lakini kwa ukweli hawajazaliwa mara ya pili. Ninataka kuwafundisha ninyi inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili ili mweze kuenda kwake Mungu na kumwomba awazae ninyi mara ya pili. Nina tumaini Mungu atafanya vile ameandika katika neno lake: “Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema” (Waefeso 2:4-5). Mungu anapenda sana kuonyesha utukufu wake katika kazi yake ya kuwaokoa watu wake. Mungu anapenda sana wakati watu wake wanamhubiri Yesu Kristo ili wote waje kwake na kuokoka. Ni maombi yangu kwamba Yesu Kristo atainuliwa katika kitabu hiki na wengi wataokoka wakisoma kitabu hiki.

**Mpangilio wa sehemu hii.**

Katika sehemu hii ya kitabu hiki, tunauliza swali hili: je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili? Biblia inatupatia majibu matatu ya swali hili:

1. Kwanza, Biblia inatufundisha kwamba kile kinafanyika wakati mtu anazaliwa mara ya pili si kwamba mtu huyu anakuwa mtu wa dini kwa uwezo wake, bali Mungu huwa amempatia maisha mapya.

2. Pili, Biblia inatufundisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anayo maisha ya Yesu Kristo moyoni mwake.

3. Tatu, Biblia inatufundisha kwamba yule ambaye ameokoka amekuwa kiumbe kipya. Hii inamaanisha kwamba yeye bado ni yule ambaye alikuwa zamani, lakini pia yeye sasa ni mtu mpya, yeye amesamehewa na kuoshwa na yeye sasa ni kiumbe kipya, ameumbwa na Roho Mtakatifu mwenyewe.

Katika sura ifuatavyo tutaangazia kwa uangalifu haya mambo matatu.

# Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kupewa maisha mapya kutoka kwa Mungu

Yule ambaye amezaliwa mara ya pili amepewa uzima upya kutoka kwa Mungu. Yeye si yule ambaye amedai kuokoka na kwa hivyo ameanza kuwa mtu wa dini na mtu mwema mbele za watu wa dunia. Kuna wengi leo ambao wanawaza kwamba mtu akitaka kuokoka, yeye kwanza anahitaji kuamua kuokoka halafu anahitaji kuanza kuhudhuria kanisa na kuanza kuishi maisha mema mbele za watu wa dunia ili watu wa duina waone kwamba yeye amebadilika. Kuna wengi ambao wanafanya hivyo, lakini wao hawajazaliwa mara ya pili, bali wamejaribu tu kwa nguvu zao kuwa watu wa dini. Hii si kuzaliwa mara ya pili.

Katika Biblia tunasoma maneno haya:

> "Basi palikuwa na mtu mmoja Farisayo, jina lake Nikodemo, mmoja wa Baraza la Wayahudi lililotawala. Huyu alimjia Yesu usiku akamwambia, 'Rabi, tunajua kuwa Wewe ni mwalimu uliyetumwa na Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya miujiza hii uifanyayo Wewe, kama Mungu hayuko pamoja naye.' Yesu akamjibu, 'Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" (Yohana 3:1-3).

Katika kifungu hiki Yohana anatuambia kwamba Nikodemo alikuwa Mfarisayo na pia alikuwa mtawala wa Wayahudi. Mafarisayo walikuwa watu ambao walifuata dini kwa uangalifu sana katika nchi ya Israeli. Yesu alimwambia Mfarisayo huyu, "Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" (mstari 3), na tena, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili" (mstari 7). Kwa kusema hivi, Yesu anamwambia Nikodemo, "Ninajua kwamba wewe ni Mfarisayo na kwamba

wewe unajua neno la Mungu vizuri sana na unawafundisha wengine neno la Mungu na wewe ni mtu ambaye anafuata dini kwa uangalifu sana. Lakini ingawa unafanya haya yote, wewe huna budi kuzaliwa mara ya pili."

Yesu hapa anasema kwamba mtu ambaye anataka kuokoka na kuingia mbinguni, hahitaji kuwa mtu wa dini bali anahitaji kuzaliwa mara ya pili. Wakati mwanamke anazaa, analeta maisha mapya hapa ulimwenguni, na sisi pia tunahitaji maisha mapya y a kiroho. Nikodemo alikuwa na maisha ya kimwili: alikuwa anapumua na kuwaza na kusihi na kutenda matendo. Haya yote Nikodemo aliweza kufanya kwa sababu alikuwa na uhai wa kimwili na aliumbwa katika mfano wa Mungu mwenyewe. Lakini Yesu hapa anamfundisha Nikodemo kwamba yeye amekufa kwa sababu yeye hakuwa na uhai wa kiroho, katika mambo ya kiroho yeye bado hakuwa amezaliwa. Nikodemo alikuwa mtu wa dini na mwalimu wa neno la Mungu lakini yeye alihitaji kuzaliwa mara ya pili, alihitaji kuokoka.

Katika Biblia tunasoma kumhusu mtu mmoja ambaye alitaka kumfuata Yesu Kristo, lakini kwanza alitaka kumzika babake. Yesu Kristo alimwambia, "Waache wafu wazike wafu wao" (Luka 9:60). Yesu hapa alimaanisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili, kazi yake kuu ni kuhubiri Kristo, wala si kushughulika na mambo ya mazishi. Wacha wale ambao hawajazaliwa mara ya pili washughulike na mazishi. Hii haimaanishi kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili hawafai kuhudhuria mazishi, bali kazi yao kuu ni kuhubiri Kristo na si kuzika watu. Katika mfano wa mwana mpotevu, wakati mwana alirudi nyumbani, babake alisema, "Huyu mdogo wako alikuwa amekufa na sasa yu hai" (Luka 15:24).

Kuna wengi leo ambao wako hai katika miili yao lakini katika mambo ya kiroho wamekufa kwa sababu hawajazaliwa mara ya pili. Wengi wao wanahudhuria kanisa kila wiki na wanaonekana

kwamba wako hai kiroho kwa sababu wanafanya mambo mengi kanisani. Wengi wao ni waimbaji wazuri, wanaomba na wanahubiri. Haya yote wanafanya kwa sababu wako na nguvu katika miili yao, lakini katika mambo ya kiroho wamekufa.

Nikodemo alikuwa mtu wa dini na mwalimu wa neno la Mungu na kiongozi wa watu wa Israeli, lakini katika mambo ya kiroho alikuwa amekufa, yeye hakuwa amezaliwa mara ya pili na kwa hivyo yeye hakuwa ameokoka. Yeye alikuwa na uhai katika mwili wake, lakini hakuwa na uhai katika roho yake. Mtu anapata uhai katika roho yake wakati anazaliwa mara ya pili. Wakati anazaliwa mara ya pili, anapata uzima ndani ya moyo wake.

Kwa hivyo kuzaliwa mara ya pili ni kupewa uzima moyoni na Mungu.

# Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha haitoshi kujua tu kwamba Yesu Kristo ni Bwana, bali kupata maisha ya kiroho kutoka kwake

Kuna wengi duniani ambao wanajua Yesu Kristo ni nani na kwamba yeye alikuja hapa ulimwenguni kuwaokoka wenye dhambi. Kuna wale ambao wanajua kwamba alikufa juu ya msalaba kwa ajili ya wenye dhambi na kwamba wale ambao watamwamini wataokoka. Lakini kujua haya mambo yote haiwezi kuokoa mtu yeyote. Nikodemo alimwambia Yesu Kristo, "Rabi, tunajua kuwa Wewe ni mwalimu uliyetumwa na Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya miujiza hii uifanyayo Wewe, kama Mungu hayuko pamoja naye" (Yohana 3:2). Hii inamaanisha kwamba Nikodemo alisikia mafundisho ya Yesu Kristo na aliona matendo yake na yeye alijua kwamba Yesu Kristo ametoka kwa Mungu mwenyewe. Yeye aliona kwamba Yesu Kristo alifanya kazi ya Mungu hapa ulimwenguni. Lakini kujua haya yote haimaanishi kwamba yeyealikuwa amezaliwa mara ya pili. Yesu hakumwambia Nikodemo, "Kweli wewe unajua mambo mengi kunihusu, kwa hivyo ni wazi kwamba wewe umezaliwa mara ya pili." Bali Yesu alimwambia, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huwezi kuona Ufalme wa Mungu usipozaliwa mara ya pili."

Yale ambayo Yesu anafundisha hapa ni ya muhimu sana. Mtu anaweza kuhudhuria kanisa kila wiki, lakini hii haimaanishi kwamba yeye amezaliwa mara ya pili. Mtu anaweza kusikia mahubiri kutoka kwa neno la Mungu kila wiki na kuamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu ambaye alikuja hapa ulimwenguni kuwaokoa watu wake, lakini hii haimaanishi kwamba yeye amezaliwa mara ya pili. Kuamini yale ambayo Biblia inafundisha peke yake haimaanishi kwamba mtu amezaliwa mara ya pili.

Pia, mtu anaweza kuona miujiza na kuamini kwamba miujiza hii imetoka kwa Mungu, lakini hii haimaanishi kwamba yeye amezaliwa mara ya pili. Nikodemo alijua kwamba Yesu Kristo ametoka kwa Mungu kwa sababu yeye aliona matendo yake Yesu Kristo na kuamini kwamba kweli yeye ametoka kwa Mungu. Lakini hii haimaanishi kwamba Nikodemo alikuwa amezaliwa mara ya pili. Yeye bado alihitaji kuzaliwa mara ya pili, na hii ndiyo sababu Yesu Kristo alimwambia, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili” (Yohana 3:7).

Mtu anaweza kusema kwa mdomo kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na awe hajazaliwa mara ya pili. Hata shetani alijua kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu (Marko 1:24).

Hii inamaanisha kwamba mtu anahitaji kupewa uzima wa kiroho moyoni mwake. Kama yeye hajapewa uzima wa kiroho kutoka kwa Mungu, basi yeye hajazaliwa mara ya pili na yeye hajaokoka. Uzima huu ambao umetoka kwa Mungu si uzima wa kawaida ambao unapatikana hapa ulimwenguni. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema, “Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho” (Yohana 3:6). Wakati tunazaliwa hapa ulimwenguni, tu hai katika miili: “Mwili huzaa mwili.” Lakini katika mambo ya kiroho sisi ni wafu. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili anao uzima wa kiroho kutoka kwa Mungu Roho Mtakatifu: “Roho huzaa roho.” Mtu anazaliwa mara ya pili wakati Roho Mtakatifu anampa uzima.

Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alimwambia Nikodemo, “Upepo huvuna po pote upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi ukafahamu utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na Roho” (Yohana 3:8). Katika mstari huu, Yesu Kristo anafundisha kuhusu Roho Mtakatifu. Biblia inatufundisha wazi kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu mwenyewe na ni yeye ambaye anamwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili. Ni Yeye peke yake ambaye anaweza kufanya kazi hii ya kumwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili. Katika mstari huu, Yesu Kristo anafundisha kwamba

kazi ya Roho Mtakatifu ni kama upepo ambao unavuma popote upendapo. Hakuna yeyote ambaye ana mamlaka juu ya upepo na hakuna yeyote ambaye anaweza kuongoza upepo na kuuambia upepo kuvuma mahali fulani. Vilevile, hakuna yeyote ambaye anatawala Roho Mtakatifu na hakuna yeyote ambaye anaweza kumwambia Roho Mtakatifu, "Enda mahali pale na mwezesha mtu fulani kuzaliwa mara ya pili." Roho Mtakatifu ni Mungu na sisi hatuwezi kumwamuru, Yeye anafanya yale ambayo Yeye ameamua kufanya. Hii ndiyo sababu hakuna mtu ambaye anaweza kutawala kazi yake ya kuwazaa watu mara ya pili.

Kwa hivyo katika kifungu hiki Yesu Kristo anafundisha Nikodemo kwamba, "Haitoshi kuamini kwamba Mimi nimetoka kwa Mungu na kwamba ninafundisha neno la Mungu na ninafanya kazi ya Mungu. Ukiamini tu mambo haya wewe hutazaliwa mara ya pili. Wewe Nikodemo unahitaji kuzaliwa mara ya pili. Na kazi hii ya kukufanya wewe uzaliwe mara ya pili ni kazi ya Roho Mtakatifu pekee: wewe huwezi kujifanya kuzaliwa mara ya pili, Mungu Roho Mtakatifu pekee anaweza kukufanya uzaliwe mara ya pili."

### Uzima ambao tunapokea kutoka kwa Mungu ni Yesu Kristo mwenyewe.

Biblia inatufundisha kwamba wakati tunapata uzima ya kiroho kutoka kwa Roho Mtakatifu tumepata uzima wa milele kupitia kwa imani ndani ya Yesu Kristo. Tumeona katika sura hii kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili, Mungu Roho Mtakatifu anapanda uzima ndani yake. Yaani, kabla ya kuzaliwa mara ya pili, yeye hakuwa na uzima wa kiroho, lakini baada ya kuzaliwa mara ya pili yeye sasa ana uzima ndani mwake. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema, "Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu" (Yohana 6:63).

Wakati tunasoma injili ya Yohana, tunapata kujua kwamba Yesu Kristo mwenyewe ndiye ule uzima ambao Roho Mtakatifu

anatupatia wakati tunazaliwa mara ya pili. Yaani tunaweza kusema kwamba wakati Roho Mtakatifu anamfanya mtu azaliwe mara ya pili, anapanda uzima ndani mwake, na uzima huu unakuja ndani ya mtu kupitia kwa Yesu Kristo. Wakati mtu anazaliwa mara ya pili, yeye anaunganishwa kwa Yesu Kristo, na anapata uzima kutoka kwa Yesu Kristo. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu" (Yohana 14:6), na pia, "Mimi ndimi mkate wa uzima" (Yohana 6:35). Na hii ndiyo sababu Yohana anaandika katika injili yake, "Lakini haya yameandikwa ili mweze kuamini ya kuwa Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu na kwa kumwamini mpate uzima katika Jina lake" (Yohana 20:31).

Kwa hivyo ikiwa mtu hajaunganishwa kwa Yesu Kristo na yeye hamwamini Yesu Kristo, basi yeye hawezi kuwa na uzima ndani mwake, yeye hajazaliwa mara ya pili. Wakati Roho Mtakatifu anamfanya mtu azaliwe mara ya pili, yeye anamwunganisha kwa Yesu Kristo. Yesu Kristo mwenyewe ni uzima; Yesu Kristo ni mzabibu wa kweli ambaye anawapatia watu wake uzima, kama vile mti unapatia matawi maisha. Yeye ni mzabibu na sisi ni matawi (Yohana 15:1-17). Wakati mtu anazaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu anapanda uzima upya ndani mwake kwa kupitia kwa Yesu Kristo, au tunaweza kusema kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili ni kama mtu amechukua tawi ambalo lilikuwa limekufa na kuliweka kwa mti hadi tawi hilo linashikana na mti vizuri sana na linaanza kupata maisha kutoka kwa mti ule.

Kwa hiyo wakati mtu anazaliwa mara ya pili, anaanza kumwamini Yesu Kristo. Biblia inatufundisha kwamba uzima wa kiroho na imani ndani ya Yesu Kristo haya mawili yanakuja pamoja. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili atamwamini Yesu Kristo na kwa kumwamini Yesu, atapata uzima wa milele ndani ya moyo wake. Kwa hivyo kuzaliwa mara ya pili na kumwamini Yesu Kristo kwa wokovu wetu yanatendeka wakati moja.

**Kuzaliwa mara ya pili na kumwamini Yesu Kristo.**

Biblia inasema, "Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4). Yaani hapa Biblia inatufundisha kwamba yule ambaye anataka kuushinda ulimwengu na dhambi anahitajika kuzaliwa mara ya pili. Pia, inatufundisha kwamba yule ambaye anataka kuushinda ulimwengu anahitaji kuwa na imani ndani ya Yesu Kristo. Tunaona kwa hivyo kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anayo imani ndani ya Yesu Kristo. Wakati mtu anazaliwa mara ya pili anapewa uzima upya, na uzima huu ni uzima wa imani.

Hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Huu ndio ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima" (1 Yohana 5:11-12), na hii ndiyo sababu Yesu alisema, "Roho ndiye atiaye uzima" (Yohana 6:63), na pia, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:5,8), na hii ndiyo sababu Yohana anasema, "Kumwamini mpate uzima" (Yohana 20:31). Mistari hii yote inamaanisha kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu anapanda uzima ndani yake na kumwunganisha kwa Yesu Kristo kupitia kwa imani, kwa sababu Yesu Kristo ndiye uzima.

Kwa hivyo wakati tunawaza kuhusu kuzaliwa mara ya pili, tunapaswa kukumbuka maneno haya mawili: "Mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3), na, "Ye yote anayemwamini Mwana anao uzima wa milele" (Yohana 3:36). Wakati mtu anapozaliwa mara ya pili, anapata uzima ambao umepandwa ndani mwake wakati anaunganishwa kwa Bwana Yesu Kristo. Mungu anafanya kazi hii kwa kumpa huyu mtu imani ndani ya Yesu Kristo, hii ndiyo njia mtu anaunganishwa kwa Bwana Yesu Kristo.

Sura ya Nne

# Kuzaliwa mara ya pili kunamaansiha kuwa kiumbe kipya

Katika sura hii, tunaendelea kuona ni nini inafanyika wakati mtu anazaliwa mara ya pili. Yesu Kristo alimwambia Nikodemo, "Usishangae nimekuambia 'Huna budi kuzaliwa mara ya pili'" (Yoahana 3:7). Pia Kristo alimwambia Nikodemo, "Amin, amin nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3). Kwa kusema hivi, Yesu alimaanisha kwamba sisi sote tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ikiwa tutaingia mbinguni. Kwa hivyo jambo hili la kuzaliwa mara ya pili ni jambo la muhimu sana, si lile jambo la nje tu, bali ni jambo la kazi ya Mungu ndani ya moyo wa mwanadamu. Kuzaliwa mara ya pili si kama mtu ambaye anatayarisha mwili kabla ya kuuzika. Sisi sote tunajua kamba wakati mwili unatayarishwa kuzikwa, watu wanauvalisha mwili huo nguo mpya na kuufanya mwili huo uonekane mzuri sana. Lakini hata kama mwili huo una nguo mpya, na unaonekana mzuri sana, bado umekufa: hauna maisha yoyote ndani yake, umekufa. Vilevile, kuna watu ambao wanadai kwamba wameokoka, lakini kwa ukweli wao ni kama mwili ambao umetayarisha kuzikwa. Kwa nje wanaonekana kuwa wakristo wazuri sana lakini hii ni kama nguo mzuri tu ambayo umewekwa juu ya mwili ambao hauna maisha. Mtu huyu hajaokoka, ukristo wake ni wa nje tu. Mtu ambaye amezaliwa mara ya pili atapata kwamba uzima upya umeumbwa ndani yake.

Katika sehemu hii ya kwanza ya kitabu hiki tunatafuta jibu la swali hili: je, ni nini inafanyika wakati mtu anazaliwa mara ya pili? Tayari, tumeona mambo mawili: tumeona katika sura ya pili ya kitabu hiki kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili amepewa uzima upya kutoka kwa Mungu. Halafu katika sura ya tatu ya kitabu hiki tumeona kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili, roho yake imebadilishwa na Kristo.

## Uzima upya kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Nikodemo alikuwa Mfarisayo na kwa hivyo alikuwa mtu mkuu wa dini. Lakini yeye hakuwa na maisha ya kiroho ndani mwake. Yeye aliona kazi ya Mungu katika maisha ya Yesu Kristo, lakini yeye hakujua kazi ya Mungu ya kiroho ndani mwake. Kwa hivyo, Nikodemo alihitaji uzima upya kupitia kwa kazi ya Roho Mtakatifu ndani mwake. Uzima huu wa kiroho ni uzima ambao Roho Mtakatifu mwenyewe anatupatia. Mwanadamu hawezi kujipatia uzima huu wa kiroho, uzima huu unatoka mbinguni na ni Roho Mtakatifu ambaye anampatia mwanadamu uzima huu.

Yesu Kristo alisema, "Mwili huzaa mwili, Roho huzaa roho" (Yohana 3:6). Hii inamaanisha kwamba yule ambaye hajaokoka ako na uzima katika mwili wake tu, yeye hana uzima wa kiroho moyoni mwake. Yaani, Biblia inatufundisha kwamba watu wote wa dunia wako na maisha ya mwili lakini wale tu ambao wamezaliwa mara ya pili ndiyo wana maisha ya kiroho. Mwanadamu huzaa uzima wa mwili, Roho Mtakatifu huzaa uzima wa kiroho. Ikiwa sisi hatuna uzima wa kiroho hatuwezi kuona ufalme wa Mungu.

## Uzima uko ndani ya Kristo na unakuja kwetu kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Katika sura ya tatu tuliona mambo mawili muhimu sana. Tuliona kuzaliwa mara ya pili ni kumwamini Yesu Kristo, na pia tuliona kwamba tunazaliwa mara ya pili kupitia kwa njia ya imani. Yesu Kristo alisema, "Mimi ndimi njia, ukweli na uzima" (Yohana 14:6). Mtume Yohana aliandika, "Huu ndiyo ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima" (1 Yohana 5:11-12).

Kwa hivyo ule uzima wa kiroho ambao tunauhitaji uko ndani ya Mwana wa Mungu, yaani Yesu Kriso mwenyewe ni uzima. Ikiwa

wewe uko na Yesu Kristo, basi wewe uko na uzima wa kiroho, yaani uzima wa milele. Pia, Yesu Kristo mwenyewe alisema, "Roho ndiye atiaye uzima, mwili hufai kitu" (Yohana 6:63), na tena, "Amin, amin nakuambia, hakuna mtu ye yote anayeweza kuingia katika Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho" (Yohana 3:5).

Kwa hivyo yule ambaye amezaliwa mara ya pili anao uzima wa kiroho kwa sababu yeye ameunganishwa kwa Mwana wa Mungu ambaye ni uzima wetu, na pia uzima huu unakuja kutoka kwa Roho Mtakatifu. Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba wakati Roho Mtakatifu anafanya kazi ya kumwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili, anampa yule mtu uzima kwa kumwunganishwa kwa Yesu Kristo. Njia nyingine ya kusema hii ni kwamba tunaunganishwa kwa Yesu Kristo kupitia kwa Roho Mtakatifu.

Pia tumeona kwamba Biblia inasema kwamba wakati tunaamini, tunapata uzima katika Jina Lake (Yohana 20:31). Tunasoma katika Biblia, "Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4). Kwa ufupi, tunaweza kusema kwamba Roho Mtakatifu anatupatia uzima kwa kutuunganisha kwa Yesu Kristo kupitia kwa imani ndani yake.

Sasa katika sura hii, ninataka kuendelea kuangalia swali hili, ni nini inafanyika wakati mtu anazaliwa mara ya pili. Jambo la tatu ambalo linafanyika ni kwamba mtu huyu sasa ni kiumbe kipya. Hii inamaanisha kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili na kuokoka, kuna kazi kubwa sana ya Mungu ambayo imefanyika ndani mwake. Kuna wengi ambao wameacha dhambi fulani hapa na pale, na kuanza kuhudhuria kanisa na wanawaza kwamba wameokoka. Lakini haya mambo yote ambayo wamefanya ni ya nje tu; hakuna kazi ya Mungu ndani mwao; wao wamefanya mambo fulani hapa na pale kwa uwezo wao tu. Hii si kuzaliwa mara ya pili.

Yule ambaye amezaliwa mara ya pili sasa ni kiumbe kipya. Yeye bado ni mtu yule yule ambaye alikuwa kabla ya kuzaliwa mara ya pili, lakini sasa yeye ameumbwa upya na yeye sasa ni kiumbe kipya. Yeye sasa amesamehewa dhambi zake zote, ameoshwa kutoka kwa uchafu wa dhambi zake na utu upya sasa unaendelea kua ndani yake kwa sababu ya kazi ya Roho Mtakatifu ndani mwake.

Wakati tunasoma mafundisho ya Yesu Kristo katika kitabu cha Yohana, tunaona mafundisho haya yote. Yesu Kristo alimfundisha Nikodemo, "Amin, amin nakuambia, hakuna mtu ye yote anayeweza kuingia katika Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho" (Yohana 3:5). Je, Yesu anamaanisha nini wakati anaongea kuhusu "maji na Roho"? Kuna wale ambao wanaamini kwamba Yesu Kristo hapa anaongea kuhusu ubatizo. Wao wanaamini kwamba wakati mtu anabatizwa, basi dhambi zake zote zinaoshwa na yeye anaokoka. Lakini ni wazi kwamba Biblia haifundishi hii.

**Ni namna gani tunajua kwamba Yesu hapa hafundishi kuhusu ubatizo.**

Tunajua bila shaka kwamba Yesu hapa hafundishi kuhusu ubatizo wakati anasema, "Hakuna mtu ye yote anayeweza kuingia katika Uflame wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho" (Yohana 3:5). Hii ni kwa sababu hizi:

Kwanza, tunajua kwamba Yesu hapa hafundishi kuhusu ubatizo kwa sababu mara mingi katika sura hii Yesu anafundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili lakini haongei kuhusu ubatizo. Ikiwa ubatizo ni lazima kwa mtu kuzaliwa mara ya pili, Yesu angefundisha kuhusu ubatizo wazi kabisa katika sura hii, kwa sababu katika sura hii yeye anafundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili.

Katika sura hii ya Yohana 3, wakati Yesu anafundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili, Yeye anasema hii: "Kila mtu amwaminiye awe na uzima wa milele" (Yohana 3:15), na, "Ye yote amwaminye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa" (Yohana 3:18). Ikiwa mtu lazima abatizwe ili aokoke, je, ni kwa nini Yesu hakufundisha jambo hili katika mistari hii?

Pili, wakati Yesu Kristo aliongea na Nikodemo, alisema, "Upepo huvuma po pote upendapo. Mvumo wake unausikia lakini huwezi ukafahamu utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa na Roho" (Yohana 3:8). Yaani hapa Yesu anasema kwamba kumfanya mtu azaliwe mara ya pili ni kazi ya Mungu, na Mungu anachagua ni nani atazaliwa mara ya pili, na lini atazaliwa mara ya pili. Lakini ikiwa mtu anazaliwa mara ya pili wakati anabatizwa, basi hili si chaguo la Mungu, bali ni chaguo la yule mtu.

Tatu, wakati tunasoma maneno ya Yesu akiongea na Nikodemo, yeye alisema, "Wewe ni mwalimu mashuhuri wa Waisraeli, na wewe huelewi mambo haya?" (Yohana 3:10). Yaani hapa Yesu anamwambia Nikodemo, "Mambo haya yote ambayo ninakufundisha yanapatikana katika Agano la Kale. Wewe ni mwalimu wa Agano la Kale, mbona hujui mambo haya?" Sasa, ikiwa Yesu katika kifungu hiki anafundisha kwamba mtu anazaliwa mara ya pili wakati anabatizwa, je, ni namna gani Nikodemo anaweza kujua hii? Jambo hili halifundishwi katika Agano la Kale, ni namna gani mwalimu wa Agano la Kale angeweza kujua ubatizo ni nini?

Kwa hivyo, wakati Yesu alisema, "Hakuna mtu ye yote ambaye anaweza kuingia katika Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho" (Yohana 3:5), tunajua kwa hakika kwamba yeye haongei kuhusu ubatizo. Kwa hivyo, je, ni nini Kristo alimaanisha wakati alisema, "Hakuna mtu ye yote ambaye anaweza kuingia katika Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho" (Yohana 3:5)?

Jibu la swali hili linapatikana katika Agano la Kale. Hii ndiyo sababu Yesu alimwambia Nikodemo, “Wewe ni mwalimu mashuhuri wa Waisraeli, na wewe huelewi mambo haya?” (Yohana 3:10). Yale ambayo Yesu anafundisha hapa yanapatikana katika Agano la Kale, na hii ndiyo sababu Yesu alitarajia kwamba Nikodemo angejua ni nini alikuwa akifundisha.

### Mafundisho ya Ezekieli sura ya 36 kuhusu kuzaliwa mara ya pili.

Katika sura hii, nabii Ezekieli anawafundisha watu wa Israeli ni nini Mungu atawafanyia watu wake wakati wao watarudi kwao kutoka kwa nchi ya Babeli. Mafundisho haya ya Ezekieli 36 yalihusu watu wa Israeli katika Agano la Kale na pia yanahusu watu wa Mungu leo kwa sababu sisi ni watu wa Mungu wa Agano Jipya kupitia kwa damu yake Yesu Kristo. Yesu Kristo alifundisha kwamba wale wote wameokoka kupitia kwa damu Yake wako katika Agano Jipya na Mungu (Luka 22:20). Wakati tunasoma vifungu kama Ezekieli 36:24-28 na Yeremia 31:31-34, tunaona ni nini Mungu anawaahidi wale ambao watakuwa watu wake katika Agano Jipya.

> “Kwa kuwa nitawaondoa ninyi toka katika mataifa, nitawakusanya kutoka katika nchi zote na kuwarudisha kwenye nchi yenu wenyewe. Nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi, nitawatakasa kutoka katika uchafu wenu wote na kutoka katika sanamu zenu zote. Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama. Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate amri zangu na kuwafanya kuwa waangalifu kuzishika sheria zangu. Mtaishi katika nchi niliyowapa baba zenu, nanyi mtakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu” (Ezekieli 36:24-28).

Wakati Yesu Kristo alimwambia Nikodemo, “Hakuna mtu ye yote ambaye anaweza kuingia katika Ufalme wa Mungu

isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa Roho" (Yohana 3:5), alikuwa akifundisha mafundisho ya kifungu hiki cha kitabu cha Ezekieli. Katika kifungu hiki cha Ezekieli, Mungu anasema, "nanyi mtakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu." Je, Mungu hapa anamaanisha watu gani? Jibu ni kwamba anamaanisha wale ambao Yeye mwenyewe atawaosha: "Nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi, nitawatakasa kutoka katika uchafu wenu wote na kutoka katika sanamu zenu zote" (mstari 25). Pia, watu wa Mungu ni wale ambao Yeye mwenyewe amewapa mioyo mipya: "Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama" (mstari 26). Yaani, Yesu Kristo hapa anafundisha kwamba wale ambao wataingia Ufalme wa Mungu ni wale ambao wameoshwa kutoka kwa dhambi na wamefanywa watu wapya.

Kwa hivyo, wakati Ezekieli anaongea kuhusu "maji na roho" anamaanisha kwamba haya mambo mawili yatafanywa kwa yule ambaye ataokoka: yeye ataoshwa kutoka kwa uchafu wa dhambi zake, na yeye atafanywa mtu mpya, yaani, kiumbe kipya. Hii inamaanisha kwamba yule ambaye ameokoka ni yule yule tu ambaye alikuwa kabla ya kuokoka, lakini yeye sasa ni mtu mpya; yeye si mtu mwingine, yeye ni mtu yule yule tu, lakini sasa yeye ni mtu mpya. Hii ndiyo sababu yeye anahitaji kuoshwa. Kama yeye si mtu yule yule ambaye alikuwa kabla ya kuokoka, hakuna haja ya kumtakasa.

Tunajua kwamba Biblia inasema utu wetu wa zamani ulisulibiwa (Warumi 6:6) na kwamba sisi tumekufa pamoja na Kristo (Wakolosai 3:3) na kwamba Biblia inatuambia, "Jihesabuni wafu" (Warumi 6:11) na pia kwamba watu wa Mungu wanaamrishwa "Kuuvua mwenendo wenu wa zamani" (Waefeso 4:22). Lakini haya yote hayamaanishi kwamba yule ambaye ameokoka si yule yule tu ambaye aliishi kabla ya kuokoka. Mafundisho haya yote yanamaanisha kwamba kulikuwa na utu wa zamani na tabia za

zamani na mwenendo wa zamani, na kwamba haya yote yanapaswa kuondolewa kabisa.

Kwa hivyo yule ambaye ameokoka ana moyo mpya, roho mpya na utu upya, lakini yeye ni yule yule tu na kwa hivyo anahitaji kusamehewa na kuoshwa. Hii ndiyo sababu Biblia hapa inaongea kuhusu maji. Hatia yetu inahitaji kuoshwa na kuoshwa na maji ni mfano wa namna gani Mungu anatuosha katika damu ya Yesu Kristo. Biblia inasema, "Nitawatakasa dhambi zote walizofanya dhidi yangu na nitawasamehe dhambi zote za uasi dhidi yangu" (Yeremia 33:8). Yule ambaye anataka kuokoka anahitaji kusamehewa na hatia yake inahitaji kuondolewa.

**Tunahitaji kuwa watu wapya.**

Yule ambaye anataka kuokoka anapaswa kujua kwamba, kusamehewa na kuoshwa kutoka kwa uchafu wa dhambi pekee haitoshi. Yule ambaye anataka kuokoka anahitaji kuwa mtu mpya. Yeye anahitaji kubadilishwa. Yeye anahitaji maisha mapya. Yeye anahitaji kutazama kila kitu kwa njia mpya, anahitaji kuwaza katika njia mpya na kuthamini vitu vyote kwa njia mpya. Hii ndiyo sababu Mungu anawaahidi watu wake moyo mpya na roho mpya: "Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu, nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama. Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate amri zangu na kuwafanya kuwa waangalifu kuzishika sheria zangu" (Ezekieli 36:26-27).

Mistari hii inamaanisha hivi: Yule ambaye hajaokoka anao moyo wa jiwe. Moyo wake hauwezi kufahamu mambo ya kiroho. Moyo wa mtu ambaye hajaokoka unaweza kupenda mambo mengi ya ulimwengu, lakini hauwezi kupenda mambo ya kiroho. Yeye hawezi kuona uzuri wa Yesu Kristo na utukufu wa Mungu na njia ya utakatifu. Hii ndiyo sababu yule ambaye hajaokoka anahitaji moyo wake ubadilishwe.

Wakati Mungu anamzaa mtu mara ya pili, Mungu anaondoa moyo wake wa jiwe na kuweka ndani yake moyo mpya. Wakati unabii wa Ezekieli unaongea kuhusu moyo wa nyama, unamaanisha ule moyo ambao unaweza kupokea neno la Mungu na kulifahamu. Huu ni moyo ambao unaweza kuja kwa Mungu na kulitii neno lake.

Halafu wakati unabii wa Ezekieli unasema, "Nitaweka roho mpya ndani yenu...Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu" (Ezekieli 36:26-27), unabii huu unaongea kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Wakati mtu anaokoka, Mungu anaweka ndani yake maisha ya kiroho na haya maisha ya kiroho ni Roho Mtakatifu mwenyewe ambaye anafanya kazi ndani mwake akimbadilisha ili awe kama Kristo mwenywe.

Yaani, tunaweza kusema kwamba moyo wa yule ambaye ameokoka ni kama matope ambayo yanaweza kufinywa, na Roho Mtakatifu anaubadilisha moyo wake pole pole, hadi yule mtu anabadilika kabisa na kuwa kama Yesu Kristo (Waefeso 4:23).

**Mafundisho haya ya kuzaliwa mara ya pili kwa jumla.**

Katika sura hizi nne tumeona ni nini Mungu anatufundisha kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Tumeona kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu anafanya kazi Yake ndani ya huyu mtu wa kumleta kwa Kristo ili yeye aweze kuwa ndani ya Kristo kupitia kwa imani. Yaani, tunaweza kusema kwamba Roho Mtakatifu anamweka mtu ndani ya Kristo kwa sababu ndani Yake yeye anaweza kupata kuoshwa kutoka kwa uchafu wa dhambi zake. Pia, Yesu Kristo anaondoa moyo wake wa jiwe na kuweka moyo mpya ndani yake ili yeye sasa aweze kuwa mtu mpya. Kwa hivyo huyu mtu sasa atakuwa bila hatia ya dhambi zake zote na pia atakuwa mtu mpya ambaye anapenda kufanya mapenzi ya Mungu (Ezekieli 36:27).

Katika kitabu hiki, nitakufundisha mambo mengi mengine kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Ikiwa wewe hujaokoka, basi usingoje hadi umepata mafundisho haya yote: kuja kwake Kristo leo na umpokee ili uweze kuokoka kutoka kwa dhambi zako. Biblia inasema, “Wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale waliaminio Jina Lake” (Yohana 1:12).

# Sehemu ya Pili

# Je, ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili?

*"Kwa habari zenu, mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu, ambazo mlizitenda mlipofuatisha namna ya ulimwengu huu na za yule mtawala wa ufalme wa anga, yule roho atendaye kazi ndani ya wale wasiotii. Sisi sote pia tuliishi katikati yao hapo zamani, tukifuata tamaa za mwili na mawazo yake. Nasi kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu, kama mtu mwingine ye yote. Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema. Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, ili katika ule ulimwengu ujao apate kuonyesha wingi wa neema Yake isiyopimika, iliyodhihirishwa kwetu kwa wema Wake ndani ya Kristo Yesu. Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala hii si kwa matendo yenu mema. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu, si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Kwa maana sisi ni kazi ya mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Kristo Yesu, ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo".*

Waefeso 2:1-10

# Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu tumekufa katika mambo ya kiroho

Yule ambaye anataka kuwa mtu wa hekima anahitaji kujua mambo mawili. Kwanza, anahitaji kujua Mungu ni nani, na pili anahitaji kujua mwanadamu ni nani. Kujijua si jambo rahisi, kwa sababu yule ambaye anataka kujijua, kwanza anahitaji kujua Mungu ni nani. Pia, kujijua si rahisi kwa sababu wengi wanawaza kwamba tayari wanajijua, lakini kwa ukweli hawajijui hata kidogo. Mtu akitaka kujua kwa ukweli kabisa yeye ni mtu wa aina gani anahitaji usaidizi kutoka kwa Mungu. Bila usaidizi wa Mungu hakuna yeyote ambaye anaweza kujijua.

### Je, ni nani anaweza kujua moyo wa mwanadamu?

Nabii Yeremia aliandika, "Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu kupita kiasi. Ni nani awezaye kuujua?" (Yeremia 17:9). Pia Daudi aliandika, "Ni nani awezaye kutambua makosa yake? Nisamehe makosa yangu nisiyoyajua" (Zaburi 19:12). Mistari hii inatufundisha kwamba sisi wanadamu hatuwezi kufahamu mioyo yetu na dhambi zetu kamili. Tunaweza kufahamu mambo machache hapa na pale kuhusu dhambi zetu lakini hatuwezi kujua hali yetu ya dhambi kamili.

Lakini hii haimaanishi hatuwezi kujua chochote kuhusu dhambi zetu. Biblia inatufundisha wazi kuhusu dhambi zetu ili tuweze kufahamu kwamba sisi sote tunahitaji mwokozi na pia ili wale ambao wameokoka waweze kuwa na furaha nyingi sana katika wokovu wao.

Vile tumeona katika kitabu hiki, Yesu Kristo alisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:7); na pia, "Mtu hawezi kuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili" (Yohana 3:3). Mistari hii inafundisha kwamba kuzaliwa mara ya pili ni jambo muhimu

sana, kwa sababu mbinguni na jahanum inategemea juu ya jambo hili. Tayari katika kitabu hiki, tumeona kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha nini. Sasa katika sehemu hii ya pili ya kitabu hiki ninataka kuona ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili.

Je, ni kwa nini ni lazima kabisa mtu azaliwe mara ya pili akitaka kuingia mbinguni? Je, ni kwa nini haitoshi kujibadilisha hapa na pale na kuacha dhambi fulani hapa na pale? Je, ni kwa nini tunahitaji kufa na kuwa hai tena na kuanza maisha yetu tena? Haya ni maswali ambayo nitajibu katika sehemu hii ya kitabu hiki.

### Tumekufa kiroho na kwa hivyo tunahitaji kuzaliwa mara ya pili.

Katika sehemu hii ninataka kufundisha kutoka kwa kitabu cha Waefeso sura ya 2. Katika kifungu hiki, Paulo anasema, “Mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu” (Waefeso 2:1); na halafu anasema, “Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema” (Waefeso 1:4-5). Kwa hivyo katika kifungu hiki mara mbili Paulo anatuambia kwamba sisi tumekufa katika dhambi zetu.

Halafu Paulo anatueleza dawa ya hali hii ni gani. Anasema Mungu “alitufanya tuwe hai” (mstari wa 5). Wale ambao wameokoka wanaweza kufahamu ukuu wa upendo wa Mungu. Wao wanajua kwamba wao walikuwa wamekufa katika dhambi zao na uovu wao na kwamba Mungu amewafanya hai kwa neema Yake na upendo wake: “Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu.” Haya yote Mungu ameyafanya kwa sababu ya upendo wake. Kwa hivyo watu wa Mungu, yaani wale ambao wameokoka, wanafahamu upendo wa Mungu kwa sababu wao wameokoka.

Wakati Paulo hapa anasema kwamba Mungu ametufanya hai, anamaanisha kwamba sisi tumezaliwa mara ya pili. Kabla ya kuokoka sisi hatukuwa hai, lakini wakati Mungu alituokoa, alituondoa kutoka kwa hali ya kifo cha kiroho. Na sasa sisi tu hai, yaani tumezaliwa mara ya pili (Yohana 3:3). Hii ndiyo sababu Kristo alisema, “Roho ndiye atiaye uzima” (Yohana 6:63).

**Upendo wa Agano Jipya.**

Kwa hivyo katika kifungu hiki, Biblia inatufundisha kwamba Mungu anatufanya tuzaliwe mara ya pili kwa sababu mbili: (i) kwa sababu ya upendo wake, (ii) kwa sababu Yeye ni Mungu wa rehema. Angalia tena vizuri ni nini Paulo aliandika katika kifungu hiki: “Lakini Mungu, (i) kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, (ii) ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu.” Huu ni upendo wa Agano Jipya. Huu ni upendo ambao Mungu anao kwa kanisa lake. Katika kitabu cha Ezekieli tunasoma kuhusu upendo huu wa Mungu kwa watu wake:

“Siku uliyozaliwa kitovu chako hakikukatwa, wala hukuogeshwa kwa maji ili kukufanya safi, wala hukusuguliwa kwa chumvi wala kufunikwa kwa nguo. Hakuna ye yote aliyekuonea huruma au kukusikitikia kiasi cha kukutendea mojawapo ya mambo haya. Badala yake, ulipozaliwa ulitupwa nje penye uwanja, kwa kuwa katika siku uliyozaliwa ulidharauliwa. Ndipo nilipopita karibu nawe nikakuona ukigaagaa kwenye damu yako, nawe ulipokuwa umelala hapo penye hiyo damu nikakuambia, ‘Ishi!’ Nilikufanya uote kama mmea wa shambani. Ukakua na kuongezeka sana, ukawa kito cha thamani kuliko vyote. Matiti yako yakatokeza na nywele zako zikaota, wewe uliyekuwa uchi na bila kitu cho chote. Baadaye nikapita karibu nawe, nilipokutazama na kukuona kuwa umefikia umri wa kupendwa, nililitandaza vazi langu juu yako na kuufunika uchi wako. Nikakuapia na kuingia kwenye agano na wewe, asema Bwana Mwenyezi, nawe ukawa wangu” (Ezekieli 16:4-8).

Yaani hapa Biblia inatufundisha kwamba Mungu aliona kwamba watu wake walikuwa wafu, na kwa hivyo alitoa Mwana wake afe kwa ajili yao ili wao waweze kuwa hai. Na baada ya kuwafanya hai na kuwaokoa, Yeye huwalinda milele. Hii ndiyo maana ya meneno ya Yesu Kristo hapa: "Nami ninawapa uzima wa milele, hawataangamia kamwe wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka katika mikono Yangu" (Yohana 10:28).

Kwa hivyo, swali ambalo tunahitaji kuuliza ni hili, je, inamaanisha nini kwamba wale ambao hawajaokoka wamekufa? Kufa kirohoni kunamaanisha nini? Katika Agano Jipya, tunapata majibu kumi ya swali hili. Wakati tunaangalia haya majibu kumi na kuwaza juu yake, tutanyenyekezwa sana na pia tutashangazwa sana kuhusu kazi ya Mungu ya kutufanya tuzaliwe mara ya pili. Kwa hivyo katika sura hii na ile ambayo inafuata ninataka kuangalia haya mambo kumi ili tufahamu, je, inamaanisha nini kusema wale ambao hawajazaliwa mara ya pili wamekufa kiroho?

Halafu, baada ya kuangalia haya mambo kumi, tutaona ni kwa nini sisi tunahitaji kuzaliwa mara ya pili na kubadilishwa kutoka ndani kabisa. Vile tumeona hapa mbeleni, Biblia inafundisha wazi kwamba yule ambaye anataka kuokoka, anahitaji kusamehewa dhambi zake zote, na pia anahitaji kuzaliwa mara ya pili, yaani anahitaji kubadilishwa kabisa kutoka ndani mwake. Je, ni kwa nini anahitaji mabadilisho haya ndani mwake? Je, ni kwa nini haitoshi tu kusamehewa dhambi zake zote? Hili ni swali ambalo tunajibu katika sura hii.

1. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili amekufa katika dhambi na makosa (Waefeso 2:1-2).***

Kufa kunamaanisha kuwa bila uhai. Yule ambaye hajaokoka anao uhai wa mwili na anayo dhamira, lakini yeye hana uhai katika mambo ya kiroho. Katika Waefeso 2:1-2, Paulo anasema kwamba wao ambao hawajaokoka wanatembea njia ya dhambi

na kufuata dunia. Pia anasema katika kifungu hiki kwamba wao wako na tamaa za mwili na za mawazo. Hii inamaanisha kwamba yule ambaye hajazaliwa mara ya pili amekufa lakini ana uwezo wa kutenda dhambi. Yeye amekufa na kwa hivyo hawezi kuona na kufahamu utukufu wa Kristo. Yeye amekufa kwa mambo ya kiroho, yeye hana uwezo wa kupokea Mungu na Kristo na neno lake. Katika Agano Jipya, tunapata mafundisho mengine kuhusu hali hii ya kufa kiroho, na ninataka kueleza jambo hili hapa.

2. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili ni mwana wa ghadhabu (Waefeso 2:3).***

Paulo anaandika, "Sisi sote pia tuliishi katikati yao hapo zamani, tukifuata tamaa za mwili na mawazo yake. Nasi kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu" (Waefeso 2:3). Paulo hapa anasema kwamba taabu ya yule ambaye hajaokoka ni kwamba matendo yake ni maovu, na pia kwamba yeye mwenyewe ni mwana wa ghadhabu. Yaani taabu yake siyo tu matendo yake, yeye mwenyewe, yaani utu wake, ni taabu yake. Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili na anaishi maisha ya dhambi, taabu yake si wazazi wake au maadui wake au watu wengine wowote, taabu yake ni yeye mwenyewe; taabu yake imo ndani mwake.

Yaani, Biblia haifundishi kwamba yeye wakati alizaliwa alikuwa bila dhambi na kwamba alianguka dhambini baadaye na akawa mtu mbaya. Bali, Biblia inasema, "Hakika mimi nilizaliwa mwenye dhambi, mwenye dhambi tangu nilipotungwa mimba kwa mama yangu" (Zaburi 51:5). Sisi sote tulizaliwa wenye dhambi; utu wetu ni utu wa dhambi. Kila mmoja wetu ni mwenye dhambi tangu kuzaliwa: kila mmoja anajijali na ni mtu wa kutaka, na pia wakati tunatenda mabaya, tunawashtumu wengine. Wakati unaposoma hii, ikiwa unawaza, "Ndiyo ninawajua watu kama hawa," basi hii inamaanisha wewe mwenyewe umedanganywa na huwezi kuona ukweli huu. Yule

ambaye anasoma maneno ya Biblia kuhusu hali ya mwanadamu hapaswi kuwachunguza wengine bali anapaswa kujichunguza na kujinyenyekeza.

Paulo anasema kwamba wale ambao hawajaokoka ni "wana wa ghadhabu." Hii inamaanisha kwamba ghadhabu ya Mungu ni mali yetu, kama tu watoto ni mali ya mzazi. Sisi ni wenye dhambi wakuu sana mbele ya Mungu na ni watu ambao ni waovu mbele zake. Hii ndiyo sababu Yeye ana hasira na ghadhabu juu yetu.

3. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili anapenda giza na kuchukia nuru (Yohana 3:19-20).***

Yesu Kristo alisema, "Hii ndiyo hukumu kwamba: Nuru imekuja ulimwenguni, nao watu wakapenda giza kuliko nuru kwa sababu matendo yao ni maovu. Kwa kuwa kila atendaye maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili matendo yake maovu yasifichuliwe" (Yohana 3:19-20).

Maneno haya ya Yesu Kristo yanatueleza hali ya yule ambaye hajaokoka. Wakati nuru ya neno la Mungu inamjia, yeye huipuuza. Pia wakati giza inamjia yeye anaishika na moyo wake wote. Yaani yule ambaye hajaokoka anapenda ile ambayo anapaswa kuchukia na anachukia ile ambayo anapaswa kupenda.

4. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili, moyo wake ni mgumu kama jiwe (Ezekieli 36:26; Waefeso 4:18).***

Vile tumeona katika sura iliyopita, unabii wa Ezekieli unasema, "Nitaondoa ndani yenu moyo wenu wa jiwe na kuwapa moyo wa nyama" (Ezekieli 36:26). Katika waraka wa Waefeso, Paulo anatueleza ni kwa nini yule ambaye hajaokoka anapenda giza na kuchukia nuru: "Watu hao akili zao zimetiwa giza na

wametengwa mbali na uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga wao na ugumu wa mioyo yao” (Waefeso 4:18).

Yaani Paulo hapa anasema kwamba yule ambaye hajaokoka anapenda giza na kuchukia nuru si kwa sababu yeye hajui giza ni nini na nuru ni nini, bali kwa sababu moyo wake ni mgumu sana. Paulo anasema kwamba yule ambaye hajaokoka hupinga ukweli wa Mungu (Warumi 1:18). Yaani yule ambaye hajaokoka na ako katika giza, yeye ako katika hali hii si kwa sababu yeye hajui nuru ni nini au si kwa sababu yeye hajui njia ya kuokoka, bali ni kwa sababu moyo wake ni mgumu na unapinga ukweli wa Mungu.

5. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kumtii Mungu au kumpendeza (Warumi 8:7-8).***

Paulo aliandika, “Ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu wala haiwezi kuitii. Wale wanaotawaliwa na mwili, hawawezi kumpendeza Mungu” (Warumi 8:7-8). Yaani hapa Paulo anasema kwamba nia ya yule ambaye hajaokoka ni uadui dhidi ya Mungu kwa sababu haitii sheria ya Mungu. Pia Paulo anasema kwamba nia yake huyu mtu haina uwezo wa kumtii na kumpedeza Mungu.

Halafu Paulo anaongea na wale ambao wamezaliwa mara ya pili na kusema, “Lakini ninyi hamtawaliwi na mwili, bali na Roho wa Mungu anayekaa ndani yenu” (Warumi 8:9). Yaani Paulo hapa anasema kwamba kuna tofauti kuu sana kati ya wale ambao wameokoka na wale ambao hawajaokoka. Anasema kwamba wale ambao wameokoka hawatawaliwi na dhambi bali wanaongozwa na Roho Mtakatifu, lakini wale ambao hawajaokoka wanaongozwa na dhambi ambayo iko ndani ya utu wao. Ni kama vile Yesu alisema, “Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho” (Yohana 3:6).

Mafundisho haya ya Biblia yanamaanisha kwamba bila Roho Mtakatifu ndani yetu, mawazo yetu yanampinga Mungu na neno lake na pia bila Roho Mtakatifu hatuna uwezo wa kulitii neno la Mungu na kutawaliwa na hili neno: "Nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu wala haiwezi kuitii." Mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili amekufa katika mambo ya kiroho na ako gizani na ni mgumu dhidi ya Mungu hadi Mungu amfanye azaliwe mara ya pili.

6. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kupokea injili (Waefeso 4:18; 1 Wakorintho 2:14).***

Katika 1 Wakorintho 2:14 Paulo anaeleza hali ya yule ambaye hajazaliwa mara ya pili. Anaeleza inamaanisha nini wakati tunasema mtu huyu ni mgumu na amekufa. Anasema, "Mtu ambaye hana Roho ya Mungu hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho ya Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa jinsi ya rohoni" (1 Wakorintho 2:14). Yaani hapa Paulo anasema kwamba yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hawezi kufahamu na kupokea mafundisho kuhusu Mungu. Pia, Paulo anasema kwamba taabu yake siyo kwamba mafundisho haya yanahitaji akili sana na elimu sana na kwamba yeye hana akili na elimu hii. Bali, Paulo hapa anasema kwamba taabu ya yule mtu ambaye hajaokoka ni kwamba wakati yeye anasikia mahubiri ya neno la Mungu yeye anawaza kwamba haya ni upuzi. Hii ndiyo sababu yeye hawezi kufahamu mafundisho ya neno la Mungu: mawazo yake hayana uwezo wa kuyashika.

Hii inamaanisha kwamba moyo wa yule mtu ambaye hajaokoka unapenda dhambi sana, na mawazo yake pia yanapenda dhambi na kutafuta njia ya kufanya dhambi. Tunaweza kusema kwamba moyo wake na mawazo yake yamejawa na dhambi; hii ndiyo sababu mafundisho ya neno la Mungu ni upuzi kwake, ni kwa sababu yeye hupenda tu dhambi.

***7. Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kuja kwake Kristo na kumpokea kuwa Bwana (Yohana 6:44, 65; 1 Wakorintho 12:3).***

Paulo anasema, "Hakuna mtu awezaye kusema, 'Yesu ni Bwana,' isipokuwa ameongozwa na Roho Mtakatifu" (1 Wakorintho 12:3). Yaani hapa Paulo anasema kwamba yule ambaye hajaokoka hawezi kusema kwa moyo wake wote kwamba Yesu Kristo ni Bwana. Kuna wengi ambao wanaweza kusema tu kwa midomo, "Yesu ni Bwana," lakini haya ni maneno tu. Hakuna yeyote ambaye anaweza kusema kutoka kwa moyo wake kwamba Yesu Kristo ni Bwana wa maisha yake hadi Roho Mtakatifu atamwezesha. Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kumpokea Kristo na neno lake katika maisha yake na kumfuata kwa moyo wake wote.

Yesu Kristo anafundisha mara tatu katika Yohana sura ya 6 kwamba hakuna yeyote ambaye anaweza kuja kwake hadi Mungu Baba mwenyewe amvute. Na wakati Mungu anamvuta mtu fulani kuja kwa Kristo yeye anazaliwa mara ya pili. Haya ni mafundisho ya Kristo: "Wale wote anipao Baba watakuja Kwangu" (Yohana 6:37); "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu kama asipovutwa na Baba aliyenituma" (Yohana 6:44); "Hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba Yangu" (Yohana 6:65). Mungu Baba anawavuta watu na kuwapa uwezo kuja kwa Kristo wakati anawawezesha kuzaliwa mara ya pili. Bila kazi ya Mungu kutuwezesha kuzaliwa mara ya pili hakuna yeyote ambaye anaweza kuja kwake kwa sababu hakuna yeyote ambaye anataka kuja kwake bila kuvutwa na Mungu. Hii ndiyo sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili: ni kwa sababu mapenzi yetu na tamaa yetu yanahitaji kubadilishwa.

### Aina mbili ya matokeo.

Katika Waefeso 2:4-5 Paulo anaandika, "Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema,

hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema."

Kuna matokeo ya aina mbili kwa mistari hii. Mtu mmoja anaweza kusema, "Je, haya yote yanawezaje kufanywa? Je, ni namna gani Mungu anafanya haya yote?" Mtu mwingine atasema, "Mungu ameniongoza kusoma sura hii leo. Mungu ameongea nami kutoka mistari hii. Nimeona kwamba kweli ninahitaji sana rehema na upendo na neema ya Mungu." Kwa hivyo mtu huyu atamwomba Mungu, "Ee Mungu, ninapokea neema yako kwa sababu Wewe mwenyewe kupitia kwa neema Yako umeniamsha na kuniwezesha kupokea neno lako." Ashukuriwe Mungu kwa rehema yake na upendo wake na kwa nguvu za neema Yake.

*"Tunawajulisha lile lilokuwako tangu mwanzo, lile tulilosikia,ambalo tumeliona kwa macho yetu, ambalo tumelitazama na kuligusa kwa mikono yetu, kuhusu Neno la Uzima, Uzima huo ulidhihirishwa, nasi tumeuona na kuushuhudia, nasi twawatangazieni uzima wa milele, ambao ulikuwa pamoja na Baba, nao ukadhihirishwa kwetu. Twawatangazia lile tuliloliona na kulisikia ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe Yesu Kristo. Tunaandika mambo haya ili furaha yetu ipate kuwa timilifu.*

*Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka Kwake na kuwatangazia ninyi, kwamba Mungi ni nuru na ndani yake hamna giza lo lote. Kama tukisema kwamba twashirikiana naye huku tukienda gizani, wasema uongo,wala hatutendi lililo kweli. Lakini tikienenda nuruni, kama Yeye alivyo nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu, Mwana Wake yatusafisha dhambi yote. Kama tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani yetu. Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote. Kama tukisema hatukutenda dhambi, twamfanya Yeye kuwa mwongo na Neno Lake halimo ndani yetu".*

1 Yohana 1:1-10

# Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu sisi ni watumwa wa dhambi na shetani

Katika sura ya tano, tulianza kuangalia jibu la swali hili: Je, ni kwa nini tunahitaji uzaliwa mara ya pili? Katika ile sura ya tano tulisoma Waefeso 2:4-5, ambayo inasema, “Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema.” Yaani katika kifungu hiki, Paulo anasema kwamba Mungu alifutanya kuwa hai au Mungu alitufanya tuzaliwe mara ya pili. Paulo anatufundisha katika kifungu hiki kwamba sisi tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu bila kuzaliwa mara ya pili tumekufa katika makosa na dhambi zetu.

Hii ndiyo sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili, ni kwa sababu tunahitaji uhai wa kiroho. Bila kuzaliwa mara ya pili hatuwezi kuona uzuri wa Kristo na hatuwezi kumthamini. Ni yule tu ambayo amezaliwa mara ya pili ambaye anaweza kusema, “Nayahesabu mambo yote kuwa hasara tupu nikiyalinganisha na faida kubwa ipitayo kiasi ya kumjua Kristo Yesu Bwana wangu” (Wafilipi 3:8).

Kwa hivyo, katika sura ya tano, tuliangalia kufa katika mambo ya kiroho kunamaanisha nini. Tuliona kwamba Agano Jipya linasema kwamba kufa kiroho kunamaanisha mambo kumi, na katika sura ya tano tuliona mambo saba ya haya mambo kumi, yaani,

1. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili amekufa katika dhambi na makosa.*

2. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili ni mwana wa ghadhabu.*

3. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili anapenda giza na kuchukia nuru.*

4. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili, moyo wake ni mgumu kama jiwe.*

5. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kumtii Mungu au kumpendeza.*

6. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kupokea injili.*

7. *Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana uwezo wa kuja kwake Kristo na kumpokea kuwa Bwana.*

Sasa katika sura hii, ninataka kueleza yale mambo matatu ambayo yamebaki. Kumbuka kwamba ninkufundisha inamaanisha nini kufa katika makosa na dhambi, ili uelewe vizuri hali yako ya ukweli mbele za Mungu. Ninataka kukufundisha mambo haya ili wakati unaokoka, utafahamu vizuri ni nini Mungu amefanya kukuokoa na kwa hivyo utamshukuru kwa furaha sana. Mtu hawezi kumshukuru Mungu kwa moyo wake wote kwa wokovu wake hadi yeye afahamu hali yake kabla ya kuokoka ilikuwa gani.

8. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili ni mtumwa wa dhambi (Warumi 6:27).***

Katika mstari huu, Paulo anamshukuru Mungu kwa sababu Mungu alimwondoa kutoka kwa utumwa wa dhambi. Paulo

anaandika, “Lakini Mungu ashukuriwe kwa kuwa ninyi ambao kwanza mlikuwa watumwa wa dhambi, mmekuwa watii kutoka moyoni kwa mafundisho mliyopewa” (Warumi 6:17).

Yule mtu ambaye amezaliwa mara ya pili, kabla ya kuzaliwa mara ya pili aliipenda sana dhambi na hakutaka kuacha dhambi zake au kuziua. Halafu yeye alizaliwa mara ya pili. Mungu alimwezesha kupata maisha mapya ya kiroho na utu upya ambao unachukia sana dhambi na kupenda utakatifu. Hii yote ni kazi ya Mungu, na hii ndiyo sababu Paulo anamshukuru Mungu na si mwanadamu: “Mungu ashukuriwe kwa kuwa ninyi ambao kwanza mlikuwa watumwa wa dhambi, mmekuwa watii kutoka moyoni kwa mafundisho mliyopewa.” Sisi sote ni watumwa wa dhambi na tunaendelea katika utumwa huu hadi Mungu anatuamsha na kutupatia uhai. Halafu, baada ya kuzaliwa mara ya pili, tunakuwa na moyo wa kuua dhambi na kuwa watu watakatifu. Hii ndiyo sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili.

9. ***Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili ni mtumwa wa shetani (Waefeso 2:1-2; 2 Timotheo 2:24-26).***

Hili ndilo mojawapo ya mambo mabaya sana kuhusu hali yetu. Wale ambao hawajaokoka wamekufa kiroho kwa Mungu na neno lake lakini wao hawajakufa kwa shetani, bali wanamfuata. Angalia tena jinsi Paulo anaongea kuhusu wale ambao hawajaokoka: “Mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu, ambazo mlizitenda mlipofuatisha namna ya ulimwengu huu na za yule mtawala wa ufalme wa anga, yule roho atendaye kazi ndani ya wale wasiotii” (Waefeso 2:1-2). Mistari hii inamaanisha kwamba yule ambaye hajaokoka, tamaa zake na jinsi anavyofanya uamuzi wake, haya yote yanaambatana na “yule mtawala wa ufalme wa anga,” yaani shetani.

Shetani ni adui wa wanadamu wote na ni lengo lake kuyaharibu maisha ya watu wote. Hii ndiyo sababu Paulo aliandika, “Tena

haimpasi mtumishi wa Bwana kuwa mgomvi, bali inampasa awe mwema kwa kila mtu, awezaye kufundisha, tena mvumilivu. Inampasa kuwaonya kwa upole wale wanaopingana naye, kwa matumaini kwamba Mungu atawajalia kutubu na kuijua kweli, ili fahamu zao ziwarudie tena, nao waponyoke katika mtego wa shetani ambaye amewateka wapate kufanya mapenzi yake" (2 Timotheo 2:24-26). Katika kifungu hiki Paulo anaomba kwamba Mungu atawajalia wale ambao hawajaokoka kutubu na kuijua kweli. Haya ndiyo mambo ambayo yanatendeka wakati mtu anazaliwa mara ya pili, na hii ndiyo njia watumwa wa shetani wanaweza kuondolewa kutoka utumwa huu: Mungu anawajalia kutubu, yaani Mungu anawaamsha ili wao waweze kuona hatari na ubaya wa dhambi na kuona uzuri na thamani ya Kristo. Ukweli huu unamruhusu mtu kutoka kwa utumwa wa dhambi.

Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili anacheza-cheza na dhambi kwa sababu hajui hili ni jambo la hatari sana. Lakini wakati anazaliwa mara ya pili, anaamka na kuona kwamba kumbe ni dhambi ambayo anacheza nayo, na kwa hivyo anaiacha kwa haraka.

***10. Yule ambaye hajazaliwa mara ya pili hana chochote kizuri ambacho kinakaa ndani mwake (Warumi 7:18).***

Wakati yule ambaye hajazaliwa mara ya pili anasoma jambo hili anaweza kushangaa sana. Pengine yeye atasema, "Ni kweli kwamba mimi sijazaliwa mara ya pili, lakini mimi ni mtu mwema na ninafanya mambo mengi mazuri hapa ulimwenguni. Mimi sifanyi mambo mengi mabaya mabaya kama watu wengine wengi." Kuna wengi ambao wanawaza hivyo, lakini tunahitaji kukumbuka kwamba Biblia inasema ikiwa mtu hajazaliwa mara ya pili, basi yeye hana chochote kizuri ndani mwake. Hii ni kwa sababu yule ambaye hajaokoka hafanyi mambo yote maishani mwake kwa kumtegemea Mungu na kwa utukufu wake.

Kwa hivyo kuna vitu vingi hapa ulimwenguni ambavyo Mungu

ameviumba kwa utukufu wake, kama mwili wa mwanadamu na vitu kama ndoa, jamii, serikali na biashara. Haya ni mambo ambayo Mungu mwenyewe ameyaumba na Mungu ameyaumba kwa utukufu wake. Na Mungu anatuamuru kwamba tumpende kwa mioyo yetu yote na kwa nafsi zetu zote (Mathayo 22:37). Hii inamaanisha kwamba Mungu anataka tumtegemee wakati tunatumia haya mambo yote kama ndoa na serikali na biashara ili tuonyeshe thamani Yake (1 Petro 4:11). Lakini wale ambao hawajazaliwa mara ya pili hawatumii mambo haya ambayo Mungu ameyaumba kwa kumtegemea na kwa kuonyesha thamani Yake, na kwa hivyo wale ambao hawajazaliwa mara ya pili huharibu vile vitu ambavyo Mungu ameviumba.

Kwa hivyo wakati Paulo anaandika, "Kwa maana ninafahamu hakuna jema lo lote likaalo ndani yangu, yaani, katika asili yangu ya dhambi" (Warumi 7:18), yeye anamaanisha hakuna lolote jema ambalo lilikaa ndani yake kabla ya yeye kuokoka. Baada ya yeye kuokoka, kulikuwa na vitu vingi ambavyo vilikuwa vizuri ambavyo vilikaa ndani yake. Utu wake ulikuwa upya na hii ni nzuri, Roho Mtakatifu alikaa ndani yake na Yeye ni mzuri, yeye alikuwa na imani ndani yake ambayo ni nzuri, na yeye alikua katika ukristo wake na hii pia ni nzuri. Lakini kabla ya yeye kuzaliwa mara ya pili vitu hivi vyote havikuwa ndani yake na kwa hivyo yeye hakuwa na lolote jema ndani yake.

**Mafundisho ya sura ya tano na sita kwa ufupi.**

Kwa hivyo tumeona Bibia inamaanisha nini wakati inasema kwamba wale ambao hawajazaliwa mara ya pili wamekufa kiroho. Tumeona kwamba hii inamaansiha mambo kumi na tumeyachunguza haya mambo yote. Paulo aliwaandikia wakristo wa Efeso, "Kumbukeni kwamba wakati ule mlikuwa hamna Kristo, mkiwa wageni katika jumuiya ya watu wa Mungu, yaani Israeli na wageni katika lile agano la ahadi, mliishi duniani mkiwa hamna tumaini wala Mungu" (Waefeso 2:14). Kwa ufupi,

hii ni hali ya wote ambao hawajazaliwa mara ya pili. Hii ndiyo sababu sisi sote tunahitaji kuzaliwa mara ya pili. Bila kuzaliwa mara ya pili sisi hatuwezi kuwa na tumaini lolote na hatuwezi kujiokoa kwa kuacha dhambi fulani fulani hapa na pale. Wale ambao wamekufa hawawezi kurekebisha hali yao, bali wale ambao wamekufa wanahitaji kitu kimoja tu: kuwa hai. Wale ambao hawajazaliwa mara ya pili wanahitaji kitu kimoja tu: kuzaliwa mara ya pili.

# Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu tutapata faida nyingi

Katika sura ya tano na sita, tulitazama swali hili: Je, ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili? Na tumeona kwamba tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu sisi ni wenye dhambi ambao tumekufa katika dhambi zetu na makosa yetu. Tumeona kwamba tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ili tuweza kuwa na uhai na ili tuweze kufahamu uzuri na thamani ya Yesu Kristo na ili tuweze kuja kwake kwa wokovu. Hii ndiyo ni sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili: kwa sababu tumekufa katika dhambi na makosa na hatuna uhai wa kiroho ndani mwetu.

Sasa katika sura hii, ninataka kuuliza swali lingine, ambalo ni hili: ikiwa mtu atazaliwa mara ya pili, je, ni faida gani atapata? Mtu akizaliwa mara ya pili, je, ni nini atapata ambayo itamfaidi katika maisha yake ya mbele na ya milele?

Kupata jibu la swali hili tunahitaji kukumbuka maneno haya ya Yesu Kristo: “Amin, amin, nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili” (Yohana 3:3). Yaani Yesu hapa anatufundisha kwamba bila kuzaliwa mara ya pili hakuna yeyote ambaye ataona Ufalme wa Mungu, yaani, bila kuzaliwa mara ya pili hakuna yeyote ambaye ataingia mbinguni, bali ataangamizwa milele. Je, ni nini tutakosa ikiwa hatutazaliwa mara ya pili? Tutakosa kila kitu kizuri milele, na badala yake, tutahukumiwa jahanum milele.

Je, ni kwa nini yule ambaye hajazaliwa mara ya pili ataenda jahanum milele? Jibu la swali hili ni kwamba bila kuzaliwa mara ya pili hatutakuwa na yale mambo ambayo tunahitaji ili tuokoke na kuingia mbinguni. Biblia inatufundisha wazi kwamba mtu akitaka kuingia mbinguni, kuna mambo fulani ambayo yeye

anahitaji kuwa nayo, na ikiwa yeye hana haya mambo fulani, basi hawezi kamwe kuingia mbinguni. Pia, Biblia inatufundisha wazi kwamba haya mambo fulani ambayo mtu anahitaji ili aingie mbinguni, yanapatikana tu wakati yeye anazaliwa mara ya pili.

1. Bila kuzaliwa mara ya pili, mtu hawezi kuwa na imani, bali atakuwa tu na kutoamini (Yohana 1:11-13; 1 Yohana 5:1; Waefeso 2:8-9; Wafilipi 1:29; 1 Timotheo 1:14; 2 Timotheo 1:3).

2. Bila kuzaliwa mara ya pili, hatuwezi kuhesabiwa haki mbele za Mungu, bali tutahukumiwa (Warumi 8:1; 2 Wakorintho 5:21; Wagalatia 2:17; Wafilipi 3:9).

3. Bila kuzaliwa mara ya pili, hatuwezi kuwa watoto wa Mungu, bali tutakuwa watoto wa shetani (1 Yohana 3:9-10).

4. Bila kuzaliwa mara ya pili, hatuwezi kuzaa matunda ya upendo kupitia kwa Roho Mtakatifu, bali tutazaa matunda ya kifo (Warumi 6:20-21; 7:4-6; 15:16; 1 Wakorintho 1:2; 2 Wakorintho 5:17; Waefeso 2:10; Wagalatia 5:6; 2 Wathesalonike 2:13; 1 Petro 1:2; 1 Yohana 3:14).

5. Bila kuzaliwa mara ya pili, hatutakuwa na furaha ya milele katika ushirika na Mungu, bali tutakuwa na huzuni milele pamoja na shetani na malaika wake (Mathayo 25:41; Yohana 3:3; Warumi 6:23; Ufunuo 2:11; 20:15).

Tunahitaji kufahamu haya mambo matano ili tuweze kujifahamu na kufahamu ukuu wa Kristo na kufahamu wokovu wetu. Haya mambo matano yanafundisha vitu hivi:

1. Wakati Mungu anamwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili, anampatia imani na kumwunganisha kwa Yesu Kristo. Biblia inasema, “Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo

amezaliwa na Mungu" (1 Yohana 5:1). Yaani Biblia hapa inasema kwamba yule ambaye ana imani ndani ya Kristo amezaliwa tena.

2. Wakati mtu anazaliwa mara ya pili na ana imani ndani ya Kristo, yeye anahesabiwa haki kupitia kwa imani ndani ya Yesu Kristo. Biblia inasema, "Kwa hivyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo" (Warumi 5:1). Wakati mtu anazaliwa mara ya pili, anapewa imani, na kupitia kwa imani, yeye hutazama Yesu Kristo na kwa hivyo anahesabiwa haki kwa sababu anamwamini Yesu Kristo pekee.

3. Wakati mtu anazaliwa mara ya pili na kupewa imani na kuunganishwa kwa Kristo, hakuna vizuizi vyovyote kati yake na Mungu kwa sababu yeye sasa amehesabiwa haki. Kwa hivyo, baada ya kuhesabiwa haki, yeye sasa atafanywa mtoto wa Mungu na atabadilishwa katika mfano wa Yesu Kristo. Biblia inasema, "Wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale waliaminiyo Jina Lake. Hawa watoto walizaliwa si kwa damu wala mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu" (Yohana 1:12-13).

4. Baada ya mtu kuzaliwa mara ya pili na kuwa mtoto wa Mungu kupitia kwa imani ndani ya Kristo na kuhesabiwa haki, yeye sasa ataanza kuzaa matunda ya upendo. Biblia inasema, "Kwa maana ndani ya Kristo, kutahiriwa au kutotahiriwa hakuleti tofauti, bali lililo muhimu ni imani itendayo kazi kwa njia ya upendo" (Wagalaita 5:6). Pia Biblia inasema, "Sisi tunajua kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda ndugu" (1 Yohana 3:14). Yule ambaye amezaliwa mara ya pili atakuwa na upendo moyoni mwake.

5. Yule amezaliwa mara ya pili na kuhesabiwa haki sasa ana Roho Mtaktifu ambaye anaishi ndani mwake, na kwa hivyo yeye sasa anaanza kuishi maisha matakatifu. Lengo lake sasa ni ushirika wa furaha na Mungu wa milele. Biblia inasema, “Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma” (Yohana 17:3). Lengo la maisha ya ukristo ni ushirika na Mungu wa milele.

Haya ni mambo ambayo yule ambaye amezaliwa mara ya pili atayapata. Kwa hivyo tunaweza kusema, yule ambaye hajazaliwa mara ya pili amekufa kiroho katika dhambi na makosa na pia yeye hatapata hizi baraka ambazo nimeziandika hapa. Hii ndiyo sababu Kristo alisema, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili” (Yohana 3:3;7).

*"Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu! Nasi ndivyo tulivyo. Sababu kwa nini ulimwengu haututambui, ni kwa kuwa haukumtambua Yeye. Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. Kila mmoja mwenye matumaini haya katika Yeye hujitakasa, kama vile Yeye alivyo mtakatifu. Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala ndani Yake hamna dhambi. Kila mtu akaaye ndani yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi hakumwona Yeye wala hakumtambua. Watoto wadogo, mtu ye yote na asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki. Yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi. Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu. Kwa jinsi hii tunaweza kujua dhahiri watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi nao. Ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake".*

1 Yohana 3:1-10

# Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili ili tuweze kufahumu ni kwa nini Kristo alikuja hapa ulimwenguni

**Kristo alikuja ulimwenguni kuondoa dhambi.**

Katika kifungu hiki cha 1 Yohana 3:1-10, tunaambiwa mara mbili ni kwa nini Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa Mungu, alikuja hapa ulimwenguni.

(i) Kwanza, Yohana anasema, “Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala ndani yake hamna dhambi” (1 Yohana 3:5). Yaani Yohana hapa anasema kwamba Yesu Kristo hakuwa na dhambi yoyote ndani yake, na pia anatuambia kwamba Yeye alikuja hapa ulimwenguni kuziondoa dhambi.

(ii) Halafu pili Yohana anasema, “Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi za Ibilisi” (1 Yohana 5:8). Wakati Yohana anaongea kuhusu “kazi za Ibilisi” yaani kazi za shetani, yeye anamaanisha zile dhambi ambazo shetani anawaongoza watu wa dunia ndani. Hii ndiyo sababu Yohana anasema, “Yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo” (1 Yohana 3:8). Kwa hivyo ni kazi za shetani ambazo Kristo alikuja kuziangamiza.

Yaani katika kifungu hiki Yohana anasema mara mbili ni kwa nini Kisto alikuja hapa ulimwenguni. Anasema kwamba Kristo alikuja hapa ulimwenguni kuondoa dhambi, yaani kuangamiza kazi za shetani ambazo ni dhambi. Yesu Kristo alizaliwa na bikira Maria kupitia kwa nguvu za Roho Mtkatifu (Mathayo 1:18, 20), na

"akakua katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu" (Luka 2:52), na alikuwa kamili na alimtii Mungu katika maisha yake yote na huduma zake zote hata hadi kifo (Wafilipi 2:5-8; Waebrania 4:15). Biblia inasema kwamba Kristo alifanya haya yote ili aweze kuangamiza dhambi na kuondoa dhambi.

**Kristo alikuja ulimwenguni kutuonyesha upendo wa Mungu.**

Pia, katika kifungu hiki cha 1 Yohana 3:1-10, tunaona kwamba Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni kudhihirisha upendo wa Mungu ambao unawapatia uhai wale ambao ni maadui wa Mungu na wamekufa katika dhambi na makosa yao. Biblia inasema, "Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani mmeokolewa kwa neema" (Waefeso 2:4-5).

Kwa hivyo tunaona kwamba ukuu wa upendo wa Mungu unaonekana wakati tunaona kwamba Mungu huwawezesha wale ambao ni wenye dhambi wakuu na maadui wake kuzaliwa mara ya pili. Sisi sote tulikwa tumekufa katika dhambi na makosa, na sisi sote tulimtii shetani katika maisha yetu (Waefeso 2:2). Kwa sababu Mungu ni Mungu wa haki, alistahili kutuhukumu Lakini Mungu hakutuhukumu, bali alituokoa kwa kutuwezesha kuzaliwa mara ya pili. Kwa hivyo katika kuzaliwa mara ya pili kwetu tunaona ukuu wa upendo wa Mungu juu ya maadui wake. Wale ambao wamezaliwa mara ya pili wamezaliwa mara ya pili kwa sababu ya neema na upendo wa Mungu.

Hii ndiyo sababu Yohana anaandika, "Oneni ni pendo kuu namna gani aliotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu! Nasi ndivyo tulivyo. Sababu kwa nini ulimwengu haututambui, ni kwa kuwa haukumtambua Yeye. Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu likini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya

kwamba Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo" (1 Yohana 3:1-2).

Katika kifungu hiki tunaona mambo manne makuu kuhusu upendo wa Mungu. Haya mambo manne pia yanaonekana katika Waefeso 2:4.

***1. Kupitia kwa upendo wa Mungu, tunakuwa watoto wa Mungu.***

Yohana anasema, "Oneni ni pendo kuu namna gani aliotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu!" Hii inamaanisha kwamba wale ambao hawajazaliwa mara ya pili si watoto wa Mungu. Wao ni watu wa dunia na wamekufa kiroho. Lakini wale ambao wamezaliwa mara ya pili ni watoto wa Mungu. Hii ndiyo sababu Yohana anasema, "Oneni ni pendo kuu namna gani aliotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu! Nasi ndivyo tulivyo." Yohana hapa anasema kwamba sisi tulikuwa tumekufa na maadui wa Mungu lakini Mungu alituita kutoka kwa wafu, kama tu vile Yeye alimwita Lazaro atoke kwa wafu. Yesu Kristo alisimama kaburini na kumwita Lazaro, na kwa kumwita, alimpatia Lazaro uhai (Yohana 11:43). Vilevile, Mungu alituita kutoka kwa wafu, na kwa kutuita alitupatia uhai. Hii ndiyo maana ya kuzaliwa mara ya pili: Mungu alitufanya tuwe hai, kama tu vile aliwafanya watu wa Efeso wawe hai (Waefeso 2:5).

***2. Tunazaliwa mara ya pili kupitia kwa upendo kuu wake Mungu.***

Sisi tunazaliwa mara ya pili na kuingia katika jamii ya Mungu kwa sababu ya upendo kuu wa Mungu, kama vile tunafundishwa katika Waefeso 2:4-5. Yohana anasema, "Oneni" (1 Yohana 3:1), yaani, "Tazameni, hili ni jambo la kutushangaza." Na halafu anaendelea kusema, "Oneni ni pendo kuu namna gani aliotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu! Nasi ndivyo tulivyo." Yohana hapa anatufundisha, kama tu vile Paulo anafundisha katika Waefeso

2:4-5 kwamba hili ni jambo la kutushangaza kwamba sisi ambao tulikuwa tumekufa katika dhambi na makosa na ambao tulikuwa maadui wa Mungu, tumezaliwa mara ya pili. Anasema kwamba hili ni jambo la kutushangaza kwamba sisi tumezaliwa mara ya pili kwa sababu sisi tulikuwa waasi na maadui wa Mungu na wafu katika dhambi na watumwa ambao hawakuwa na uwezo wa kusikia na kulitii neno la Mungu. Yohana anasema kwamba ni jambo la kutushangaza kwamba sisi sasa tumezaliwa mara ya pili na kuitwa watoto wa Mungu. Hii ndiyo sababu anasema, “Oneni!”

***3. Upendo wa Mungu unatuhakikishia kwamba siku moja tutakamilika.***

Yohana hapa anatufundisha kwamba huu ni upendo wa Mungu kwamba sisi ambao tulikuwa tumekufa na kuwa maadui wa Mungu na waasi dhidi ya sheria yake, sasa tumezaliwa mara ya pili na kuokoka. Na anaendelea kusema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili bila shaka watakamilika kabisa, yaani watakuwa bila dhambi yoyote, na wataishi pamoja na Mungu milele.

Tazama vizuri ni nini Yohana anafundisha katika mstari wa 2 ambao unasema, “Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua kwamba, Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa manaa tutamwona kama alivyo” (1 Yohana 3:2). Yohana hapa anaongea kuhusu mambo matatu: upendo wa Mungu, maisha yetu ya sasa kama watoto wa Mungu, na maisha ya mbele ambayo tunatarajia. Yohana hapa anasema kwamba ikiwa mtu amezaliwa mara ya pili sasa, yeye bila shaka atakuwa pamoja na Yesu milele. Anasema, “Twajua,” yaani jambo hili ni la hakika na bila shaka. Kwa ufupi, katika mstari huu Yohana anasema, “Sisi sasa ni watoto wa Mungu, na ile ambayo tutakuwa bado haijadhihirishwa, lakini ile siku Yesu Kristo atarudi, tunajua kwa hakika kwamba sisi tutakuwa kama Yeye mwenyewe.” Wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanajua

bila shaka kwamba wao watakuwa pamoja na Kristo milele kwa sababu kwa kupitia upendo wake, wao sasa ni watoto wa Mungu. Wao tayari ni watoto wa Mungu lakini hawajakamilika. Ile siku Yesu Kristo atarudi, wao bila shaka watakamilika.

***4. Upendo wa Mungu unatukumbusha kwamba ni lazima tuzaliwe mara ya pili.***

Kwa hivyo katika kifungu hiki cha 1 Yohana 3:1-10, tunaona wazi ni nini mtu atakosa ikiwa yeye hajazaliwa mara ya pili. Yohana hapa anasema kwamba ikiwa mtu hajazaliwa mara ya pili yeye hatakamilika na kuishi pamoja na Mungu milele. Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili” (Yohana 3:7). Yule ambaye amezaliwa mara ya pili kweli ataona ufalme wa Mungu, yaani atamwona Kristo uso kwa uso na atakamilika na ataishi pamoja naye milele kwa furaha.

Kwa hivyo hapa tunaona jibu la swali hili, “Je ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili?” Jibu ambalo tunapata katika kifungu hiki ni kwamba ikiwa wewe hujazaliwa mara ya pili, wewe hutamwona Kristo na hutabadilishwa katika mfano wake, bali utaishi chini ya ghadhabu yake milele, kama vile Yesu mwenyewe alifundisha katika Yohana 3:36. Lakini ikiwa wewe umezaliwa mara ya pili kupitia kwa upendo wa Mungu ambao hauwezi kupimwa, basi unajua kwa hakika kwamba wakati Yeye atakuja wewe utakuwa kama Yeye. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili ndiye pekee ataingia mbinguni. Hii ndiyo sababu unahitaji kuzaliwa mara ya pili.

# Uhusiano kati ya kuja kwake Kristo na kuzaliwa kwetu mara ya pili

Je, ni kwa nini Kristo alikuja hapa ulimwenguni? Tayari tumeona kwamba yule ambaye anataka kuingia mbinguni anahitaji kuzaliwa mara ya pili, lakini, je, ni kwa nini Kristo alikuja hapa ulimwenguni? Je, ni kweli kwamba Yeye alihitaji kuja hapa ulimwenguni ili watu wake waweze kuzaliwa mara ya pili? Je, watu wangeweza kuzaliwa mara ya pili bila kuja kwake Kristo?

Jibu la swali hili ni kwamba kuzaliwa mara ya pili na matokeo yake yote kama imani na kuhesabiwa haki na kutakaswa na kuwa kama Kristo mwenywe, haya yote hayawezekani bila kuzaliwa kwake Kristo na maisha Yake hapa ulimwenguni na kifo chake. Hili ni jambo ambalo tunapata katika kifungu hiki cha 1 Yohana 3:1-10.

1. ***Tunazaliwa mara ya pili ili tuweza kumtazama na kumwamini Kristo ambaye alikuwa Mungu na Mwanadamu.***

Lengo la kuzaliwa mara ya pili ni ili tuweze kuwa na imani ndani ya Kristo ambaye alikuja hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu. Yesu hangekuja hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu, kuzalizwa mara ya pili hakungekuwa na lengo lolote. Biblia inasema, "Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu," Wakati Yohana hapa anasema, "kwamba Yesu ndiye Kristo" anamaanisha, "Kila mtu anayeamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwokozi ambaye aliahidiwa na Mungu na ambaye alikuwa hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu." Hii inamaanisha kwamba wakati Roho Mtakatifu anamwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili, anafanya kazi hii ili yule mtu awe na imani ndani ya Yesu Kristo ambaye alikuwa mwanadamu (1 Yohana 4:2-3). Hili ndilo lengo la kuzaliwa mara ya pili, na huu ndiyo ushahidi kwamba mtu

amezaliwa mara ya pili, kwamba yeye anaamini Yesu Kristo ambaye alikuwa mwanadamu kamili. Hii ndiyo sababu Yohana anasema, "Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu." Imani ndani ya Kristo ni ushahidi kwamba mtu amezaliwa mara ya pili.

2. ***Maisha mapya ambayo tunapewa wakati tunazaliwa mara ya pili yanakuja kwa sababu tumeunganishwa na Yesu Kristo ambaye alikuwa mwanadamu.***

Sababu ya pili ni kwa nini Kristo alihitaji kuja hapa ulimwenguni ili wenye dhambi waweze kuzaliwa mara ya pili ni kwa sababu yule ambaye amezaliwa mara ya pili anapewa maisha ya kiroho, na maisha haya ya kiroho yanakuja kwake kupitia kwa Yesu Kristo ambaye alikuwa mwanadamu kamili. Yesu Kristo alisema, "Mimi ni mkate wa uzima ule uliotoka mbinguni. Mtu ye yote akiula mkate huu ataishi milele. Mkate huu ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu" (Yohana 6:51). Maisha ambayo tunapewa wakati tunazaliwa mara ya pili ni yale maisha ambayo Yesu Kristo mwenyewe alituchukulia sisi wakati Yeye aliishi hapa ulimwenguni na wakati alikufa juu ya msalaba.

Biblia inasema, "Kila mtu amwaminiye Mwana wa Mungu anao ushuhuda ndani mwake...Huu ndiyo ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima" (1 Yohana 5:10-12).

Yohana hapa anasema kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anao uzima na uzima huu umekuja kwake kwa sababu yeye ameunganishwa kwa Yesu Kristo. Yesu ndiye uzima wetu. Uzima wake upya ndani yetu, na mabadiliko yote ambayo yanatendeka ndani mwetu, ndiyo ushuhuda kutoka kwa Mungu kwamba sisi ni watoto wake. Na uzima huu ni uzima wa Yesu Kristo ambaye alikuwa mwanadamu kamili. Hii ndiyo sababu Bibia inasema,

"Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi tukauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli...Kutokana na ukamilifu Wake, sisi sote tumepokea neema juu ya neema" (Yohana 1:14-16). Huku ndiko kuzaliwa mara ya pili, na huu ndiyo uzima.

**Bila kuja kwake Kristo hapa ulimwengu hakungekuwa na kuzaliwa mara ya pili.**

Kwa hivyo hapa tumeona kwamba bila kuja kwake Kristo hapa ulimwenguni, mtu hawezi kuzaliwa mara ya pili. Hii ni kwa sababu mbili:

(i) Yule ambaye amezaliwa mara ya pili amefanywa hivyo ili amtazame na kuwa na imani ndani ya Kristo ambaye alikuja hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu.

(ii) Yule ambaye amezaliwa mara ya pili anapata uzima wake kutoka kwa Yesu Kristo ambaye alikuja hapa ulimwenguni na kuishi akiwa mwanadamu kamili. Bila kuja kwake, yule ambaye amezaliwa mara ya pili hangekuwa na uzima.

Hii inamaanisha kwamba dini ya ukristo iko na msingi mkuu, na msingi huu ni maisha yake Yesu Kristo wakati Yeye alikuwa hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu kamili. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima" (1 Yohana 5:12). Na pia, hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Ye yote asiyemheshimu Mwana, hamheshimu Baba aliyemtuma" (Yohana 5:23), na hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema, "Yeye anikataaye Mimi amkataa Yeye aliyenituma" (Luka 10:16). Kristo hangekuja hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu kamili, hatungeweza kuunganishwa naye na pia hatungekuwa na ushirika na Mungu Baba, na kwa hivyo hatungeweza kuzaliwa mara ya pili, na hatungeweza kuokoka.

**Uhusiano kati ya kuja kwake Kriso hapa ulimwenguni na kutakaswa kwetu.**

Kwa jumla, tunasema kwamba bila kuja kwake Kristo hapa ulimwenguni hakungekuwa na jambo kama kuzaliwa mara ya pili na kuokoka kupitia kwa imani. Na kwa hivyo hakungekuwa na kuhesabiwa haki na kutakaswa, na kuwa na utukufu milele. Hili ni jambo ambalo Biblia inafundisha wazi katika kifungu hiki: "Kila mmoja mwenye matumaini haya katika Yeye hujitakasa, kama vile Yeye alivyo mtakatifu. Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala ndani Yake hamna dhambi" (1 Yohana 3:3).

Katika kifungu hiki tunasoma kuhusu kuhesabiwa haki na pia tunasoma kuhusu kutakaswa. Yohana anaongea wazi kuhusu kutakaswa. Anasema, ikiwa wewe umezaliwa mara ya pili, utapenda sana siku ya kurudi kwake Kristo, na utangoja sana ile siku ambayo utabadilishwa na kuwa kama Yeye. Tazama kwamba katika mstari wa 2 Yohana anasema, "Yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye," na katika mstari wa 3 anasema, "Kila mmoja mwenye matumaini haya katika Yeye hujitakasa, kama vile Yeye alivyo mtakatifu." Hii inamaanisha kwamba wale wote ambao wanapenda sana siku yao ya kukamilishwa wanapenda utakatifu sasa na wanachukia uchafu sasa na wanapigana vita na dhambi sasa.

Hii inamaanisha kwamba kuzaliwa mara ya pili kunaamsha imani ndani yetu na kunatujaza na upendo wa ile siku ya kutakaswa; na pia kunaanza ndani yetu vita dhidi ya dhambi. Kwa hivyo bila kuja kwake Yesu Kristo hapa ulimwenguni hakungekuwa kuzaliwa mara ya pili, na hakungekuwa kutakaswa sasa na hakungekuwa utakatifu kamili na hakungekuwa na tumaini la kuwa kama Kristo mwenyewe.

Dini ya ukristo si dini ya kujaribu kuishi maisha mema, bali ni dini ambayo inawabadilisha watu kutoka ndani kwa sababu ya maisha yake Yesu Kristo hapa ulimwenguni. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili anayo imani ndani yake, na Kristo mwenyewe anatuhakikishia utakatifu wetu wa milele. Hii ndiyo sababu sisi tunaanza kujitakasa.

Wakati tunasoma na kujifunza Yohana 3:4-5, tunaona kwamba Yohana hapa anatufundisha pia kuhusu kuhesabiwa haki. Baada ya kusema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanajitakasa kama vile Kristo ni mtakatifu, Yohana anaendelea kusema, “Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi” (1 Yohana 3:4).

Je, ni kwa nini Yohana hapa anasema kwamba dhambi ni uasi na halafu anasema, “Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi”? Yohana anasema hivi kwa sababu anataka kutufundisha kwamba kazi yake Yesu Kristo ya kutuokoa kutoka kwa dhambi si kazi ya kututakasa pekee.

Wakati tunawaza juu ya dhambi, tunahitaji kukumbuka kwamba dhambi inatufanya tuwe wachafu, lakini pia dhambi ni kuvunja sheria ya Mungu. Yule ambaye anatenda dhambi anakuwa mchafu mbele ya Mungu na kwa hivyo anahitaji kutakaswa, lakini pia wakati anatenda dhambi anakuwa mwenye hatia mbele ya Mungu na kwa hivyo anahitaji msamaha wa dhambi zake. Pia yeye ako chini ya ghadhabu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zake, na hii ghadhabu inahitaji kuondolewa. Pia wakati mtu anatenda dhambi yeye anapungukiwa na utukufu wa Mungu.

Hii ndiyo sababu Yohana anasema, “Dhambi ni uasi. Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi.” Wakati Yohana hapa anasema kwamba Kristo alikuja hapa ulimwenguni ili aziondoe dhambi hamaanishi tu kwamba alikuja kututakasa kutoka kwa uchafu wa dhambi, bali anamaanisha kwamba Kristo alikuja

hapa uliwmenguni kuondoa hatia ya dhambi na pia kuondoa ghadhabu ya Mungu. Je, ni namna gani Kristo alifanya haya yote? Alifanya haya kupitia kwa kuzaliwa kwake na maisha yake na kifo chake. Biblia inasema hivi: "Huu ndiyo upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Yohana 4:10). Biblia hapa inasema kwamba Mungu alimtuma Mwana wake kuja hapa ulimwenguni ili Yeye afe kwa ajili yetu na aondoe ghadhabu ya Mungu ambayo sisi tulistahili. Hiki ndicho kipatanisho – kuondoa ghadhabu ya Mungu. Kwa sababu Kristo alikufa, ghadhabu ya Mungu iliondolewa milele kutoka kwa wale ambao wamezaliwa mara ya pili.

Pia katika Biblia tunasoma, "Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki" (1 Yohana 2:1). Tazama hapa kwamba Yohana anamwaita Kristo "Mwenye haki." Hii ni kwa sababu wakati Yeye anatuokoa, anatumia damu Yake na pia haki Yake. Hii ndiyo sababu Yohana anasema, "Ndani Yake hamna dhambi" (1 Yohana 3:5). Sisi wanadamu ni wenye dhambi na tunahitaji kuwa kamili mbele ya Mungu. Tunakamilishwa kwa imani ndani yake. Yeye alichukua dhambi zetu na Yeye anatupatia haki yake.

Kwa hivyo, kwa jumla tunaweza kusema kwamba sisi wenye dhambi tunaweza kupata wokovu kwa sababu moja tu, na hii ni kwa sababu Yesu Kristo ambaye ni Mwana wa Mungu alikuja hapa ulimwenguni kuwa mwanadamu kamili. Alihitaji kuja kuwaokoa wenye dhambi. Mwana wa Mungu alikuwa Mwanadamu ambaye ni Mungu; "Neno alifanyika mwili" (Yohana 1:14). Bila kuja kwake hakungekuwa na imani, kuhesabiwa haki, kutakaswa na tumaini la utukufu wa milele.

Mungu, ambaye anayo rehema nyingi, kutoka kwa upendo wake ambao alitupendanao, alimtuma Mwana Wake hapa ulimwenguni

kuishi na kufa kwa ajili yetu, ingawa sisi tulikwa wafu katika dhambi. Huu ni upendo ambao Mungu ametuonyesha! Hapa tunaona kutii kwake Kristo na dhabihu yake kwa ajili yetu. Hapa tunafahamu kwamba Roho Mtakatifu mwenyewe ametuamsha na anafanya kazi yake kwa kutuleta katika imani na maisha ya milele.

# Sehemu ya Tatu

# Je, ni namna gani mtu anazaliwa mara ya pili?

*“Kwa hiyo, vifungeni viuno vya nia zenu, mwe na kiasi, mkitumainia kikamilifu ile neema mtakayopewa, Yesu Kristo atakapodhihirishwa. Kama watoto watiifu, msifuate tamaa zenu mbaya za kwanza za wakati wa ujinga. Bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote, kwa maana imeandikwa: ‘Mtakuwa watakatifu, kwa kuwa Mimi ni mtakatifu.’*

*Nanyi kama mnamwita ‘Baba,’ Yeye ahukumuye kila mtu kulingana na matendo yake pasipo upendeleo, enendeni kwa hofu ya kumcha Mungu wakati wenu wa kukaa hapa duniani kama wageni. Kwa maana mnafahamu kwamba mlikombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliurithi kutoka kwa baba zenu, si kwa vitu viharibikavyo, yaani, kwa fedha na dhahabu, bali kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ile ya Mwana-Kondoo asiye na dosari wala doa. Yeye aliwekewa hayo kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu, lakini akadhihirishwa katika siku hizi za mwisho kwa ajili yenu, ambaye kwa Yeye mmemwamini Mungu aliyemfufua kutoka kwa wafu akampa utukufu, ili imani yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu.*

*Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni. Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele. Maana, Mwili wote ni kama majani na utukufu wote wa binadamu ni kama ua la majani, majani hunyauka na ua lake hupukutika, lakini neno la Mungu ladumu milele.*

*Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu”.*

1 Petro 1:13-25

# Ni nini Mungu anafanya ili tuweze kuzaliwa mara ya pili

**Kazi ya Mungu na Jukumu la Wanadamu.**

Yesu Kristo alisema kwamba kila mtu anahitaji kuzaliwa mara ya pili (Yohana 3:3). Lakini ukweli ni kwamba hakuna yeyote ambaye anaweza kuamua ni lini atazaliwa mara ya pili na ni namna gani. Sisi sote tunajua kwamba mtoto hawezi kuamua ni lini atazaliwa, na yule ambaye amekufa hawezi kuamua kufufuka. Sisi sote tumekufa katika dhambi na makosa. Hii ndiyo sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili na hii ndiyo sababu hatuwezi kujizaa mara ya pili: sisi ni wafu, na wafu hawawezi kujipatia uhai! Hii ndiyo sababu tunaongea kuhusu utawala wa Mungu wa neema, na hii ndiyo sababu tunapenda utawala wa Mungu wa neema.

Hali yetu kabla ya kuzaliwa mara ya pili ni kwamba tunathamini dhambi na kiburi na kwa hivyo hatumthamini Kristo. Yaani sisi ni waasi dhidi ya Mungu mioyoni mwetu, na kwa hivyo hatuwezi kumtazama Yesu Kristo kwa unyenyekevu. Na sisi tuna hatia kwa sababu ya dhambi hii. Kuna uovu kuu ndani mwetu na tuna hatia ya dhambi zetu kwa sababu sisi ni watu wagumu na tumekufa. Sisi tunampuuza Kristo na hata dhamira zetu zinajua jambo hili.

Hii ndiyo sababu ni lazima tuzaliwe mara ya pili. Kristo alisema kwamba ni lazima tuzaliwe mara ya pili (Yohana 3:3). Roho Mtakatifu anahitaji kufanya muujiza ndani ya mioyo yetu na kutupatia maisha ya kiroho. Tulikuwa tumekufa na tulihitaji kufanywa hai. Tunahitaji masikio ambayo yanasikia ukweli wa Mungu na kuutamani; tunahitaji macho ambayo yanamwona Kristo na njia yake ya wokovu kuwa mzuri sana. Tunahitaji mioyo ambayo inaweza kulipokea neno la Mungu. Kwa ufupi, tunahitaji uhai, tunahitaji kuzaliwa mara ya pili.

Tumeona, ni namna gani Mungu anatupatia uhai: Roho Mtakatifu anatuunganisha kwa Yesu Kristo kupitia kwa imani. Kwa hivyo yale maisha mapya tunapata wakati tunazaliwa mara ya pili, yanakuja kutoka kwa Kristo na yanakuja kupitia kwa imani: haya mambo matatu: maisha mapya na kuunganishwa kwa Kristo na imani hayawezi kutenganishwa. Wakati Mungu, kutoka kwa rehema yake mingi na upendo wake kuu na utawala wa neema yake, anaamua kutufanya tuzaliwe mara ya pili, anatupatia maisha ya kiroho kwa kutuunganisha kwa Yesu Kristo. Biblia inasema, "Huu ndiyo ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe" (1 Yohana 5:11). Sisi wenyewe tunapata uzima huu wakati tunaweka imani yetu ndani ya Yesu Kristo. Hii haimaanishi kwamba kwanza tunapata uzima wa kiroho, halafu baada ya muda tunamwamini Kristo, bali wakati tunapata uzima, dakika ile ile tunamwamini Kristo, na wakati tunamwamini Kristo, basi tunajua kwamba tumezaliwa mara ya pili. Wakati kuna moto, kuna joto, na wakati kuna kuzaliwa mara ya pili, kuna imani.

Katika kitabu hiki, tayari tumetazama maswali mawili: je, inamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili, na je, ni kwa sababu gani tunahitaji kuzaliwa mara ya pili. Sasa, katika sehemu hii ya kitabu hiki, ninataka kuuliza swali hili: Je, ni namna gani mtu anazaliwa mara ya pili? Katika sehemu hii, tutaona ni kazi gani Mungu anafaya wakati anamzaa mtu mara ya pili, na pia tutaona jukumu la mwanadamu: je, ni nini Mungu anafanya wakati anamfanya mtu azaliwe mara ya pili, na je, ni nini mtu anafaa kufanya ili azaliwe mara ya pili?

Pengine unawaza kwamba hakuna chochote tunafaa kufanya ili tuzaliwe mara ya pili kwa sababu tumekufa katika dhambi, lakini hii si kweli. Hata yule ambaye amekufa kimwili anafanya jambo fulani wakati anafufuliwa: yeye anafufuka! Kwa mfano, wakati Lazaro alikufa, yeye alilala tu ndani ya kaburi, yeye hakufanya chochote kupata uhai kwa sababu yeye alikuwa amekufa. Ni Kristo ambaye alimpatia uhai.

Katika Yohana 11:43 tunasoma kwamba Kristo alimwambia, "Lazaro, njoo huku!" Na mstari ambao unafuata unasema, "Yule aliyekuwa amekufa alitoka nje." Kwa hivyo Lazaro alikuwa na jukumu la kufanya katika kufufuka kwake: ni yeye ambaye alitoka kaburini. Ni Kristo ambaye alimwezesha kutoka kaburini, na ni Lazaro mwenyewe ambaye alitoka kaburini. Tunaweza kusema kwamba Kristo alimpatia Lazaro uhai, na Lazaro alitoka kaburini. Ile dakika Kristo alimwamuru Lazaro aamke, Lazaro aliamka, na ile dakika Mungu anatupatia uzima, tunaanza kuishi maisha ya kiroho, na ile dakika Mungu anatupatia imani, tunamwamini Kristo.

Hii ndiyo sababu katika sehemu hii ninauliza maswali mawili. Tunataka kuona ni namna gani tunazaliwa mara ya pili, na ili tujue jambo hili, tunahitaji kuuliza maswali mawili: je, ni nini Mungu anafanya kutuwezesha kuzaliwa mara ya pili, na ni nini sisi tunafaa kufanya ili tuzaliwe mara ya pili.

### Je, ni namna gani Mungu anatufanya tuzaliwe mara ya pili?

Tunapata majibu matatu ya swali hili katika sura ya kwanza ya waraka ya 1 Petro.

(i) Kwanza, tunasoma kwamba Mungu "Ametuzaa sisi mara ya pili katika tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwa Yesu Kristo kutoka kwa kifo" (1 Petro 1:3).

(ii) Pili, Biblia inasema, "Mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele" (1 Petro 3:23).

(iii) Tatu, Biblia inasema, "Kwa maana mnafahamu kwamba mliokombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa ambao aliurithi kutoka kwa baba zenu" (1 Petro 1:18).

**Kazi ya Mungu ya kuwazaa wenye dhambi mara ya pili ni kazi ambayo inadumu.**

Wakati tunachunguza hii mistari, tunaona kwamba mambo haya matatu ambayo Mungu anafanya yanadumu milele. Hili ni jambo ambalo Petro anasema mara tatu katika kifungu hiki cha 1 Petro 1:13-25.

(i) Kwanza Petro anasema, "Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Kwa rehema zake kuu ametuzaa sisi mara ya pili katika tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwa Yesu Kristo kutoka kwa wafu ili tuupate urithi usioharibika" (1 Petro 1:3-4).

Hii inatufundisha kwamba wakati Mungu anatuzaa mara ya pili, lengo lake ni kwamba tuwe na uzima wa milele. Hii ndiyo sababu Petro hapa anasema kwamba "Kwa rehema zake kuu ametuzaa sisi mara ya pili katika tumaini lenye uzima." Yaani, Biblia hapa inasema kwamba tumepewa tumaini la maisha ya milele, na kwamba tumaini hili linaishi, halitakufa. Pia urithi wetu ni ule ambao hautaharibika: uzima wetu wakati tunazaliwa mara ya pili ni uzima wa milele, sisi ambao tumezaliwa mara ya pili hatutakufa kiroho.

(ii) Pili, Petro anasema, "Kwa maana mnafahamu kwamba mlikombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliurithi kutoka kwa baba zenu, si kwa vitu viharibikavyo, yaani kwa fedha na dhahabu, bali kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ile Mwana-Kondoo asiye na dosari wala doa" (1 Petro 1:18-19).

Damu ya Kristo (mstari 19) ndiyo malipo ya ukombozi wetu, na damu hii si kama vitu ambavyo havina thamani kama fedha na dhahabu. Vitu kama fedha na dhahabu havina thamani kwa sababu vitu hivi huharibika. Lakini Biblia hapa inasema kwamba sisi tumekombolewa, "si kwa vitu viharibikavyo, yaani kwa fedha na dhahabu."

Kwa hivyo tena tunaona hapa kwamba yule ambaye amekombolewa na damu ya Kristo Yesu hawezi kurudi kwa utumwa wa dhambi kwa sababu yale malipo ambayo Kristo amelipa kwa kutuzaa hayawezi kuharibika.

Damu ya Yesu Kristo ni ya thamani ya milele na kwa hivyo dhamana yake haiwezi kuisha. Hii ndiyo njia tumekombolewa, na haya ndiyo malipo ya maisha ambayo tunapata wakati tunazaliwa mara ya pili. Na ni Kristo ambaye analipa malipo haya.

(iii) Tatu, Petro anasema, "Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele" (1 Petro 1:23). Baada ya kusema hii, Petro ananukuu Isaya ambaye aliandika, "Mwili wote ni kama majani na utukufu wote wa binadamu ni kama ua la majani, majani hunyauka na ua lake hupukutika, lakini neno la Mungu ladumu miele." Yaani Petro hapa anafundisha yale ambayo alifundisha katika mstari wa 3 kuhusu kufufuka na yale ambayo alifundisha katika mstari 18 kuhusu kukomblewa kwetu. Mbegu ya neno la Mungu haiharibiki na kwa hivyo yale maisha ambayo mbegu hii inazaa pia hayaishi.

Kwa hivyo, hapa tumeona kwa jumla mafundisho ya Petro kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Petro anafundisha kwamba tunazaliwa mara ya pili katika tumaini la uzima, yaani yale maisha ambayo Mungu anaweka ndani yetu wakati anatuzaa mara ya pili ni maisha ambayo hayataisha; ni maisha ya milele. Utu upya ambao unakuja wakati mtu anazaliwa mara ya pili hauwezi kufa, bali unaishi milele. Haya ndiyo mafundisho ya Petro katika kifungu hiki. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili hatakufa kamwe. Petro anayaandika mambo haya kwa sababu aliandika waraka wake kwa wale ambao waliteswa kwa ajili ya imani yao. Petro alitaka kuwaambia wale wakristo ambao wanateswa, "Msiogope wale ambao wanawatesa; wao wanaweza kuua mwili lakini hawawezi kuyaua yale maisha mapya ambayo Mungu ameyaweka ndani yenu. Haya ni ya milele."

**Kukombolewa kwetu, kufufuka kwake Kristo na kuitwa kwetu.**

Kwa hivyo sasa tunataka kuangalia hizi kazi tatu za Mungu kwa uangalifu na kuona ni namna gani Mungu anamzaa mtu mara ya pili. Tutachukua kila moja ya kazi hizi ya Mungu na kuitazama jinsi Mungu anaifanya hii kazi. Hizi ni kazi tatu ambazo Mungu anafanya kuwazaa wenye dhambi mara ya pili:

(i) Mungu alitukomboa kupitia kwa damu ya Yesu Kristo.
(ii) Mungu alimfufua Yesu Kristo kutoka kwa wafu.
(iii) Mungu alituita katika uzima kupitia kwa neno lake ambalo ni hai na ni la milele.

(i) Kwanza, Petro anasema kwamba mtu akitaka kuzaliwa mara ya pili, anahitaji kwanza kukumbolewa kwa damu ya Yesu Kristo. Petro anaandika, “Kwa maana mnafahamu kwamba mlikombolewa kutoka katika mwenendo wenu usiofaa ambao mliurithi kutoka kwa baba zenu, si kwa vitu viharibikavyo, yaani, kwa fedha na dhahabu, bali kwa damu ya thamani ya Kristo kama ile ya Mwana-Kondoo asiye na dosari wala doa” (1 Petro 1:18-19).

Jambo ambalo Petro anafundisha hapa ni kwamba, kuzaliwa mara ya pili ni yale maisha ya milele ambayo wale ambao ni watumwa wa dhambi hawawezi kupata hadi wao wakombolewe. Katika kifungu hiki Petro anasema kwamba sisi sote wakati moja tulikuwa watumwa wa dhambi na tulikuwa na ile tabia ya maisha na ya mawazo ambayo inaweza kutuangamiza. Sisi sote tulikuwa chini ya ghadhabu ya Mungu, na Mungu alikuwa ametuacha tufuate njia ya uovu (Warumi 1:21, 24,26,28). Utumwa wa dhambi unamwangamiza mtu hadi yeye akombolewe kutoka utumwa huu. Mungu alilipa fidia ya ukombozi huu kwa kumtuma Kristo achukue ghadhabu yake juu yake (Warumi 8:3; Wagalatia 3:13).

Huu ni msingi ambao unawezesha sisi kuzaliwa mara ya pili. Kuja kwake Kristo na maisha yake na kifo chake ndiyo njia ya Mungu Baba kutuleta kwa Kristo na kutuunganisha kwa Kristo na kutuingiza katika ushirika wa karibu sana naye. Pia, kuja kwake Kristo na maisha yake na kifo chake ndiyo njia kwa Mungu kutupatia imani na maisha mapya. Kristo mwenyewe alisema, "Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kujitoa uhai Wake kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi" (Marko 10:45). Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni na kuishi hapa.

"Mwana wa Adamu alikuja kujitoa uhai Wake kuwa ukombozi kwa ajili ya wengi." Yeye alihitaji kufanya hii ili Mungu kwa neema Yake aweze kuwapa wenye dhambi kama sisi maisha bila malipo. Na kwa sababu kuzaliwa mara ya pili ni zawadi ya maisha ya milele na si maisha ya miaka michache tu, malipo ya ukombozi ilipaswa kuwa ile ambayo haiwezi kuharibika. Malipo ya kutukomboa haiwezi kuwa vitu kama fedha na dhahabu ambavyo vinaweza kuharibika. Damu yake Yesu iko na thamani ya milele na haiwezi kupoteza uwezo wake wa kuwakomboa wenye dhambi. Maisha ambayo damu yake yanatupatia ni ya milele. Kwa hivyo njia ambayo Mungu anaweza kuzaa mara ya pili wenye dhambi ni kulipa malipo ya kuwakomboa kwa milele.

(ii) Jambo la pili ambalo lilihitajika ili sisi tuweze kuzaliwa mara ya pili ni kufufuka kwake Kristo. Petro anaandika, "Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo kwa rehema zake kuu ametuzaa sisi mara ya pili katika tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwa Yesu Kristo kutoka kwa wafu ili tuupate urithi usioharibika, usio na uchafu, ule usionyauka, uliyotunzwa mbinguni kwa ajili yenu" (1 Petro 1:4-5). Petro anasema kwamba sisi tumezaliwa mara ya pili kupitia kwa kufufuka kwake Yesu Kristo. Kwa hivyo njia ya pili ambayo Mungu anatumia kutuzaa mara ya pili ni ufufuo wake Yesu Kristo kutoka kwa wafu.

Sisi tunazaliwa mara ya pili wakati Roho Mtakatifu anaondoa mioyo yetu ya dhambi na kutuunganisha kwa Yesu Kristo kupitia kwa imani ili maisha yake yanakuwa maisha yetu. Kwa hivyo ni lazima Kristo afufuke kutoka kwa wafu kwa sababu watu wake wanahitaji kuwa na ushirika wa karibu naye ili wao wapate maisha ya milele. Tunazaliwa mara ya pili wakati tunaunganishwa kwa karibu na Yesu Kristo ambaye alikuja hapa ulimwenguni na kuishi hapa. Maisha mapya ambayo tunapata wakati tunazaliwa mara ya pili ni maisha ya Yesu Kristo ambaye alikuwa hapa ulimmwenguni. Kwa hivyo ikiwa yeye hangefufuka kutoka kwa wafu, basi sisi hatungeweza kupata maisha mapya. Kwa hivyo njia ya pili jinsi Mungu anatuzaa mara ya pili ni kumfufua Yesu Kristo.

(iii) Njia ya tatu ambayo Mungu anatumia kuzaa wenye dhambi mara ya pili ni kutuita. Petro aliandika, “Kama watoto watiifu, msifuate tamaa zenu mbaya za kwanza za wakati wa ujinga. Bali kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote” (1 Petro 1:14-15). Katika kifungu hiki Petro anatuambia kwamba tunahitaji kuishi maisha tofauti kwa sababu kuna kitu fulani ambacho kimefanyika ndani mwetu. Anasema, “Kama Yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote” (mstari 15). Wakati Mungu anatuita, Yeye anatuzaa mara ya pili. Kwa hivyo tunaona hapa kwamba Mungu anatuzaa mara ya pili kwa njia hii: anatukomboa kwa damu ya Yesu Kristo, alimfufua Yesu Kristo na anatuita ili tuje kwake na tuunganishwe kwa Yesu Kristo.

Tunahitaji kufahamu mwito huu ambao Mungu ametuita. Kuna mwito ambao unahubiriwa kila siku kwa watu wote. Katika kifungu hiki Petro anaandika, “Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele” (mstari 23). Tazama kwamba tunazaliwa mara ya pili kupitia kwa neno la Mungu.

Petro hapa anasema, “Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu” (mstari 25).

Injili inahubiriwa kwa watu wote lakini si wote ambao wanaipokea na kuokoka. Hii ndiyo sababu tunasema kwamba Mungu anawaalika wote kwa jumla kupitia kwa injili. Kuna mwito wa Mungu kupitia kwa mahubiri ya injili ambao wote wanasikia, lakini si wote ambao wanaokoka. Je, ni kwa nini kuna wale ambao wanasikia mahubiri ya neno la Mungu na wanayatii na kuokoka, na kuna wale ambao wanasikia mahubiri haya haya, lakini hawaokoki?

Jibu la swali hili linapatikana mahali kwingi katika Agano Jipya. Katika kifungu hiki, Petro anasema, “Mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo” (mstari 23). Yaani, tunaweza kusema kwamba injili inahubiriwa kwa wote, lakini Mungu anapanda neno lake katika mioyo ya wachache. Wao wameitwa na Mungu na wamewezeshwa kuja. Mwito huu ni kama ule mwito ambao Yesu alimwita Lazaro, “Lazaro, njoo huku” (Yohana 11:43). Wakati Kristo aliongea maneno haya alimpatia Lazaro uwezo wa kutii neno lake na kuja.

Jambo hili pia tunalipata wakati injili inahubiriwa. Watu wote wanasikia mahubiri ya neno la Mungu, lakini ni wachche tu ambao Mungu anafanya kazi yake ndani mwao ili wao waweze kuyasikia mahubiri na kuyatii. Kwa watu hawa, Mungu anaongea kwa mioyo yao, si kwa masikio yao pekee. Wakati Mungu anaongea kwa mioyo yao, wao macho ya roho zao yanafunguka na masikio ya mioyo yao pia yanafunguka ili yule mtu aweze kufahamu thamani ya Yesu Kristo. Kwa hivyo moyo wa huyu mtu unampokea Kristo kwa furaha. Hii ndiyo kazi Mungu anafanya wakati Yeye anamwita mtu kupitia kwa injili (1 Petro 2:9; 5:10).

Wakati tunasoma 1 Wakorintho 1:22-24, tunaona jambo hili la kumwita mtu kupitia kwa mahubiri ya injili wazi sana. Hapa

Paulo anasema, “Wayahudi wanataka miujiza na Wayunani wanatafuta hekima, lakini sisi tunamhubiri Kristo aliyesulibiwa, ambaye kwa Wayahudi ni kitu cha kukwaza na kwa Wayunani ni upuzi. Lakini kwa wale ambao Mungu anawaita, yaani, Wayahudi na Wayunani, Kristo ni nguvu na hekima ya Mungu.” Paulo hapa anasema kwamba wote wanasikia ujumbe wa injili: Wayahudi na Wayunani. Lakini kuna Wayahudi wachache na Wayunani wachache ambao Mungu anafanya kazi Yake ndani mwao. Kwao, Kristo sasa si kitu cha kukwaza au upuzi. Wao sasa wanafahamu kwamba Kristo ni nguvu ya Mungu na hekima ya Mungu. Je, ni kwa nini hawa wachache wanafahahmu Kristo ni nani? Ni kwa sababu wao wameitwa: “Lakini kwa wale ambao Mungu anawaita.” Mungu aliwaita wao wachache mioyoni mwao na alifungua macho yao, na wao waliona kwamba Kristo kweli ni nguvu na hekima ya Mungu.

Hii ni njia ya tatu ambayo Mungu anatumia kuwazaa watu mara ya pili. Katika sura hii kwa hivyo tumeona mambo matatu ambayo Mungu anafanya wakati anawazaa watu mara ya pili:

1. Yeye alitukomboa kutoka kwa dhambi na ghadhabu yake kupitia kwa damu ya Yesu Kristo na alilipa deni la wenye dhambi ili wao waweze kuwa na uzima wa milele.

2. Yeye alimfufua Kristo kutoka kwa wafu ili wale ambao wameunganishwa naye waweze kupata uzima wa milele ambao hauishi.

3. Yeye alituita kutoka kwa giza na kuingiza nuruni, na kutoka kwa kifo kwa kutupatia maisha mapya kupitia kwa mahubiri ya injili, na alitupatia macho kuona na masikio kusikia. Yeye alifanya mwangaza wa utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo kung’aa ndani ya mioyo yetu kupitia kwa injili. Hii ndiyo sababu tuliamini na tulimshika Kristo kwa sababu tulifahamu Yeye ni wa thamani.

Ikiwa wewe umeokoka, ninaomba kwamba utafahamu vizuri ni nini Mungu amefanya ili akuokoe. Je, unafahamu ni nini Mungu amefanya kwa ajili yako na ndani ya moyo wako? Wewe umekombolewa na damu ya Kristo ambayo haiharibiki. Umefufuliwa na Kristo kutoka kwa wafu na kupewa maisha ya milele. Umeitwa kutoka kwa wafu kama Lazaro na umeona kwamba Kristo ni wa thamani sana. Umezaliwa mara ya pili. Ulimpokea Kristo na umeokoka.

Pengine wakati unapata majaribu mengi unasoma Warumi 8:28, "Nasi tunajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hutenda kazi pamoja na wampendao, katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi Lake." Ikiwa wewe ni mmoja wao ambao wameitwa na umezaliwa mara ya pili, kumbuka kwamba Mungu hutumia kila kitu kwa faida yako. Na ikiwa wewe hujazaliwa mara ya pili, sikia mwito wa Mungu leo! Sikia mwito wake katika injili ya Yesu Kristo na uje kwake kwa kumwamini. Ukimpokea Kristo atakuokoa kutoka kwa ghadhabu ya Mungu na Yeye atatumia kila kitu kwa faida yako ya milele.

*"Wakumbushe watu kuwanyenyekea watawala na kuwatii wenye mamlaka, wawe tayari kutenda kila lililo jema. Wasimnenee mtu ye yote mabaya, wasiwe wagomvi, bali wawe wapole, wakionyesha unyenyekevu kwa watu wote. Maana sisi wenyewe wakati fulani tulikuwa wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa wa tamaa mbaya na anasa za kila aina. Tuliishi katika uovu na wivu, tukichukiwa na kuchukiana sisi kwa sisi. Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu, ambaye Mungu alitumiminia kwa wingi kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu, ili kwamba, tukiisha kuhesabiwa haki kwa neema Yake, tupate kuwa warithi tukiwa na tumaini la uzima wa milele. Hili ni neno la kuaminiwa. Nami nataka uyasisitize mambo haya, ili wale ambao wamemwamini Mungu wapate kuwa waangalifu kujitoa kwa ajili ya kutenda mema wakati wote. Mambo haya ni mazuri tena ya manufaa kwa kila mtu".*

Tito 3:1-8

# Kuzaliwa upya kwa viumbe vyote

Katika kifungu hiki tunasoma kwamba Mungu, "Alituosha, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu" (Tito 3:5).

Katika kitabu hiki tumeangalia kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha nini (sura ya kwanza hadi nne), na halafu, tumeangalia ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili (sura ya tano hadi nane). Halafu katika sura iliyopita (sura ya tisa) tulianza kuangalia ni namna gani mtu anazaliwa mara ya pili. Katika sura hii, tunataka kuendelea kuangalia jambo hili, ni namna gani mtu anazaliwa mara ya pili. Lakini kabla ya kuangalia jambo hili, tunataka kuchunguza kwa uangalifu kifungu hiki cha Tito 3:1-8. Katika kifungu hiki tunapata mafundisho fulani kuhusu kuzaliwa mara ya pili.

Biblia inatufundisha kwamba si wanadamu pekee ambao wanazaliwa tena, Yesu Kristo alifundisha kwamba viumbe vyote vitazaliwa mara ya pili. Kristo alisema, "Amin, amin, nawaambia, wakati wa kufanywa upya vitu vyote, wakati mwana wa Adamu atakapoketi kwenye kiti chake cha utukufu cha enzi, ninyi mliomfuata pia mtaketi katika viti vya enzi kumi na viwili, mkiyahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli" (Mathayo 19:28). Yesu Kristo hapa anatufundisha kwamba kutakuwa na wakati ambapo viumbe vyote vitaumbwa upya. Hii ndiyo sababu Biblia inaongea kuhusu, "mbingu mpya na dunia mpya" (Isaya 65:17; 66:22).

Kristo hapa anasema siku moja viumbe vyote vitakuwa vipya, yaani viumbe vyote vitaumbwa tena na kuzaliwa tena. Hii ni kwa

sababu si wanadamu pekee ambao wameharibiwa na dhambi, bali viumbe vyote vimeharibiwa na dhambi. Wakati Adamu na Hawa walianguka dhambini, Mungu alilaani viumbe vyote kuwaonyesha wanadamu ubaya wa dhambi. Ugonjwa na uovu na mambo kama mitetemeko na njaa yanatendeka kwa sababu dhambi iliingia hapa ulimwenguni.

**Kuzaliwa upya kwa viumbe vyote.**

Katika Biblia tunasoma, "Kwa kuwa viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali kwa mapenzi Yake Yeye aliyevitiisha katika tumaini, ili kwamba viumbe vyote vipate kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa uchungu kama utungu wa wakati wa mwanamke kuzaa hata sasa. Wala si hivyo viumbe peke yao, bali hata sisi ambao ndio matunda ya kwanza ya Roho, kwa ndani tunalia kwa uchungu tukisubiri kwa shauku kufanywa wana wa Mungu, yaani, ukombozi wa miili yetu" (Warumi 8:20-23).

Kifungu hiki kinatufundisha ni nini Kristo alimaanisha wakati Yeye alisema kwamba viumbe vyote vitazaliwa mara ya pili. Kwa hivyo wakati tunaangalia mafundisho ya Biblia hapa, tunaona haya: ni lengo la Mungu kwamba viumbe vyote vizaliwe mara ya pili. Hii inamaanisha kwamba ulimwengu wote utakuwa upya na yale mambo ambayo yalikuja hapa kwa sababu ya dhambi kama ugonjwa na mambo mabaya mabaya, yote yataondolewa na viumbe vyote vitakuwa vipya.

Katika Tito 3:5, wakati Paulo anasema kwamba Mungu, "Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili," yeye anamaanisha kwamba kuzaliwa mara ya pili kwetu ni sehemu ya kuzaliwa mara ya pili ya kiumbe chote. Wale ambao wamezaliwa mara ya pili sasa ni mifano wa jinsi Mungu siku moja atafanya

viumbe vyote kuwa vipya. Wao ni watu wapya na wanaanza maisha yao tena kuonyesha kwamba siku moja viumbe vyote vitazaliwa mara ya pili na kuanza maisha mapya. Hii ndiyo sababu Paulo anasema kwamba sisi ambao tumeokoka ni “matunda ya kwanza ya Roho,” na pia kwamba sisi, “ndani tunalia kwa uchungu tukisubiri kwa shauku kufanywa wana wa Mungu.” (Warumi 8:23).

Kwa hivyo wakati unawaza juu ya kuzaliwa mara ya pili kwako, kumbuka kwamba wewe ni mfano wa yale ambayo yatatendeka kwa ulimwengu wote. Siku moja, mwili wako utakuwa mpya na viumbe vyote vitakuwa kipya. Lengo la Mungu si kuzaa nafsi zetu mara ya pili pekee. Akifanya hivyo tu, nafsi zetu ambazo zimezaliwa mara ya pili zitaishi ndani ya miili ambayo haitakuwa mipya, na pia tutaishi miongoni mwa viumbe ambavyo vina madhara ya dhambi ndani yake. Hii haiwezekani. Siku moja, nafsi zetu zitakuwa mpya, miili yetu itakuwa mipya na viumbe vyote vitakuwa vipya.

Kwa hivyo katika kifungu hiki cha Tito 3:5, Paulo anaongea kuhusu kazi ya Mungu kufanya watu wake wapya na pia lengo la Mungu kufanya viumbe vyote kuwa vipya: “Alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu.” Hii ndiyo sababu katika kifungu hiki Paulo anasema, “Tukiishi kuhesabiwa haki kwa neema Yake, tupate kuwa warithi tukiwa na tumaini la uzima wa milele” (Tito 3:7). Wakati Paulo hapa anasema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili watakuwa warithi, anamaanisha kwamba wao watakuwa warithi wa ulimwengu wote ambao utakuwa upya. Anamaanisha kwamba wao watakaa katika ulimwengu huu na wote ambao wamezaliwa mara ya pili na wataishi maisha mapya humu.

*"Wakumbushe watu kuwanyenyekea watawala na kuwatii wenye mamlaka, wawe tayari kutenda kila lililo jema. Wasimnenee mtu ye yote mabaya, wasiwe wagomvi, bali wawe wapole, wakionyesha unyenyekevu kwa watu wote. Maana sisi wenyewe wakati fulani tulikuwa wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa wa tamaa mbaya na anasa za kila aina. Tuliishi katika uovu na wivu, tukichukiwa na kuchukiana sisi kwa sisi. Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu, ambaye Mungu alitumiminia kwa wingi kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu, ili kwamba, tukiisha kuhesabiwa haki kwa neema Yake, tupate kuwa warithi tukiwa na tumaini la uzima wa milele. Hili ni neno la kuaminiwa. Nami nataka uyasisitize mambo haya, ili wale ambao wamemwamini Mungu wapate kuwa waangalifu kujitoa kwa ajili ya kutenda mema wakati wote. Mambo haya ni mazuri tena ya manufaa kwa kila mtu".*

Tito 3:1-8

# Mungu anatuzaa mara ya pili kwa kutuosha na kwa kutufanya watu wapya

Katika kifungu hiki cha Tito 3:1-8, Paulo anatufundisha mambo matuatu. Kwanza, anatufundisha ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili, halafu pili anatufundisha ni kwa nini Mungu anatuzaa mara ya pili, na tatu, anatufundisha ni namna gani Mungu anatuzaa mara ya pili.

**1. Ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili.**

Paulo anasema, "Maana, sisi wenyewe wakati fulani tulikuwa wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa wa tamaa mbaya na anasa za kila aina. Tuliishi katika uovu na wivu, tukichukiwa na kuchukiana sisi kwa sisi" (Tito 3:3). Hapa Paulo anaongea kuhusu moyo wa mwanadamu na anasema kwamba mwanadamu ana moyo ambao umejawa na dhambi na anayo tabia ya dhambi.

Tunahitaji kuzaliwa mara ya pili kwa sababu Mungu hataruhusu mtu ambaye ana moyo wa dhambi kuishi katika mbingu mpya na nchi mpya. Kama vile Kristo alisema, ikiwa mtu hajazaliwa mara ya pili, basi yeye hataona Ufalme wa Mungu (Yohana 3:3). Hii ndiyo sababu tunahitaji kuzaliwa mara ya pili: tunahitaji kubadilishwa.

**2. Ni kwa nini Mungu anatuzaa mara ya pili.**

Baada ya kuandika maneno haya, Paulo anaandika, "Lakini...Mungu." Haya ni maneno ya thamana sani. Sisi ambao tumeokoka, zamani tulikuwa "wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa

wa tamaa mbaya na anasa za kila aina." Hii ndiyo ilikuwa hali yetu kabla ya kuokoka. "Lakini neema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa" (Tito 3:4). Hili ni jambo ambalo tunaona katika kitabu cha Waefeso na sura ya pili. "Sisi sote pia tuliishi katikati yao hapa zamani, tukifuata tamaa za mwili na mawazo yake. Nasi kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu, kama mtu mwingine ye yote. Lakini Mungu, kwa upendo wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Kristo Yesu, yaani, mmeokolewa kwa neema" (Waefeso 2:3-5). Sisi tulikuwa wafu lakini Mungu alitufanya hai. Hii ndiyo maana ya neema. Wale ambao wamekufa hawawezi kufanya chochote kuwa hai. Lakini Mungu anawafanya hai.

Hili ni jambo ambalo Paulo anafundisha hapa katika Tito 3:3-5. Sisi tulikuwa watumwa wa tamaa na anasa ambazo zilikuwa na nguvu nyingi na kwa hivyo hatukuweza kuona kwamba Bwana ni mwema. Sisi tulikuwa tumekufa, na kwa hivyo hatukuwa na uwezo wa kumwamini Mungu na kumpenda. Lakini Mungu ni Mungu wa upendo: "Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu" (Tito 3:4-5).

### 3. Ni namna gani Mungu anatufaya tuzaliwe mara ya pili.

Kwa hivyo, sasa tunaangalia jambo hili: je, ni namna gani Mungu anatuzaa mara ya pili? Je, ni namna gani jambo hili la kuzaliwa mara ya pili linafanyika? Katika kifungu hiki, Paulo anasema kwamba kuzaliwa mara ya pili kunajumlisha mambo mawili: kutakaswa na kufanywa mpya. Paulo anasema hapa, "Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu" (Tito 3:5). Kumbuka kwamba Yesu Kristo alisema, "Hakuna mtu ye yote anayeweza kuingia katika

Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa kwa maji na kwa roho" (Yohana 3:5). Tazama kwamba mafundisho ya Yesu Kristo na yale ya Paulo ni sawa: wote wawili wanasema kwamba kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kutakaswa na kuwa mtu mpya. Vile tumeona katika sura ya nne, hili pia ni jambo ambalo tunapata katika Agano la Kale: "Nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi, nitawatakasa kutoka katika uchafu wenu wote na kutoka katika sanamu zenu zote. Nitawapa moyo mpya na kuweka roho mpya ndani yenu...Nami nitaweka Roho yangu ndani yenu na kuwafanya ninyi mfuate amri zangu" (Ezekieli 36:25-27). Katika kitabu cha Yohana sura ya 3, Yesu Kristo alifundisha hivi: "Wakati wa Agano Jipya umefika. Ile ambayo Mungu alituahidi katika unabii wa Ezekieli imetabiriwa kupitia kwa kazi ya Roho Mtakatifu na kupitia Kwangu. Roho Mtakatifu anawapa maisha (Yohana 6:63), na mimi ndimi njia na kweli na uhai (Yohana 14:6). Wakati Roho Mtakatifu anawaunganisha kwa Kristo ninyi mtazaliwa mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kutakaswa na kuwa watu wapya." Haya, kwa jumla, ni mafundisho ya Yesu Kristo wakati aliongea na Nikodemo.

Haya yalikuwa mafundisho ya Yesu Kristo, na haya yalikuwa mafundisho ya Paulo wakati aliandika, "Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu" (Tito 3:5). Paulo anamaanisha kwamba ahadi za Agano Jipya zimetabiriwa, kazi ya Mungu kufanya viumbe vyote vipya imeanza. Na Paulo anasema kwamba wale ambao tayari wamezaliwa mara ya pili ni dhihirisho kwamba Mungu siku moja atatakasa na kuzaa viumbe vyote vipya. Paulo anawaambia wale ambao wamezaliwa mara ya pili, "Ninyi mmeumbwa tena na Roho Mtakatifu, na ninyi sasa ni watu safi na watu wapya. Hii ndiyo maana ya kuzaliwa mara ya pili."

Je, ni namna gani Mungu alifanya kazi hii ya kuzaa watu mara ya pili? Paulo hapa anasema kwamba Mungu alifanya kazi hii si kwa sababu ya matendo ambayo sisi wenyewe tumetenda, bali ni kwa

sababu ya Yeye ni nani. Katika Tito 3:4-5, Paulo anasema mambo matatu kumhusu Mungu. Paulo anaandika, "Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake. Alituokoa kwa kutuosha, kwa kuzaliwa mara ya pili na kufanywa wapya kwa njia ya Roho Mtakatifu" (Tito 3:4-5). Katika kifungu hiki lengo lake ni kutufundisha kuhusu wokovu: "Alituokoa." Njia ambayo Mungu anatuokoa ni kuzaa watu wake mara ya pili. Paulo anasema haya mambo mawili ni kwa sababu ya wema wake Mungu na kwa rehema Zake. Hii ndiyo sababu Mungu anazaa watu mara ya pili: Yeye ni Mungu Mwema, Mungu wa upendo na Mungu wa rehema.

**Tunazaliwa mara ya pili kwa sababu ya neema ya Mungu.**

Ikiwa wewe umezaliwa mara ya pili, yaani, ikiwa wewe umeamshwa kutoka kwa kifo cha kiroho na umepewa macho ya kuona na masikio ya kusikia na unafahamu kwamba Yesu Kristo ndiye Mwokozi, na pia ikiwa umepewa moyo wa kumwamini Kristo, haya yote ni kwa sababu ya neema ya Mungu. Paulo anatueleza kuhusu neema ya Mungu hivi: "Ili katika ule ulimwengu ujao apate kuonyesha wingi wa neema Yake isiyopimika, iliyodhihirishwa kwetu kwa wema Wake ndani ya Kristo Yesu" (Waefeso 2:7).

Mungu anapenda sana kuonyesha neema Yake kwa watu wake. Mungu ni mwumba wa ulimwengu na dunia na anatawala viumbe vyote hapa duniani (Mathayo 10:29-30). Yeye ni mwenye nguvu zote na mwenye hekima na mtakatifu na mwenye haki. Na pia Yeye ni mwenye rehema: "wema wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa" (Tito 3:4). Tumezaliwa mara ya pili kwa sababu ya rehema ya Mungu. Wewe ambaye umeokoka, kumbuka kila lisaa na kila siku kwamba wewe umezaliwa mara ya pili kwa sababu ya wema wa Mungu. Mungu amekurehemia.

### Tunazaliwa mara ya pili kwa sababu ya upendo wa Mungu.

Jambo la pili ambalo Paulo anasema hapa ni kwamba Mungu ni Mungu wa upendo. Mungu anawapenda wanadamu, na Mungu anapenda kuwafanyia wanadamu wema. Kwa hivyo Paulo hapa anasema kwamba ikiwa wewe umezaliwa mara ya pili, hii ni kwa sababu ya upendo wa Mungu na ni kwa sababu Mungu anapenda kuwabariki wanadamu.

Katika kifungu hiki, Paulo anasema upendo huu wa Mungu ulifunuliwa: "Lakini wema na upendo wa Mungu Mwokozi wetu ulipofunuliwa, alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya rehema Zake" (Tito 3:4). Halafu katika mstari wa 6 Paulo anasema kwamba Yesu Kristo ndiye Mwokozi wetu: "Kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu." Yaani Paulo anasema kwamba Mungu, ambaye ni Mwokozi wetu, alifunuliwa katika Yesu Kristo ambaye ni Mwokozi wetu. Kwa hivyo wakati Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni, wema na upendo wa Mungu ulifunuliwa.

Hii inamaanisha kwamba tunazaliwa mara ya pili kwa sababu ya kazi yake Yesu Kristo. Hili ni jambo ambalo tumeona katika kitabu hiki. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili amezaliwa, kwa sababu ameunganishwa kwa Yesu Kristo ambaye alikuja hapa ulimwenguni kuwaokoa wenye dhambi. Tunazaliwa mara ya pili kwa sababu Kristo alikuja hapa ulimwenguni na wema na upendo wa Mungu ulifunuliwa ndani Yake, na kwa sababu Yeye alikufa kwa ajili ya wenya dhambi na kufufuka.

### Tumezaliwa mara ya pili si kwa sababu matendo mazuri ambayo tumeyatenda.

Jambo la tatu ambalo Paulo anasema hapa ni kwamba Mungu ni Mungu wa rehema. Paulo anasema kwamba Mungu, "alituokoa, si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa sababu ya

rehema Zake" (Tito 3:5). Ikiwa wewe umezaliwa mara ya pili hii ni kwa sababu ya rehema ya Mungu. Mungu ni mwenye rehema, sisi hatustahili kuzaliwa mara ya pili, sisi tulikuwa watu wagumu na tulipuuza neno lake na tulikuwa tumekufa kwa dhambi. Mungu angeweza kutuacha katika dhambi zetu na kutuhukumu. "Lakini Mungu, kwa upendo Wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni mwingi wa rehema, hata tulipokuwa wafu kwa ajili ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Yesu Kristo, yaani, mmeokolewa kwa neema" (Waefeso 2:4-5). Sisi tumezaliwa mara ya pili na kufanywa watu wapya kwa sababu ya rehema ya Mungu.

Mungu ni mwema, Mungu ni Mungu wa upendo na Mungu ni mwenye rehema. Hii ndiyo sababu tumezaliwa mara ya pili. Paulo anafundisha haya yote katika kifungu hiki cha Tito 3:1-8. Lakini Paulo hakuachia hapo. Yeye aliendelea kusema, "Si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda" (Tito 3:5). Paulo anajua moyo wa mwanadamu. Yeye anajua kwamba ikiwa mtu amepata baraka fulani, yeye atawaza kwamba ni kwa sababu amefanya kitu fulani kizuri. Hii ndiyo sababu Paulo aliandika maneno haya.

Wakati unapowaza juu ya wewe kuzaliwa mara ya pili, usiwaze hivyo. Kumbuka kwamba hapa Paulo anasema kwamba sisi tumezaliwa mara ya pili si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyotenda. Usiwaze kwamba ulitenda matendo ya haki na umezaliwa mara ya pili kwa sababu ya haya matendo ya haki. Ukweli ni kwamba wewe unatenda matendo ya haki kwa sababu umezaliwa mara ya pili, si kwamba umezaliwa mara ya pili kwa sababu ulitenda matendo ya haki.

Hii ndiyo sababu wakati Paulo anasema kwamba Mungu alituosha, yeye hamaanishi ubatizo. Sisi hatujazaliwa mara ya pili kwa sababu ya kubatizwa. Tunazaliwa mara ya pili kwa sababu ya wema wa Mungu na upendo wa Mungu na rehema ya Mungu ambayo ni bila malipo. Ni haya mambo matatu ambayo yanatueleza kuzaliwa mara ya pili kwetu. Tumezaliwa mara ya

pili si kwa sababu tumebatizwa au tumetahiriwa au kwa sababu tumetenda matendo mema. Mtu kwanza anazaliwa mara ya pili na halafu anatenda matendo mema. Matendo mema ni matunda ya kuzaliwa mara ya pili.

Ninaomba kwamba Mungu atafungua macho yako ili uone kwamba umezaliwa mara ya pili kwa sababu ya wema na upendo na rehema Yake, na kwamba utakuwa mtu wa unyenyekevu na kumtii na kumtumikia Mungu.

# Mungu anatuzaa mara ya pili kupitia kwa imani

Katika kitabu hiki ninataka kuandika yale mambo tu ambayo yatakuwa ya maana na yatakufaidi katika maisha yako. Hii ndiyo sababu katika sura hii ninaendelea kufundisha ni namna gani mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili. Katika kitabu hiki siandiki kuhusu mambo ya dunia kama umaskini na ukimwi na mambo kama haya, kwa sababu kuna jambo moja ambalo ni la maana na ambalo litakufaidi, na hili ni kujua ni namna gani unaweza kuzaliwa mara ya pili. Baada ya mtu kuzaliwa mara ya pili, yeye anaweza kujali haya mambo mengine na kujaribu kuwasaidia maskini na mambo kama hayo. Lakini jambo la kwanza ambalo unahitaji kufahamu ni namna gani mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili.

Yesu Kristo alisema, “Mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili” (Yohana 3:3). Yule ambaye hawezi kuuona Ufalme wa Mungu ndiye yule ambaye hawezi kuingia ndani ya ufalme wa Mungu. Yesu Kristo alisema kwamba wale ambao hawamo ndani ya Ufalme wa Mungu “Watatupwa katika giza la nje, ambako kutakuwa na kulia na kusaga meno” (Mathayo 8:11-12). Pia Kristo alisema kwamba hapa ni mahali pa hukumu ya milele (Mathayo 25:46). Yaani kuna mahali pa hukumu ya milele, na kuna Ufalme wa Mungu, ambako ni mahali pa furaha ya milele katika ushirika na Mungu na Yesu Kristo mwenyewe (Yohana 17:24).

Hii ndiyo sababu jambo hili la kuzaliwa mara ya pili ni la muhimu sana kuliko mambo yote mengine. Jambo la muhimu sana ni kujua na kufahamu utukufu wa Yesu Kristo. Siku moja, utukufu wake utajaza viumbe vyote na Yeye mwenyewe ataishi miongni mwa viumbe vyake.

**Ni nini unahitaji kufanya ukitaka kuzaliwa mara ya pili.**

Katika sura hii, ninataka kuuliza swali hili: je, ni nini sisi wanadamu tunapaswa kufanya ili tuzaliwe mara ya pili? Kwanza, wacha nikupe lile jibu ambalo linapatikana katika Biblia, halafu nitakuonyesha jibu hili linapatikana wapi katika Biblia.

Wewe ukitaka kuzaliwa mara ya pili, unahitaji kumwamini Yesu Kristo ambaye alikufa juu ya msalaba na alifufuka. Unahitaji kumwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi wako na Bwana wako na Mkuu wa maisha yako yote. Njia ya kuokoka ni kumwamini Kristo, ni kumpokea Yesu Kristo kama vile anavyofunuliwa katika neno la Mungu.

Wakati utamwamini Kristo, dakika ile ile Mungu atakupatia maisha; Yake ni kukupatia maisha, yako ni kumwamini Kristo. Wewe utamwamini Kristo kwa sababu Yeye amekupatia maisha, kwanza Yeye anakupatia maisha, na kwa sababu anakupatia maisha wewe utamwamini. Kwa mfano, wakati mtu anawasha moto, watu wanapata joto na mwangaza. Haya yote yanakuwa pamoja: moto, joto na mwangaza, lakini ni moto ambao umeleta joto na mwangaza. Vile vile wakati Mungu anakupatia maisha, dakika ile ile utaweza kumwamini Kristo. Hili ndilo jibu ambalo linatoka kwa Biblia, ni nini mwanadamu anahitaji kufanya ili azaliwe mara ya pili. Sasa ninataka kukuonyesha jibu hili limetoka wapi katika Biblia.

**Yule ambaye anataka kuzaliwa mara ya pili anahitaji kutii neno la Mungu.**

Kwanza, tusome 1 Petro 1:22-23: “Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka kwa moyoni. Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa

mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele."

Tazama mambo fulani katika kifungu hiki. Moja, kusudi la yale ambayo yanatendeka ni upendo: "Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni." Yaani, Petro anasema kwamba Mungu anatakasa nafsi zetu kupitia kwa kutii neno la Mungu kwa sababu Yeye ana kusudi la kufanya kazi hii, na kusudi la kufanya kazi hii ni kwamba wale ambao wametakaswa watapenda ndugu zao. Biblia inatuambia kwamba upendo ni tunda la Roho Mtakatifu.

Pia, Petro anasema hapa kwamba hawa wakristo walitii, na kwa sababu walitii, walikuwa na upendo kwa ndugu zao. Yaani, Petro hapa anasema kwamba wakristo ni wale ambao wanatii ukweli wa Mungu, yaani neno la Mungu. Hii ndiyo sababu katika kifungu hiki anasema, "neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele." Pia katika mstari wa 25 anasema, "Neno la Mungu ladumu milele."

Biblia hapa inatufundisha kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wametii neno la Mungu, yaani wameutii ujumbe wa injili na kwa hivyo wamemwamini Yesu Kristo mwenyewe. Ujumbe wa injili unasema kwamba sisi tunahitaji kuwa na imani: "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka" (Matendo ya Mitume 16:31; 1 Wakorintho 15:1-2). Ujumbe wa injili hausemi kwamba kwanza unahitaji kupenda ndugu yako, unasema kwamba kwanza unahitaji kumwamini Yesu Kristo.

Jambo hili tunaliona tena katika maneno haya ya Petro: "Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu, ili kama wako wasioamini lile Neno, wapate kuvutwa na mwenendo wa wake zao pasipo neno" (1 Petro 3:1). Kutotii neno kunamaanisha

kwamba hawa waume hawajaokoka. Petro pia anaongea kuhusu wale ambao hawalitii neno la Mungu (1 Petro 2:8 na 1 Petro 4:17). Wale ambao hawaamini neno la Mungu hawaamini ujumbe wa injili na kwa hivyo hawana wokovu.

Paulo naye anaandika kwamba Mungu, "Atawaadhibu wale wasiomjua Mungu na ambao hawakutii Injili ya Bwana wetu Yesu" (2 Wathesalonike 1:8). Paulo hapa anasema kwamba wakati ujumbe wa Mungu unahubiriwa, unahitaji watu wauamini. Na hapa Paulo anasema kwamba kuna wale ambao wanasikia ujumbe wa injili lakini wanakataa kuuamini. Wao "hawakutii Injili ya Bwana wetu Yesu."

Kwa hivyo wakati Petro anasema, "Mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho" (1 Petro 1:22), anamaanisha kwamba "mmejitakasa nafsi zenu kwa kuamini ujumbe wa injili ya Yesu Kristo na imani hii inawaongoza ninyi katika upendo wa ndugu zenu." Hii ni imani ambayo inafanya kazi kupitia kwa upendo (Wagalatia 5:6). Biblia inasema upendo unatoka kwa moyo safi, dhamira njema na imani ya kweli (1 Timotheo 1:5).

### 2. Yule ambaye anataka kuzaliwa mara ya pili anahitaji kuamini ujumbe wa injili.

Vile tumeona wakati tulisoma 1 Yohana 3:5 na Tito 3:5, wakati tunazaliwa mara ya pili, nafsi zetu zinatakaswa. Ni hii kazi ya kuzaliwa mara ya pili ambayo inatakasa nafsi zetu. Hii ni kuzaliwa mara ya pili. Hii inamaanisha kwamba wakati tunazaliwa mara ya pili tunatakaswa kwa kulitii neno la Mungu. Hii inamaanisha kwamba tunashirikia na Roho Mtakatifu katika hii kazi ya kuzaliwa mara ya pili: ni sisi ambao tunazaliwa mara ya pili. Sisi tunahitaji kuamini ujumbe wa injili ya Yesu Kristo. Bila kuamini, mtu hawezi kuzaliwa mara ya pili.

Vile tumeona, Petro alisema, “Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni. Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele” (1 Petro 1:22-23).

Yaani, Biblia hapa inatufundisha kwamba tunamwamini Mungu kwa sababu Mungu kwanza anatuzaa mara ya pili. Haya ni mafundisho ya Petro katika kifungu hiki. Wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanajitakasa nafsi zao. Yaani, Biblia hapa inatufundisha kwamba mtu anazaliwa mara ya pili kwa sababu Mungu kwanza anafanya kazi ndani ya moyo wake. Bila kazi ya Mungu ndani ya moyo wa mtu, hakuna yeyote ambaye anaweza kuzaliwa mara ya pili hadi kwanza Mungu afanye kazi yake ndani ya moyo wa yule mtu. Hii ndiyo sababu kuna wengi ambao wanasikia neno la Mungu lakini hawaliamini na hakuzaliwi mara ya pili. Ni kwa sababu Mungu hajafanya kazi yake kwanza ndani yao.

**Bila kazi ya Mungu ndani yetu kwanza, hatuwezi kuzaliwa mara ya pili.**

Petro anafundisha wazi kwamba Mungu kwanza anatuzaa mara ya pili, na halafu sisi tunamwamini Kristo. Kazi ya Mungu inakuja kwanza, halafu sisi tunatii neno lake kwa kumwamini Kristo. Katika kifungu hiki cha 1 Petro 1:13-25, Petro anatufundisha jambo hili kwa njia tatu.

1. Kwanza, Petro anasema, “Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuutii ule ukweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka kwa moyoni.” Angalia hapa kwamba Petro anasema, “Pendeni kwa dhati kutoka moyoni,” lakini kabla ya amri hii, anaandika, “Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu.” Yaani, Petro anajua

kwamba kwanza Mungu anawazaa watu mara ya pili, na baada ya kazi hii ya Mungu watu hawa wanaweza kuamini ujumbe wa injili ambao unatakasa mioyo yao, na pia wao wanaweza kuwapenda ndugu zao. Kazi ya Mungu kuwazaa watu wake inakuja kwanza.

2. Pili, tunaona kwamba kwanza Mungu anafanya kazi yake ya kuwazaa watu, na halafu hawa watu wanamwamini kwa sababu Petro anasema kwamba neno la Mungu ni chombo ambacho Mungu anatumia kumzaa mtu mara ya pili. Petro aliandika, “Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele.” Wakati Petro anaongea kuhusu mbegu ile isiyoharibika, anamaanisha neno la Mungu, na kwa hivyo hapa Petro anasema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili, wamezaliwa kupitia kwa neno la Mungu.

Kwa hivyo Biblia hapa inatufundisha kwamba Mungu anatumia neno lake wakati anamzaa mtu mara ya pili kwa kumpatia imani. Hii ndiyo jambo ambalo Paulo alifundisha: “Basi, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo” (Warumi 10:17). Hii inamaanisha kwamba kazi ya kumzaa mtu mara ya pili ni ya Mungu: Mungu anatumia neno lake kumpatia mtu imani ili aweze kuamini ujume wake. Hii pia ni mafundisho ya Yakobo: “Kwa mapenzi Yake mwenyewe alituzaa kwa neno la kweli” (Yakobo 1:18). Yakobo hapa anasema wazi kwamba Mungu alituzaa kwa mapenzi Yake mwenyewe. Mungu kwanza hakuona ni nani anaamua kuzaliwa mara ya pili, kazi ya kuwazaa watu mara ya pili ni kazi ya Mungu pekee.

3. Tatu, wakati tunasoma Matendo ya Mitume 15:9, tunaona kwamba hii kazi ya kuzaa mtu mara ya pili ni kazi ya Mungu na ni kazi ambayo yeye anafanya kwanza, na halafu sisi tunamwamini. Hapo, Petro anasema, “Mungu hakutofautisha

kati yetu na wao, bali alitakasa mioyo yao kwa imani." Angalia vizuri ni nini Petro anasema hapa. Petro anasema kwamba ni Mungu ambaye anatakasa mioyo ya watu. Yeye hasemi hapa ni watu ambao kwanza wanatakasa mioyo yao na halafu kuja kwa Mungu. Hii inatuonyesha kwamba kazi ya kuwazaa watu mara ya pili ni kazi ya Mungu na si ya wanadamu. Pia tunaona kwamba wakati Mungu anafanya kazi hii, anatupatia imani.

**Haya yote yanamaanisha nini kwetu.**

Mafundisho haya yote yanamaanisha mambo manne kwetu.

1. Kwanza, yanamaanisha kwamba sisi tunahitaji kuamini ikiwa tutaokoka: "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka" (Matendo ya Mitume 16:31). Bila kuamini hatuwezi kuzaliwa mara ya pili. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili ana imani.

2. Pili, yanamaanisha kwamba bila kazi ya Mungu ndani yetu, sisi hatuwezi kuamini. Yule ambaye amekufa kwa kimwili hawezi kupumua, ya yule ambaye amekufa kwa kiroho hawezi kuamini.

3. Tatu, yanamaanisha kwamba Mungu ambaye ni Mungu wa rehema na upendo kuu na neema ndiye Yule ambaye anatupatia imani.

4. Nne, Petro anasema katika 1 Petro 1:22 kwamba tunda la ule moyo ambao umezaliwa mara ya pili ni upendo. Hii inamaanisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili, maisha yake yatabadilika katika kila sehemu. Yeye atawajali watu wengine.

Kwa hivyo ninakusihi, mwamini Yesu Kristo. Mpokee kuwa Mwokozi wako, Bwana wako. Na ikiwa wewe tayari umezaliwa

mara ya pili, ujinyenyekeze chini ya mkono wa Mungu wa neema, na hakikisha kwamba maisha yako ni maisha ya upendo kwa watu wote wa ulimwengu.

*“Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu. Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna cho chote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu. Nuru hung’aa gizani nalo giza halikuishinda. Alikuja mtu mmoja aliyetumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana. Alikuja kama shahidi apate kuishuhudia hiyo nuru, ili kwa kupitia yeye watu wote waweze kuamini. Yeye mwenyewe hakuwa ile nuru, bali alikuja kuishuhudia hiyo nuru. Nuru halisi, imwangaziayo kila mtu ilikuwa inakuja ulimwenguni. Alikuwepo ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, haukumtambua. Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea. Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake. Hawa watoto wamezaliwa si kwa damu wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu. Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi takauona utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli”.*

Yohana 1:1-14

# Tunazaliwa mara ya pili kupitia kwa mahubiri ya ujumbe wa Biblia

Kama vile tuliona katika sura iliyopita, Petro anasema kwamba sisi tumezaliwa mara ya pili, "si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele" (1 Petro 1:23). Hapa Petro anasema kwamba tumezaliwa mara ya pili, yaani Roho Mtakatifu ametuunganisha kwa Yesu Kristo kupitia kwa neno la Mungu. Muujiza huu wa kuzaliwa mara ya pili, wa kuondolewa kutoka kwa kifo na kuwa na maisha unafanywa kupitia kwa kusikia neno la Mungu. Halafu Petro anaendelea kutueleza anamaanisha nini wakati anasema kwamba tumezaliwa mara ya pili kupitia kwa neno la Mungu. Anasema, "Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu" (1 Petro 1:25). Yaani, Petro anasema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili, wamezaliwa mara ya pili kwa sababu wamesikia neno la Mungu, ambalo ni ujumbe wa injili.

### Ujumbe wa injili ni nini.

Biblia inatufundisha ujumbe huu wa injili ni nini. Paulo aliandika, "Basi ndugu zangu nataka niwakumbushe kuhusu Injili niliyowahubiria, mkaipokea na ambayo katika hivyo mmesimama. Kwa Injili hii mnaokolewa mkishikilia kwa uthabiti neno nililowahubiria ninyi. La sivyo, mmeamini katika ubatili. Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemayo Maandiko, ya kuwa alizikwa na alifufuka siku ya tatu, na kwamba alimtokea Kefa, kisha akawatokea wale kumi na wawili" (1 Wakorintho 15:1-5).

Ujumbe wa injili unahusu matendo ambayo yalitendeka na maana ya yale matendo. Ujumbe huu unahusu matendo ambayo watu waliweza kuyaona na macho yao na kuwaza juu yake na kuongea juu yake. Huu ni ujumbe kuhusu kifo cha Yesu Kristo na kufufuka kwake. Ujumbe wa injili ni yale mafundisho ambayo tunapata katika Biblia kumhusu Yesu Kristo na kifo chake na kufufuka kwaka. Hii ndiyo sababu Paulo anasema, "Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemayo Maandiko."

Paulo anasema hapa kwamba tunaokolewa wakati tunaamini ujumbe huu, yaani tunasikia na kufahamu ujumbe wa injili na kuupokea na kuuamini. Hii ndiyo sababu Paulo anasema, "hili ndilo tulihubirilo na hili ndilo mliaminilo" (1 Wakorintho 15:11). Haya ni mafundisho ya Biblia kila mahali, kwamba ujumbe wa injili ulihubiriwa na wale ambao waliupokea na kuuamini waliokoka. Paulo anasema, "Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo" (Warumi 10:17); na, "Mlipokea Roho wa Mungu kwa kushika sheria, au kuyaamini yale mliyosikia? Je, Mungu huwapa Roho Wake na kufanya miujiza katikati yenu kwa sababu mnatii sheria, au kwa sababu mnaamini kile mlichosikia?" (Wagalatia 3:2;5). Yaani yule ambaye amezaliwa mara ya pili anasikia ujumbe wa injili kwa imani na kwa kusikia kwa imani, anazaliwa mara ya pili kupitia neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele. Hii inamaanisha kwamba neno la Mungu linahubiriwa na watu wanalisikia na kulipokea, na kwa kulipokea, wao wanazaliwa mara ya pili – wao sasa wako na imani. "Kwa mapenzi Yake mwenyewe alituzaa kwa neno la kweli" (Yakobo 1:18).

**Neno alifanyika mwili.**

Sasa katika Yohana 1:1 tunasoma, "Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyu Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu," na katika Yohana 1:14 tunasoma, "Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi takauona

utukufu Wake, utukufu kama wa Mwana wa pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli." Yohanna hapa anatuambia kwamba Yesu Kristo ambaye ni Mungu mwenywe alikuja hapa ulimwenguni kama mwanadamu kamili na aliishi hapa miongoni mwa wanadamu. Biblia inatuambia kwamba Yeye alikuwa ufunuo wa Mungu: wale ambao walimwona Kristo walimwona Mungu.

Pia, Biblia inatufundisha wazi kwamba Yeye alikufa juu ya msalaba kwa ajili ya dhambi zetu. Huu ni ujumbe ambao unahubiriwa na ambao wote wanasikia. Wengi ambao wanasikia ujumbe huu na kwa rehema ya Mungu wanaufahamu na kuupokea. Hii ndiyo njia wao wanazaliwa mara ya pili.

**Tunazaliwa mara ya pili si kwa uwezo wa mwanadamu bali kwa uwezo wa Mungu.**

Tazama ni nini Yohana anasema hapa: "Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea. Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio Jina Lake. Hawa watoto wamezaliwa si kwa damu wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu" (Yohana 1:11-13). Kifungu hiki kimepangwa kama tu vile kifungu cha 1 Petro 1:22-23 kimepangwa. Tunaambiwa hapa kwamba wale ambao wamepewa haki kuwa watoto wa Mungu ndiyo wale ambao wanampokea Kristo na kuamini Jina Lake. Kwa hivyo kuwa mtoto wa Mungu kunamaanisha kumwamini Kristo. Ukimpokea Kristo na kuamini Jina Lake basi wewe ni mtoto wa Mungu, yaani wewe umezaliwa mara ya pili na wewe umo katika jamii ya Mungu milele. Kwa hivyo wale ambao wanamwamini Kristo wao ni watoto wa Mungu. Haya ndiyo mafundisho ya Yohana na ya 1 Petro 1:22.

Halafu katika Yohana 1:13 tunasoma kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wamezaliwa na Mungu mwenyewe.

Yohana anasema, “Hawa watoto wamezaliwa si kwa damu wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu.” Biblia hapa inatufundisha kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wamezaliwa si kwa sababu ya uwezo wao au kwa sababu ya uwezo wa mtu mwingine, bali ni kwa sababu ya uwezo wa Mungu: ni Mungu ambaye anawazaa watu mara ya pili. Yohana anasema hapa kwamba sisi tunazaliwa si kwa sababu ya uwezo wa mwanadamu, yaani si kwamba mtu anaamua kwamba yeye atazaliwa mara ya pili au kwamba mwingine atazaliwa mara ya pili. Haya si mambo ambayo mwanadamu anaweza kuamua kufanya. Pia Biblia hapa inasema mtu hawezi kuwa amezaliwa mara ya pili kwa sababu wazazi wake walikuwa wamezaliwa mara ya pili. Yesu alisema, “Mwili huzaa mwili” (Yohana 3:6). Mwanadamu hawezi kuzaa mwingine mara ya pili, mwanadamu anaweza tu kuzaa mtoto kimwili, si kiroho.

Kwa hivyo mwanadamu hawezi kuzaliwa mara ya pili kwa uwezo wake, ni Mungu pekee ambaye anawazaa watu mara ya pili. Wale ambao wanampokea Kristo na kuamini Jina Lake wanazaliwa mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili ni kazi ya Mungu, si kazi ya mwanadamu. Hili ndilo jambo ambalo kifungu hiki katika kitabu cha Yohana kinatufundisha.

Biblia inatufundisha wazi kwamba kazi ya Mungu ya kumzaa mtu inafanyika kwanza. Mtu kwanza anazaliwa mara ya pili, na halafu baada ya kuzaliwa mara ya pili, anamwamini Yesu Kristo. Biblia inasema, “Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu na ye yote ampendaye Baba humpenda pia mtoto aliyezaliwa naye” (1 Yohana 5:1). Tazama vizuri ni nini Yohana anaandika hapa. Yoahana anasema kwamba yule ambaye anaamini, anaamini kwa sababu yeye tayari amezaliwa mara ya pili: kwanza anazaliwa mara ya pili na halafu anamwamini Kristo.

**Mungu kwanza anatuzaa mara ya pili, na halafu sisi tunamwamini Kristo.**

Kwa hivyo katika sura hii na sura iliyopita, tumejifunza mambo haya: Mungu anafanya kazi kwa kumzaa mtu mara ya pili, na wakati yeye anafanya kazi hii, yule mtu anazaliwa mara ya pili kwa sababu ya kazi ya Mungu. Kabla ya kuzaliwa mara ya pili yeye alikuwa amekufa na hakuamini. Kazi ya kuzaa mtu mara ya pili ni kazi ya Mungu ambayo Yeye anafanya kupitia kwa neno lake ambao ni ujumbe wa injili (1 Petro 1:23; Yakobo 1:18). Injili ya Yesu Kristo kupitia kwa nguvu ya Roho Mtakatifu inamwezesha mtu kufahamu neno la Mungu na inampatia imani. Kabla ya mtu kupewa imani hii, yeye alikuwa kipofu na bila imani. Ujumbe huu unamhusu Yesu Kristo na kazi yake. Unahusu kifo chake Yesu Kristo na kufufuka kwake, na ujumbe huu unafunua utukufu wa Kristo (2 Wakorintho 4:4-6). Ujumbe huu kuhusu maisha ya Kristo na kazi yake ni nguvu za Mungu kumzaa mtu mara ya pili na kumpatia imani (Warumi 1:16).

Kwa hivyo, kuzaliwa mara ya pili kunafanyika wakati mtu anapokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wa maisha yake. Hii ndiyo sababu ninakusihi, mtazame Kristo katika ujumbe wa injili ambayo ni hadithi ya maisha yake na kifo chake na kufufuka kwake. Unahitaji kufahamu kwamba bila Kristo huwezi kuwa na maisha ya milele. Mpokee Kristo na amini Jina Lake na wewe utakuwa mtoto wake.

# Sehemu ya Nne

# Je, matokeo ya kuzaliwa mara ya pili ni gani?

*"Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu na ye yote ampendaye Baba humpenda pia mtoto aliyezaliwa naye. Hivi ndivyo tunavyojua kwamba tunawapenda watoto wa Mungu, kwa kumpenda Mungu na kuzitii amri Zake. Kwa kuwa huu ndio upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito. Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu. Ni nani yule aushindaye ulimwengu? Ni yule aaminiye kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu".*

1 Yohana 5:1-5

# Yule ambaye amezaliwa mara ya pili ataushinda ulimwengu

Katika kitabu hiki, tumeona ni kwa nini tunahitaji kuzaliwa mara ya pili, halafu tuliona kunamaanisha nini kuzaliwa mara ya pili, na halafu tuliona katika sehemu iliyopita ni namna gani mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili. Sasa katika sehemu hii, tunataka kuangalia matokeo ya kuzaliwa mara ya pili na kuuliza maswali haya, je, kuzaliwa mara ya pili kunamwongoza mtu wapi? Je, yule ambaye amezaliwa mara ya pili atazaa matunda gani? Je, kuna ishara gani katika maisha yako kwamba Mungu amekuzaa mara ya pili?

Sasa katika Biblia kuna kitabu kimoja ambacho kimeandikwa kutufundisha ni namna gani tunaweza kujua kwa hakika kama mtu amezaliwa mara ya pili au la, na kitabu hiki ni 1 Yohana. Kitabu hiki cha 1 Yohana kiliandikwa ili yule ambaye anadai ameokoka aweze kujichunguza na kujua kwa kweli kama ameokoka au la.

Ninataka kukuhimiza kusoma na kujifunza kitabu hiki cha 1 Yohana. Kwa hivyo katika sura hii ya kitabu hiki ninataka kukufundisha kwa jumla ni nini kitabu cha 1 Yohana kinafundisha, na ni namna gani kitabu hiki kimepangwa. Halafu baada ya kukufundisha haya, ninataka kuangalia mafundisho ya 1 Yohana 5:3-4.

### Je, ni kwa nini Yohana aliandika kitabu hiki cha 1 Yohana?

Jambo la kwanza ambalo tunahitaji kujua ni, je, ni kwa nini Yohana aliandika kitabu hiki? Katika kitabu hiki, Yohana anatuambia ni kwa nini aliandika kitabu hiki. Katika mistari ifuatayo, Yohana anasema hii:

> "Tunaandika mambo haya ili furaha yetu ipate kuwa timilifu" (1 Yohana 1:4). Yohana hapa anasema kwamba lengo lake la

kuandika kitabu hiki lilikuwa ili wale ambao wameokoka waweze kuwa na furaha kwa sababu wanalo hakikisho kwamba wameokoka. Furaha yao itamletea Yohana furaha.

“Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki (1 Yohana 2:1). Hapa Yohana anatumaini kwamba kitabu chake kitawapatia nguvu za kushinda dhambi. Kwa hivyo anawahimiza kwamba hata kama wameanguka dhambini maishani mwao, hii haimaanishi kwamba wameshindwa kabisa na dhambi.

“Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu dhambi zenu zimesamehewa kwa ajili ya Jina Lake. Nawaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua Yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi vijana kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nawaandikia ninyi watoto wadogo, kwa sababu mmejua Baba” (1 Yohana 2:12-13). Yohana hapa anasema kwamba ana tumaini kwamba wale ambao anawaandikia kweli wameokoka. Wao wamesamehewa dhambi zao, wanamjua Mungu na wamemshinda shetani.

“Siwaandikii kwa sababu hamjui kweli, bali kwa sababu mnaijua, nanyi mnajua hakuna uongo utokao katika kweli” (1 Yohana 2:21). Yohana hapa anasema kwamba lengo lake kuandika kitabu hiki si kuwasaidia kuanza maisha ya ukristo bali kuwahakikishia maisha yao ukristo.

“Ninawaandikia mambo haya kuhusu wale watu ambao wanajaribu kuwapotosha” (1 Yohana 2:26). Yohana alisumbuliwa kwa sababu ya walimu wa uongo, na aliandika kitabu hiki kuwalinda watu wa Mungu. Hata wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanahitaji kuonywa.

> "Nawaandikia mambo haya ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu ili mpate kujua ya kuwa mnao uzima wa milele" (1 Yohana 5:13). Hili ndilo lengo kuu la Yohana kuandika kitabu hiki. Yale ambayo anaandika katika kitabu hiki yanapatikana kwa ufupi katika mstari huu. Yohana anasema hapa, "Ninaandika mambo haya ili mjue kwamba mmezaliwa mara ya pili.

Kwa hivyo, tunaweza kujumlisha mafundisho ya mistari hii yote kwa kusema hivi: Yohana anasema, "Ninawaandikia kwa sababu ninyi ni wafuasi wa Mungu wa ukweli, lakini miongoni mwenu kuna wale ambao ni wadanganyifu, na ninataka mwe na hakikisho la nguvu sana kwamba kweli ninyi mko na uzima wa milele kwa sababu mmezaliwa mara ya pili na ninyi ni watoto wa Mungu, na kwa hivyo msiweze kuongozwa na dhambi. Na ikiwa kitabu hiki kinaweza kuwapatia hakiksho hili, basi furaha yangu itakuwa kamili." Kwa hivyo, Yohana aliandika kitabu hiki ili aweze kusaidia wakristo kujua kwamba wao wamezaliwa mara ya pili - yaani wao sasa wako na uzima upya wa milele.

### Ishara kumi na moja ambazo tutapata katika wale ambao wamezaliwa mara ya pili.

Katika kitabu cha 1 Yohana, Yohana anatupatia ishara kumi na moja ambazo zinapatikana katika mtu ambaye amezaliwa mara ya pili. Hizi ishara kumi na moja zote zinahusu imani na upendo. Sasa, ninataka kuangalia hizi ishara kumi na moja kama tu vile Yohana anazifundisha.

***1. Wale ambao wamezaliwa mara ya pili hutii amri za Mungu.***

"Basi katika hili twajua ya kuwa tumemjua kama tunazishika amri Zake. Mtu ye yote asemaye kuwa, 'Ninamjua' lakini hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala ndani ya mtu huyo hamna kweli" (1 Yohana 2:3-4).

“Hakikisheni kwamba lile mlilosikia tangu mwanzo linakaa ndani yenu. Kama lile mlilosikia tangu mwanzo linakaa ndani yenu, ninyi mtakaa ndani ya Mwana na ndani ya Baba” (1 Yohana 3:24).

***2. Wale ambao wamezaliwa na Mungu wanatembea kama vile Kristo alitembea.***

“Lakini kama mtu ye yote analitii Neno Lake, upendo wa Mungu umekamilika ndani yake kweli. Katika hili twajua kuwa tumo ndani yake. Ye yote anayesema anakaa ndani Yake hana budi kuenenda kama Yesu alivyoenenda” (1 Yohana 2:5-6).

***3. Wale ambao wamezaliwa na Mungu hawachukii wengine bali wanawapenda.***

> “Ye yote anayesema yumo nuruni lakini anamchukia ndugu yake bado yuko gizani” (1 Yohana 2:9).
>
> “Sisi tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda ndugu. Kila asiyempenda ndugu yake akaa mautini” (1 Yohana 3:14).
>
> “Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu naye anamjua Mungu. Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo” (1 Yohana 3:7-8).
>
> “Ikiwa mtu atasema, ‘Nampenda Mungu’, lakini anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo” (1 Yohana 4:20).

***4. Wale ambao wamezaliwa mara ya pili hawapendi dunia.***

> “Kama mtu ye yote akiupenda ulimwengu, kumpenda Baba kakumo ndani yake” (1 Yohana 2:15).

5. ***Wale ambao wamezaliwa na Mungu hukiri Mwana wa Mungu na kumpokea.***

"Hakuna ye yote amkanaye Mwana aliye na Baba. Ye yote anayemkubali Mwana anaye na Baba pia" (1 Yohana 2:23).

"Kila akiriye kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu hukaa ndani yake, naye ndani ya Mungu" (1 Yohana 4:15).

"Aliye naye Mwana anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima" (1 Yohana 5:12).

6. ***Wale ambao wamezaliwa na Mungu hutenda haki.***

"Kama mkijua kuwa Yeye ni mwenye haki, mwajua kwamba kila atendaye haki amezaliwa na Yeye" (1 Yohana 2:29).

7. ***Wale ambao wamezaliwa na Mungu hawana tabia ya dhambi.***

"Kila mtu akaaye ndani yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi hakumwona Yeye wala hakumtambua" (1 Yohana 3:6).

"Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu. Kwa jinsi hii tunaweza kujua dhahiri watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi nao. Ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake" (1 Yohana 3:9-10).

"Tunajua ya kuwa yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, bali aliyezaliwa na Mungu hujilinda wala yule mwovu hawezi kumdhuru" (1 Yohana 5:18).

***8. Wale ambao wamezaliwa na Mungu wanaye Roho Mtakatifu.***

"Wale wote wanaozishika amri Zake hukaa ndani Yake na Yeye ndani yao. Hivi ndivyo tunavyojua kwamba anakaa ndani yetu. Nasi twajua hili kwa njia ya Roho yule aliyetupatia" (1 Yohana 3:24).

"Tunajua kwamba twakaa ndani Yake na Yeye ndani yetu, kwa sababu ametupatia sisi sehemu ya Roho Wake" (1 Yohana 4:13).

***9. Wale ambao wamezaliwa na Mungu wanasikia na kupokea na kutii neno laMungu.***

"Sisi twatokana na Mungu na ye yote anayemjua Mungu hutusikiliza, lakini asiyetokana na Mungu hatusikilizi. Hivi ndivyo tunavyoweza kutambua Roho wa Kweli na roho ya upotovu" (1 Yohana 4:6).

***10. Wale ambao wamezaliwa na Mungu wanaamini kwamba Yesu ndiye Kristo.***

"Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu" (1 Yohana 5:1).

***11. Wale ambao wamezaliwa na Mungu hushinda ulimwengu.***

"Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4).

**Hali ya kiroho ya wale ambao wamezaliwa mara ya pili.**

Wakati watu wengi wanasoma haya mafundisho ya Yohana, wengi wao wanaanguka katika makosa ya mawazo ya aina fulani.

Kuna wale ambao wanawaza kwamba Yohana anasema yule ambaye amezaliwa mara ya pili sasa anaishi maisha bila dhambi yoyote na amekamilika kabisa. Wao wanawaza kwamba yule ambaye ameokoka sasa hawezi kushindwa na dhambi, bali atashinda dhambi na shetani kila mara. Kuna wale ambao wanawaza kwamba Yohana anafundisha mambo haya, lakini hii si kweli kamwe.

Halafu, kuna wale ambao wanawaza kwamba Yohana hapa anasema kwamba mtu anaweza kuokoka, na halafu kupoteza wokovu wake. Wao wanawaza kwamba Yohana hapa anafundisha kwamba mtu anaweza kufanya haya yote ambayo yeye anafundisha katika kitabu chake kwa muda, na kwa hivyo wawe wameokoka kwa ile muda, lakini wanapoanza kuacha mafundisho haya, wanapoteza wokovu wao. Hii pia si kweli kamwe, Yohana hayafundisi mambo kama haya.

Yohana alijua wakati aliandika kitabu chake kwamba watu wanaweza kukosa kufahamu vizuri ni nini anasema, na kwa hivyo katika kitabu hiki yeye anafundisha wazi kabisa kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili haimaanishi hawana dhambi, wao hawajakamilika. Pia, Yohana anafundisha wazi kabisa kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili hawezi kupoteza wokovu wake.

Katika kitabu chake, Yohana aliandika maneno haya: "Kama tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani yetu. Kama tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha toka kwenye udhalimu wote" (1 Yohana 1:8-9). Hapa Yohana anafundisha kwamba "kuenenda nuruni" (mstari wa 7), haimaanishi kuwa bila dhambi yoyote. Kuenenda nuruni kunamaanisha kwamba wakati tunaanguka dhambini, nuru ya Kristo inatuwezesha kuona kwamba tumeanguka dhambini na kwamba tumefanya makosa, na pia hii nuru inatuwezesha kukiri dhambi zetu na kupokea msamaha na kuendelea katika Kristo.

Pia, Yohana anatufundisha katika kitabu chake kwamba mtu hawezi kuzaliwa mara ya pili na halafu kupoteza wokovu wake. Katika kitabu hiki, Yohana anafundisha wazi ni kwa nini kuna wale ambao wanadai wameokoka, lakini baada ya muda wanaacha dini ya ukristo kabisa na kurudi dhambini. Anasema, "Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu hasa. Kwa maana kama wangelikuwa wa kwetu, wangekaa pamoja nasi, lakini kutoka kwao kulionyesha kwamba hakuna hata mmoja wao aliyekuwa wa kwetu" (1 Yohana 2:19).

Katika mstari huu Yohana anafundisha mambo matatu.

1. Kwanza, anasema kwamba wale ambao walidai wameokoka, lakini baada ya muda wanaacha kabisa njia ya ukristo hawakuwa wale ambao wameokoka kutoka mwanzo: "Walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu hasa." Yaani, wao wamerudi dhambini si kwa sababu wamepoteza wokovu wao, bali kwa sababu hawakuwa wameokoka kutoka mwanzo.

2. Pili, wale ambao wameokoka kwa kweli hawataacha njia ya Kristo. Yohana anasema, "kama wangelikuwa wa kwetu, wangekaa pamoja nasi." Yule ambaye amezaliwa mara ya pili atavumilia katika dini ya ukristo ikiwa kweli amezaliwa mara ya pili. Hili ndilo hakikisho kwamba yeye kweli amezaliwa mara ya pili.

3. Mungu anafunua wazi ni nani amezaliwa mara ya pili na ni nani hajazaliwa mara ya pili, kwa sababu wale ambao hawajazaliwa mara ya pili baada ya muda wataacha dini ya ukristo. Yohana anasema, "lakini kutoka kwao kulionyesha kwamba hakuna hata mmoja wao aliyekuwa wa kwetu." Yaani, Yohana anamaanisha kwamba wale ambao hawakuwa wamezaliwa mara ya pili, baada ya muda, waliacha njia ya Kristo. Hii ni kuonyesha kwamba hawakuwa wamezaliwa mara ya pili.

Kumbuka kwamba ishara moja ya wale ambao kweli wamezaliwa mara ya pili ni kwamba wao wanasikia na kupokea neno la Mungu (1 Yohana 4:6). Wao wanapenda sana mafundisho ya neno la Mungu na wanayashika na nguvu zao zote: "ye yote anayemjua Mungu hutusikiliza, lakini asiyetokana na Mungu hatusikilizi." Wale ambao hawajazaliwa mara ya pili watasikia neno la Mungu kwa muda kidogo. Pengine wao watasema kwamba wamepokea neno la Mungu kwa furaha (Luka 8:13), na kuonekana kwamba wao kweli wamezaliwa mara ya pili. Lakini wakati majaribu yanakuja na udanganyifu wa utajiri wa ulimwengu unakuja, wao wanaacha maisha ya ukristo na kurudi dhambini. Hii inaonyesha kwamba wao hawakuwa wamezaliwa mara ya pili kamwe.

**Mafundisho ya 1 Yohana 5:3-4.**

Katika kifungu hiki, Yohana anaandika, "Kwa kuwa huu ndio upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito. Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:3-4).

Katika kifungu hiki Yohana anafundisha mambo matatu ambayo yanashikana.

1. Jambo la kwanza ambalo anatufundisa ni hili: "Kwa kuwa huu ndio upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito." Yaani, Yohana hapa anatufundisha kwamba yule ambaye anampenda Mungu ataonyesha upendo wake kwa Mungu kwa kuzitii amri zake, na kwake kuzitii amri hizi si nzito. Ishara kwamba mtu amezaliwa mara ya pili ni kwamba yeye anampenda Mungu. Na ishara kwamba yeye anampenda Mungu ni kwamba yeye atazitii amri za Mungu kwa furaha na bila kulalamika.

2. Jambo la pili ambalo anatufundisha ni hili: "Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu." Yule ambaye amezaliwa mara ya pili atazitii amri zote za Mungu kwa furaha kwa sababu yeye sasa anayo nguvu na uwezo wa kuushinda ulimwengu. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili anamtumikia Mungu bila kulazimishwa na kwa furaha kwa sababu yeye sasa hana upendo wa dunia moyoni mwake. Yeye sasa anapenda sana Mungu kwa sababu yeye sasa amezaliwa mara ya pili. Upendo wa dunia sasa unaanza kuondoka moyoni mwake. Sheria ya Mungu sasa si nzito kwake.

3. Jambo la tatu ambalo Yohana anafundisha ni hili: "Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu." Je, ni namna gani mtu anaweza kuacha upendo wake wa dunia na kupenda sana sasa mambo ya Ufalme wa Mungu? Ni kwa sababu ya imani; yule ambaye amezaliwa mara ya pili anayo imani na ni imani yake ambayo inashinda upendo wa ulimwengu.

Kwa hivyo mafundisho ya Yohana katika kifungu hiki cha 1 Yohana 5:3-4 ni haya: wakati neno la Mungu linakuja kwetu kupitia kwa ujumbe wa injili na tunalipokea, tunazaliwa mara ya pili. Matokeo ya kwanza ya kuzaliwa mara ya pili ni kwamba tunamwona Mungu kama Yeye alivyo na kumpokea na pia kumpokea Mwana wake na kazi yake na mapenzi yake, kwa sababu tumeona thamani ya Mungu na kazi zake. Hii ni imani. Imani inashinda ulimwengu, yaani inashinda upendo na utumwa wa ulimwengu ndani ya mioyo yetu.

Kwa hivyo imani inatuongoza katika kutii neno la Mungu kwa furaha na bila kulazimishwa. Sisi sasa tunapenda Mungu na mapenzi Yake, sasa mapenzi Yake si mazito kwetu. Kwa sababu sisi tumezaliwa mara ya pili, sisi sasa si vipofu, sisi sasa tunaona kila kitu kama vile kilivyo, na tuko na uhuru ya kumtii Mungu kwa furaha.

Ninaomba kwamba Mungu atahakikisha kuzaliwa mara ya pili kwako na kwamba wewe utaishinda dunia. “Kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu.”

# Kuzaliwa mara ya pili, imani na upendo

Katika sura hii tunaangalia tena mafundisho ya Biblia katika 1 Yohana 5:1-5. Katika sura hii ninataka kukufundisha kwamba wakati tunawapenda wengine, hata kama upendo wetu si kamili, katika Kristo na haki yake kazi zetu zote zimekamilika. Yaani ninataka kukufundisha kwamba njia ya kuwa na furaha katika ushirika wako na Yesu Kristo ni njia ya imani. Kwa hivyo jambo la kwanza ambalo tunahitaji ni imani, na imani ni mizizi ya upendo. Bila imani hatuwezi kuwa na upendo.

Yule ambaye anajaribu kuwapenda wanadamu bila imani ndani ya Yesu Kristo atashindwa, hataweza kuvumilia.

Katika sura hii ninataka kuangalia ni namna gani kuzaliwa mara ya pili na imani na kuwapenda wengine, jinsi mambo haya yanashikana pamoja. Ninataka kukufundisha jambo hili kutoka kwa Biblia si kwa mawazo yangu.

**Hatua ya kwanza: Kuwapenda wengine.**

Katika mstari wa 3 wa kifungu hiki, Yohana anasema, "Kwa kuwa huu ndiyo upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito" (1 Yohana 5:3). Biblia hapa inatufundisha kwamba wale ambao wanapenda Mungu watatii amri Zake. Pia Biblia hapa inatufundisha kwamba kwa wale ambao wanampenda Mungu, amri Zake si nzito, bali ni zile ambazo wao wanapenda kufanya. Ikiwa mtu anapenda sana kufanya jambo fulani, basi lile jambo si nzito kwake, ni jambo la furaha. Wale ambao wamezaliwa mara ya pili, amri za Mungu si nzito, bali wao wanafurahia kuzitii. Katika kitabu cha Zaburi tunalisoma jambo hili wazi.

> "Ee Mungu wangu, natamani kufanya mapenzi yako, sheria yako iko ndani ya moyo wangu" (Zaburi 40:8).
>
> "Shuhuda zako ni furaha yangu, nazo ni washauri wangu" (Zaburi 119:24).
>
> "Niongoze kwenye njia ya amri zako, kwa kuwa huko napata furaha" (Zaburi 119:35).
>
> "Kama nisingekuwa nafurahia sheria yako, ningekuwa nimeangamia katika taabu zangu" (Zaburi 119:92).

Mistari hii yote inatufundisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anampenda Mungu sana na kumthamini, na kwa hivyo kuzitii sheria zake si nzito, bali ni jambo la furaha.

Pia, wakati tunasoma haya maneno ambayo Yohana ameandika, ni wazi kwamba sheria ambayo wale ambao wamezaliwa mara ya pili watafuata sana ni kuwapenda ndugu zao. Yohana anaandika, "Ikiwa mtu atasema, 'Nampenda Mungu,' lakini anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo. Kwa maana kila mtu asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, atampendaje Mungu ambaye hajamwona? Naye ametupa amri hii; Ye yote anayempenda Mungu lazima pia ampende ndugu yake" (1 Yohana 4:20). Kwa hivyo Yohana hapa anasema kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili atatii amri za Mungu kwa furaha, na amri kuu ambayo atatii na moyo wake wote ni ile amri ya kuwapenda wengine, hasa, wakristo wengine.

Hili ni jambo ambalo Yohana anafundisha tena wakati anasema, "Kila mtu anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu na ye yote ampendaye Baba humpenda pia mtoto aliyezaliwa naye" (1 Yohana 5:1). Tena katika mstari huu tunaona kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili atampenda Mungu, na ishara kwamba yeye anampenda Mungu ni kwamba yeye

atawapenda watu wa Mungu. Halafu Yohana anaendelea kuandika, "Hivi ndivyo tunavyojua kwamba tunawapenda watoto wa Mungu, kwa kumpenda Mungu na kuzitii amri Zake." Yaani Yohana hapa anafundisha kwamba ikiwa mtu anataka kuwapenda wanadamu wengine kwa ukweli, yeye kwanza anahitaji kumpenda Mungu, na halafu kuwapenda wanadamu. Kuna watu ambao hawaamini Mungu, wao si watu wa dini na watu wa kanisa, lakini wao wanadai kwamba wanapenda wanadamu. Lakini huu si upendo wa kweli. Upendo wa kweli unaanza na upendo kwa Mungu na halafu upendo kwa wanadamu wengine, hasa watu wa Mungu.

Ikiwa wewe hupendi Mungu, basi wewe kwa ukweli huwezi kuwafanyia wengine mema. Unaweza kuwalisha wengine na kuwanunulia nguo na kuwapatia nyumba na kuwasaidia katika mambo haya yote ya dunia. Lakini huwezi kuwasaidia katika mambo ya milele kwa sababu wewe mwenyewe huna maisha ya milele. Upendo wa kweli ni ule upendo ambao unampenda Mungu kwanza, na kwa sababu unampenda Mungu kwanza, unawapenda watu wa Mungu. Upendo kwa Mungu unakuja kwanza.

Kwa hivyo tumeona kwamba wakati Yohana anasema, "Kwa kuwa huu ndiyo upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito" (Yohana 5:3), anamaanisha kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili watampenda Mungu na kwa hivyo watawapenda watu wa Mungu. Mafundisho ya mstari huu ni haya: huu ni upendo wa Mungu, kwamba tunawapenda wengine, hasa watoto wake, na maisha haya ya kuwapenda watoto wa Mungu si maisha mazito, kwa sababu haya ni maisha ambayo tunayapenda sana kuishi kwa sababu tunampenda Baba wetu ambaye ni Mungu.

**Hatua ya pili: Kuzaliwa mara ya pili.**

Katika sehemu hii ya sura hii tunajifunza 1 Yohana 5:3-4 ambayo inasema, "Kwa kuwa huu ndiyo upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito. Kwa maana kila

aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu." Tayari tumeona hapa juu kwamba hatua ya kwanza katika mistari hii ni upendo wa Mungu: "Huu ndiyo upendo wa Mungu, kwamba tuzitii amri Zake. Nazo amri Zake si nzito." Sasa tunaendelea kuangalia hatua ya pili: "Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu."

Hapa Yohana anafundisha ni kwa nini kumpenda Mungu na kuwapenda watu wake si mambo mazito kwa wale ambao wamezaliwa mara ya pili. Mambo haya ya kumpenda Mungu na kuzitii amri Zake siyo mazito kwa sababu yule ambaye amezaliwa mara ya pili ameshinda ulimwengu. Tunaweza kumpenda Mungu na kuwapenda wengine kwa sababu Mungu ametuwezesha kuushinda ulimwengu. Ulimwengu huu unajaribu kutuzuia kumpenda Mungu. Vitu vya dunia vinavuta watu wa Mungu, na wengi wanajaribiwa kufuata vitu vya dunia kama fedha. Kuna wengi ambao bado wako na upendo kwa vitu vya dunia mioyoni mwao na wanavutwa sana na anasa za dunia. Hii ndiyo njia ulimwengu unajaribu kutumia kuwazuia watu wa Mungu wasimwabudu Mungu.

Yohana anafundisha wazi kuhusu ulimwengu na hatari yake katika mistari hii: "Msiupende ulimwengu wala mambo yaliyoko ulimwenguni. Kama mtu ye yote akiupenda ulimwengu, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Kwa maana kila kitu kilichomo ulimwenguni, yaani, tamaa ya mwili, tamaa za macho na kiburi cha uzima, havitokani na Baba bali hutokana na ulimwengu. Nao ulimwengu unapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu milele" (1 Yohana 2:15-17).

Hapa tunaona mambo ya dunia ambayo tunahitaji kuyashinda: "tamaa ya mwili, tamaa za macho na kiburi cha uzima." Kwa ufupi tunaweza kusema hatari ya dunia ni tamaa za vile vitu

ambavyo tunapenda sana kuwa navyo, na kiburi cha vile vitu ambavyo tuko navyo.  Wakati hatuna vile vitu ambavyo tunapenda sana kuwa navyo, ulimwengu unaweka tamaa ndani yetu; na wakati tuko na vile vitu ambavyo tunapenda sana, ulimwengu unaweka kiburi ndani yetu.

Hii ndiyo sababu wengi hawampendi na hawamtumikii Mungu, ni kwa sababu ya upendo wa vitu vya dunia.  Sisi wanadamu hupenda vitu vya dunia kwa mioyo yetu yote.  Wakati hatuna kitu fulani ambacho tunataka, tunakitafuta kwa mioyo yetu yote, na halafu baada ya kukipata, tunaongea kukihusu kila wakati kwa sababu sasa tuko na kiburi.  Kwa kufanya haya yote, tunamsahau Mungu kabisa.  Hata kama tunamshukuru Mungu kwa vile vitu ambavyo tuko navyo, shukrani hizi  hazikutoka kwa mioyo yetu, bali ni kwa sababu tunataka Mungu atupatie vitu vingine vingi.

Hii ndiyo sababu wengi hawampendi Mungu na wanapata kuwapenda wengine kuwa jambo nzito sana.  Ni kwa sababu mioyo yao inapenda ulimwengu na vitu vyake.  Hivi vitu vya dunia vinaweza kuwa vitu vizuri kama elimu au vitu vibaya kama pombe; lakini ikiwa vitu hivi tunavitamani sana na tunavifuata kabisa kwa mioyo yetu yote, basi hivi vitu kwetu vimekuwa sanamu na vimechukua nafasi ya Mungu mioyoni mwetu.  Hii ndiyo taabu watu wote wa dunia wako nayo: sisi sote tunapenda vitu vya dunia na tunavifuata kwa mioyo yetu yote.

Lakini yule ambaye amezaliwa mara ya pili ameshinda ulimwengu.  Yohana anasema, “Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu.  Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu” (1 Yohana 5:3). Tunaweza kufahamu ni nini Yohana anatufundisha hapa. Anamaanisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili upendo wa vitu vya dunia na tamaa za vitu hivi vimeanza kuondolewa.  Mizizi ya tamaa za vitu vya dunia sasa imeanza kun’golewa.

### 3. Hatua ya tatu, imani katika Kristo.

Jambo la tatu ambalo Yohana anatufundisha katika kifungu hiki ni namna gani huu upendo wa dunia unaanza kung'olewa. Yohana anasema, "Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:3). Wakati mtu anazaliwa mara ya pili, yeye sasa ana imani na hii ndiyo njia anashinda ulimwengu na tamaa za vitu vya ulimwengu.

Wakati mtu anazaliwa mara ya pili, yeye anapata fahamu kwamba Yesu Kristo ni wa thamani kuliko vitu vyote vya dunia (2 Wakorintho 2:4,6). Hii ndiyo sababu yule ambaye amezaliwa mara ya pili anampokea Yesu Kristo kuwa mwokozi wake. Ni kwa sababu yeye alizaliwa mara ya pili, macho yake yamefunguliwa na yeye sasa anafahamu vizuri thamani ya Kristo na ya Ufalme wa Mungu. Hii ndiyo imani: kumpokea Kristo kwa sababu macho yetu yamefunguliwa na sisi tumeona kwamba Yeye ni mwenye uzuri wote.

Hii ndiyo sababu imani inaushinda ulimwengu. Kabla ya mtu kuokoka yeye alikuwa akiwaza kwamba vitu vya dunia ni vya thamani sana. Lakini sasa macho yake yamefunguliwa kwa sababu yeye amezaliwa mara ya pili na yeye ameona kwamba vitu vya dunia havina thamani ya milele, bali Kristo ndiye yule ambaye ana thamani. Thamani ya Yesu ni kuu kuliko tamaa za mwili na kuliko utajiri wa dunia ambao hutuletea kiburi na tamaa.

## Mpango ya Mungu: Kuzaliwa mara ya pili, imani na upendo

Sasa tunaweza kuona kuzaliwa mara ya pili na imani na upendo yanahusiana namna gani.

Kwanza, tunaweza kusema kwamba mtu ambaye amezaliwa mara ya pili ana imani. Hii tunasoma katika Biblia, "Kila mtu

anayeamini kwamba Yesu ndiye Kristo amezaliwa na Mungu" (1 Yohana 5:1). Wakati tunazaliwa mara ya pili na Mungu, tunakuwa na imani. Yule ambaye anamwamini Mungu anashuhudia kwamba yeye amezaliwa mara ya pili.

Pili, tunaweza kusema kwamba yule ambaye anayo imani atazaa matunda ambayo ni upendo kwa watu wa dunia. Hili ndilo jambo ambalo Yohana anafundisha hapa: "Huku ndiko kuushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu" (1 Yohana 5:4). Yohana hapa anasema kwamba imani inashinda ulimwengu, yaani inashinda upendo wa ulimwengu. Kwa hivyo yule ambaye amezaliwa mara ya pili sasa hana upendo wa ulimwengu moyoni mwake bali anao upendo wa watu kwa ulimwengu.

Kwa hivyo, haya mambo yanafanyika katika mpango huu:

1. Mtu anazaliwa mara ya pili.
2. Anakuwa na imani ndani ya Kristo.
3. Anatii sheria za Mungu na hii sheria si nzito kwake sasa, bali anawapenda wengine kwa furaha.

Ni Mungu ambaye anafanya mtu azaliwe mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kuwa na maisha ambayo yanaona thamani na uzuri wa Kristo Yesu, na kumpokea Kristo. Wakati mtu anampokea Kristo, mizizi ya upendo wa ulimwengu inakatwa na yeye sasa ana huru kumpenda Mungu na kuwapenda watu wake.

Ni lazima tufahamu kwamba imani na upendo ni mambo mawili tofauti. Mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili anaweza kuwa na upendo kwa watu wengi na anaweza kuwasaidia wengi, lakini hii haimaanishi kwamba yeye anayo imani ya kweli, na kwamba yeye ameokoka. Ikiwa yeye hajazaliwa mara ya pili, basi yeye hajaokoka, ingawa anawapenda watu wa dunia.

**Uhusiano kati ya imani na matendo.**

Wakristo wengi wamechanganyikiwa kuhusu uhusiano kati ya imani na matendo. Kuna mambo mawili ambayo tunahitaji kukumbuka kuhusu haya mambo mawili: moja, imani na matendo yetu katika maisha ya ukristo ni mambo tofauti. Yaani imani si matendo na matendo si imani. Pili, imani ya ukweli inazaa matendo mema katika maisha ya mkristo.

Haya ni mambo ambayo ni lazima tuyafahamu kwa sababu kuna wengi ambao wakati wanaanguka dhambini wanawaza kwamba wamepoteza wokovu wao. Wanawaza kwamba wao wameokoka kwa sababu wanatenda mambo mazuri maishani mwao. Lakini hii si kweli.

Biblia inatuambia kwamba sisi tunaokoka kupitia kwa imani, na imani hii inazaa matunda mema. Katika maisha ya ukristo kwa kawaida kuna wakati ambapo tunaanguka dhambini au tunakosa kufanya juhudi zetu ambazo Mungu ametupatia. Wakati huo, tunahitaji kukumbuka kwamba Yesu Kristo ni mkombozi wetu. Biblia inasema, “Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mkombozi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki” (1 Yohana 2:1). Hapa Yohana anasema kwamba ule wakati tunakosa kutii Mungu na kuanguka dhambini, Yesu Kristo ni Mkombozi wetu ambaye ni Mwenye haki. Wakati Yohana anasema kwamba Kristo ni Mwenye haki anamaanisha kwamba Kristo ni bila dhambi yoyote.

Biblia inatufundisha kwamba kwa sababu Yesu Kristo ni mwenye haki na bila dhambi yoyote, Yeye amechukua nafasi yetu. Yaani Yeye aliishi maisha matakatifu na bila dhambi yoyote badala ya watu wake. Hata kama sisi tumekosa kumtumikia Mungu kama vile tunavyohitajika kumtumikia, Yeye hajakosa, lakini alimtumikia Mungu kamili. Na Yeye ni mkombozi wetu ambaye

anasimama pamoja nasi, si kinyume nasi. Hii nidyo sababu Yohana anasema, “Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mkombozi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki” (1 Yohana 2:1).

Hii ndiyo sababu tunahitaji kukumbuka kwamba hakuna yeyote ambaye anaweza kuokoka kupitia kwa matendo yake mema, bali kupitia kwa imani. Tunaokoka si kwa sababu tumetii neno la Mungu kamili, bali ni kwa sababu Kristo ametii neno la Mungu kamili, na tunamwamini. Kupitia kwa imani tunapokea kazi yake Yesu Kristo ambaye alifanya kwa ajili yetu. Yeye ndiye haki yetu na ukamilifu wetu na matendo yetu mema. Ni kwa sababu hii tunalo tumaini mbele ye Mungu, ni kwa sababu Yesu Kristo ni Mkombozi wetu.

Kwa hivyo tunapaswa kukumbuka kwamba yule ambaye ameokoka, ameokoka kwa sababu ya imani ndani ya Yesu Kristo na imani hii inazaa matendo mema. Hii ndiyo sababu wale ambao wameokoka wanawapenda wengine. Kuwapenda wengine kunamaanisha kuwasaidia wengine kwa mioyo yetu yote. Hii tunaweza kufanya, hata kama tunafanya makosa katika upendo wetu, kwa sababu Yesu Kristo ndiye ukamilifu wetu. Yule ambaye anampokea Kristo ana imani ndani yake, na imani hii ndiyo msingi wa wokovu wetu na tumaini letu.

Sisi tunaokoka si kwa sababu ya matendo yetu mema au haki yetu, bali kwa sababu ya kutii kwake Kristo na haki yake; tunaokoka kwa sababu ya ukamilifu wake na upendo wake kwa ajili yetu mbele za Mungu Baba.

Hii ndiyo sababu yule ambaye ameokoka anaweza kuwa na tumaini hata ule wakati ameanguka dhambini. Yeye hawezi kuupoteza wokovu wake na halafu kupata wokovu tena na halafu kuupoteza tena wakati ameanguka dhambini. Yeye hajaokoka kwa sababu ya matendo yake mema na kwa sababu ya haki yake, bali

kwa sababu ya haki ya Yesu Kristo. Yesu Kristo, ambaye ni Mwombezi wetu anamwomba Baba kwa ajili ya watu wake kwa njia hii: "Mungu Baba, kwa ajili Yangu mhesabie baraka huyu ambaye hastahili. Kwa ajili ya upendo wangu kamili, mhesabie kuwa mwenye upendo kamili hata kama upendo wake ni mdhaifu. Wewe unajua kila kitu ee Baba (1 Yohana 3:20). Ee Baba, wewe unajua kwamba moyoni mwake yeye ananiamani. Kwa hivyo Mimi ni wake na upendo wangu kamili uhesabie kuwa wake."

**Yesu Kristo Mwombezi wetu.**

Wakati Mungu anamwangalia yule ambaye ameokoka, anamwangalia akiwa katika Kristo. Hii ndiyo sabab yule ambaye ameokoka hahitaji kuwa na huzuni. Yeye si mtu ambaye hana tumaini. Yeye hukiri dhambi zake na makosa yake yote (1 Yohana 1:9). Yeye anapokea msamaha ambao Kristo analeta. Yeye anamwamini Kristo ambaye aliondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu yake (1 Yohana 3:19). Hii nidyo sababu yeye analo hakikisho moyoni mwake kwamba Mungu anamwangalia akiwa katika Mwombezi wake.

Kwa hivyo, kwa ufupi, katika sura hii nimekufundisha kwamba hata wewe ukifanya makosa mengi, hii haimaanishi kwamba umepoteza wokovu wako, kwa sababu katika Kristo, sisi tumekamilika mbele za Mungu. Yeye aliwapenda watu wa ulimwengu kikamilifu, na kwa hivyo wakati tunawapenda watu wengine, huu ni upendo kamili kwa sababu sisi tuko ndani ya Kristo kupitia kwa imani. Tumeokoka kupitia kwa imani ndani ya Kristo na kwa hivyo tuko na hakikisho kwamba tumeokoka milele. Hii ndiyo sababu tunaweza kutenda matendo mema.

*"Oneni ni pendo kuu namna gani alilotupa Baba, kwamba sisi tuitwe watoto wa Mungu. Nasi ndivyo tulivyo. Sababu kwa nini ulimwengu haututambui, ni kwa kuwa haukumtambua Yeye. Wapenzi, sasa tu watoto wa Mungu, lakini bado haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua ya kwamba, Yeye atakayepodhihirishwa, tutafanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. Kila mmoja mwenye matumaini haya katika Yeye hujitakasa, kama vile Yeye alivyo mtakatifu.*

*Kila mtu atendaye dhambi afanya uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. Lakini mwajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala ndani Yake hamna dhambi. Kila mtu akaaye ndani Yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi hakumwona Yeye wala hakumtambua.*

*Watoto wadogo, mtu ye yote na asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki. Yeye atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa sababu Ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa ili aziangamize kazi ya Ibilisi. Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu. Kwa jinsi hii tunaweza kujua dhahiri watoto wa Mungu na watoto wa Ibilisi nao. Ye yote asiyetenda haki hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu yake".*

1 Yohana 3:1-10

# Uhuru kutoka kwa tabia ya dhambi

Katika sura hii tutauliza na kujibu swali hili: "Je, ni namna gani wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanashughulikia dhambi zao na ni namna gani wanaweza kuwa na hakikisho kwamba wao kweli wamokoka?"

Yaani, katika sura hii, tutaona kwamba mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili na bado awe na dhambi maishani mwake. Je, ni namna gani mtu anaweza kuwa na hakikisho kwamba yeye ataokoka milele ingawa anaanguka dhambini? Je, ni namna gani mtu anaweza kuhakiksha kwamba ataendelea kupigana vita na dhambi na hatasema tu, "Nimeokoka milele" na kwa hivyo kupumzika tu?

Majibu ya maswali haya yote yanapatikana katika kitabu cha 1 Yohana. Kwa mfano, katika kitabu hiki tunasoma maneno haya, "Nawaandikia mambo haya ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu ili mpate kujua ya kuwa mnao uzima wa milele" (1 Yohana 5:13). Hapa, Yohana anasema kwamba ameandika kitabu chake ili wale ambao wameokoka waweze kuwa na hakiksho kwamba wao kweli wameokoka, yaani wao sasa wako na maisha mapya ndani mwao ambayo hayataangamizwa. Mungu anataka kwamba wakati tunasoma kitabu hiki cha 1 Yohana, tuwe na hakikisho bila shaka yoyote kwamba tumeondolewa kutoka kwa kifo cha kiroho na tumepata maisha ya kiroho.

Yohana anasema, "Sisi tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini na kuingia uzimani" (1 Yohana 3:14). Yesu Kristo alisema, "Amin, amin, ninawaambia, ye yote anayesikia maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenituma anao uzima wa milele, naye hatahukumiwa, bali amepita kutoka mautini, na kuingia uzimani" (Yohana 5:24). Yesu Kristo na Yohana wote wawili

wanafundisha hapa kwamba yule ambaye ameokoka hatahukumiwa siku ya hukumu kwa sababu Yesu Kristo alihukumiwa badala yake. Wanataka kuwafundisha wale ambao wamezaliwa mara ya pili kwamba wao hawatahukumiwa kifo kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili yao. Wanataka kuwafundisha wale ambao wamezaliwa mara ya pili kwamba wao wako na maisha ndani mwao, na kwamba maisha haya hayataangamizwa na hayatachukuliwa kutoka kwao na yeyote. Maisha haya ambayo wamepewa ni maisha ya milele. Hili ni hakikisho ambalo Kristo na Yohana wanataka tuwe nalo: "Nawaandikia mambo haya ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu ili mpate kujua ya kuwa mnao uzima wa milele" (1 Yohana 5:13).

**Ni nini walimu wa uongo walifundisha.**

Wakati Yohana aliandika kitabu hiki cha 1 Yohana, kuna mambo fulani ambayo yalikuwa yakitendeka katika makanisa, na mambo haya yalimsumbua sana. Kulikuwa na walimu wa uongo ambao walileta mafundisho ya uongo katika makanisa haya. Mafundisho yao yalikuwa haya:

1. Kwanza, hawa walimu wa uongo walisema kwamba Yesu Kristo hakuja hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu kamili. Wao hawakuamini kwamba Yesu Kristo alikuwa mwanadamu kamili na Mungu kamili katika utu moja. Yohana alisema haya kuwahusu watu hawa: "Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho mwone kama zimetoka kwa Mungu, kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea ulimwenguni. Hivi ndivyo mnavyoweza kutambua Roho wa Mungu: Kila roho inayokubali kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatoka kwa Mungu. Lakini kila roho ambayo haimkubali Yesu haitoki kwa Mungu. Hii ndiyo roho ya mpinga Kristo, ambayo mmesikia kwamba inakuja na sasa tayari iko ulimwenguni" (1 Yohana 4:1-3).

Hawa walimu wa uongo walitenganisha Kristo na mwili wake, yaani wao walifundisha kwamba Kristo hakuwa na mwili kamili wakati alikuja hapa ulimwenguni. Hii tunaona katika mstari wa 2 wa kifungu hiki ambapo Yohana anasema, "Hivi ndivyo mnavyoweza kutambua Roho wa Mungu: Kila roho inayokubali kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatoka kwa Mungu." Walimu wa uongo hawakupenda mafundisho ambayo yalisema kwamba Yesu Kristo alikuwa Mungu kamili na pia alikuwa mwanadamu kamili.

Je, ni kwa nini tunahitaji kuelewa vizuri mafundisho ya hawa walimu wa uongo? Ni kwa sababu wao walitenganisha Kristo na mwili wake, na pia wao walitenganisha mkristo na maisha yake ya kila siku.

Hii ndiyo sababu Yohana anaandika, "Watoto wangu, mtu ye yote asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki" (1 Yohana 3:7). Yohana hapa anaongea kuhusu walimu wa uongo: "Mtu ye yote asiwadanganye." Anasema hapa kwamba kuna wale ambao wanafundisha kwamba mtu anaweza kuwa mkristo bila kuishi maisha ya ukristo. Yohana anasema hapa kwamba kuna wale ambao wanafundisha kwamba mtu anaweza kudai yeye ni mkristo bila kuwa mwenye haki. Hii nidyo sababu yeye anaandika hapa, "Mtu ye yote asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki."

Kwa hivyo katika kitabu hiki, Yohana anasema kwamba wale ambao wanatenganisha Kristo na mwili wake na pia wanatenganisha ukristo na maisha ya kila siku ni walimu wa uongo. Hawa walimu wa uongo walisema, "Mwili haukuwa muhimu kwa Kristo. Yale ambayo ni ya muhimu ni kwamba yeye ndiye Kristo. Yeye hakuwa mwanadamu wa kweli. Kwa hivyo miili yetu pia haina maana yoyote. Mtu anaweza kuwa mkristo na kuishi maisha ya dhambi katika mwili wake. Mtu anawezakuwa amezaliwa mara ya pili na pia aishi maisha ya dhambi mwilini mwake." Haya

yalikuwa mafundisho ya walimu wa uongo, na hii ndiyo sababu Yohana alisema, “Watoto wangu, mtu ye yote asiwadanganye. Kila mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki” (1 Yohana 3:7).

Yohana anayo mambo matatu ya kusema kuhusu mafundisho haya.

1. Kwanza, Yohana anafundisha kwamba Yesu Kristo, ambaye ni Mungu kamili pia alikuwa mwanadamu kamili. Yohana anafundisha katika kitabu hiki kwamba mtu hawezi kutenganisha Yesu Kristo, ambaye ni Mungu kamili, na mwili wake ambao ni mwili wa mwanadamu kamili. Yohana aliandkika, “Hivi ndivyo mnavyoweza kutambua Roho wa Mungu: Kila roho inayokubali kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatoka kwa Mungu” (1 Yohana 4:2). Tazama vizuri kwamba Yohana hasemi, “Yesu Kristo alikuja katika mwili,” bali anasema, “Yesu Kristo amekuja kwa mwili.” Hii inamaanisha hata leo Yesu Kristo bado ana mwili; si kwamba wakati alipaa mbinguni baada ya kufufuka aliuacha mwili wake hapa, bali alirudi mbinguni na mwili wake, na bado anao huo mwili.

Milele wale ambao wameokoka watakuwa na Yesu Kristo ambaye ni Mungu kamili na mwanadamu kamili, ambaye ni wa kwanza wa mandugu wengi (Warumi 8:29). Mungu hachukii ulimwengu ambao Yeye mwenyewe ameumba; Yeye Mwenyewe ambaye ni Mungu alikuja hapa ulimwenguni akiwa na mwili, na Yeye atakuwa na mwili milele. Kwa hivyo, kitu cha kwanza Yohana anafanya ni kuwafundisha hawa walimu wa uongo ukweli kumhusu Kristo. Yeye anasema kwamba Yesu Kristo ambaye ni Mungu alikuja hapa ulimwenguni akiwa mwanadamu kamili na akiwa na mwili kamili ya mwanadamu. Yeye sasa anayo mwili ambayo ni Yake milele.

2. Pili, Yohana anafundisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili ataishi maisha ya ukristo ulimwenguni. Yohana anasema, “Watoto wangu, mtu ye yote na asiwadanganye. Kila

mtu atendaye haki ana haki, kama Yeye alivyo na haki" (1 Yohana 3:7). Walimu wa uongo walisema mtu anaweza kuwa ameokoka, yaani anaweza kuwa mwenye haki mbele ya Mungu halafu awe anaishi maisha ya dhambi. Lakini Yohana anasema yule ambaye ameokoka, yaani ni mwenye haki mbele ya Mungu ataishi maisha ya haki kuonyesha kwamba yeye ni mwenye haki. Yohana anasema kwamba maisha ya mtu unadhihirisha hali yake ya kiroho.

Hili ni jambo ambalo Yohana anafundisha tena na tena katika kitabu hiki. Kwa mfano, katika 1 Yohana 2:29, yeye anasema, "Kama mkijua kuwa Yeye ni mwenye haki, mwajua kwamba kila atendaye haki amezaliwa na Yeye." Yaani hapa anasema kwamba yule ambaye anatenda matendo mema maishani mwake anadhihirisha kwamba yeye amezaliwa mara ya pili.

Pia katika 1 Yohana 3:9, Yohana anasema, "Ye yote anayezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa Mungu wakaa ndani yake." Yaani hapa Yohana anasema kwamba tabia ya dhambi inadhihirisha kwamba mtu hajazaliwa mara ya pili. Matendo yetu yanadhihirisha hali yetu ya kiroho. Yule ambaye haishi maisha ya dhambi anaonyesha kwamba yeye amezaliwa mara ya pili.

Pia, Yohana anatuambia ni kwa sababu gani yule ambaye kweli amezaliwa mara ya pili hataendelea na tabia ya dhambi: ni kwa sababu "uzao wa Mungu wakaa ndani yake," na kwa hivyo yeye hawezi kuendelea kutenda dhambi. Tunaona hapa kwamba hali yetu ya kiroho inahusiana na maisha yetu ya kila siku. Wakati Yohana hapa anaongea kuhusu "uzao wa Mungu," huenda anamaanisha mambo matatu: huenda anamaanisha Roho Mtakatifu au neno la Mungu au utu wa Mungu. Haya yote yanafaa hapa. Hii inamaanisha kwamba Mungu mwenyewe anafanya kazi wakati mtu anazaliwa mara ya pili, na kazi hii ya Mungu ni ya nguvu sana hadi yule ambaye amezaliwa mara ya pili hawezi

kuendelea kutenda dhambi. Mungu mwenyewe anaishi ndani ya yule ambaye amezaliwa mara ya pili na Mungu hawezi kuacha dhambi iendelee kukaa ndani ya yule mtu.

Wale walimu wa uongo ambao wanawaza kwamba mtu anaweza kuzaliwa mara ya pili na kuendelea kuishi maisha ya dhambi hawaelewi kamwe kuja kwake Yesu hapa ulimwenguni kuwa mwanadamu, na pia hawaelewi kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha nini. Wakati Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni, alikuwa mwanadamu kamili na alikuwa na mwili wa mwanadamu kamili. Na wakati mtu anazaliwa mara ya pili, kuzaliwa mara ya pili kwake kunabadilisha maisha yake ya kila siku.

3. Jambo la tatu ambalo Yohana anafundisha katika kitabu hiki ni kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili haimaanishi hawana dhambi yoyote. Hawa walimu wa uongo walifundisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili, nafsi yake sasa imekamilika kabisa na bila dhambi yoyote, kwa sababu huyu mtu amezaliwa mara ya pili. Wao walisema, "Mtu ambaye amezaliwa mara ya pili anawezaje kutenda dhambi? Yeye sasa amezaliwa mara ya pili na hawezi sasa kutenda dhambi tena. Wao sasa wamezaliwa na Mungu, wao sasa ni watu wapya, na kwa hivyo wao sasa hawawezi kutenda dhambi." Haya ndiyo yalikuwa mafundisho ya hawa walimu wa uongo.

Yohana anafundisha kuhusu jambo hili mara tatu. Hapa tutaona kila moja ya haya matatu katika kitabu chake.

(i) Kwanza, Yohana anaandika, "Kama tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe wala kweli haimo ndani yetu" (1 Yohana 1:8). Anaongea maneno haya kuhusu wale ambao wamezaliwa mara ya pili, si kuhusu wale ambao hawajazaliwa mara ya pili. Yohana hapa anasema hawa walimu wa uongo wanadai kwamba yule ambaye

amezaliwa mara ya pili hana dhambi, lakini ninyi watu wa Mungu msiseme hivyo kwa sababu huu ni uongo. Hakuna kitu kama watu ambao hawana dhambi.

(ii) Pili, Yohana anaandika, “Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki” (1 Yohana 2:1). Yohana hapa anasema, “Msiwaze kwamba ikiwa mmetenda dhambi mmepoteza wokovu wenu na ninyi hamjazaliwa mara ya pili.” Anasema kwamba wakati tunaanguka dhambini tunapaswa kukumbuka kwamba tunaye Mwombezi ambaye atatusaidia.

(iii) Tatu, Yohana anaandika, “Kama mtu akimwona ndugu yake anatenda dhambi isiyo ya mauti, inampasa aombe, naye Mungu atampa uzima mtu huyo, yaani, kwa wale ambao dhambi yao si ya mauti. Iko dhambi ya mauti, sisemi kwamba utaomba kwa ajili ya hiyo. Jambo lo lote lisilo la haki ni dhambi, lakini iko dhambi isiyo ya mauti” (1 Yohana 5:16-17). Angalia vizuri ni nini Yohana anasema hapa mwisho. Anasema, “iko dhambi isiyo ya mauti.” Hii ndiyo sababu unaweza kuona mtu ambaye amezaliwa mara ya pili akitenda dhambi. Yeye ni ndugu yako na yeye amezaliwa mara ya pili, na yeye anatenda dhambi. Je, hii inawezakanaje? Jibu ni, inawezekana kwa sababu kuna dhambi ambayo siyo ya mauti. Yohana haisemi kwamba kuna dhambi fulani ambayo ni ya mauti na kuna dhambi fulani ambayo siyo ya mauti; bali anasema kwamba kuna wale ambao dhambi imewashika sana na ina mizizi ndani ya mioyo yao. Wao wanaweza kuendelea kutenda dhambi hadi mioyo yao iwe migumu sana na wao hawataweza kutubu na kuokoka. Wao watakuwa kama Esau ambaye alitafuta kutubu lakini hakuweza kwa sababu alitenda dhambi nyingi sana na alifanya moyo wake uwe mgumu

(Waebrania 12:16-17). Aliuza urithi wake kwa bakuli ya supu na kuudharau urithi wake. Baada ya muda yeye alijaribu kutubu lakini hakuweza. Angetubu, angepata wokovu, lakini moyo wake ulikuwa mgumu sana na kwa hivyo hakuweza kutubu, kwa hivyo hata wakati alisema alitaka kutubu, hii ilikuwa uongo tu.

**Kuhusu dhambi zetu za kila siku.**

Kwa hivyo sasa tunaweza kuangalia tena yale maswali tuliuliza mwanzo wa sura hii. Tuliuliza swali hili: "Je, mtu ambaye amezaliwa mara ya pili anawezaje kuendelea kuwa na hakikisho kwamba kweli yeye ameokoka, ilahali anaanguka katika dhambi?" Jibu la swali hili ni kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anahitaji kutumia mafundisho ya Yohana katika maisha yake ya kila siku. Yohana anafundisha kwamba kuna hatari ya unafiki, yaani yule mtu ambaye anadai amezaliwa mara ya pili, lakini kwa ukweli yeye hajazaliwa mara ya pili. Pia, Yohana anasema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanahitaji kukumbuka kwa furaha kwamba Yesu Kristo ameondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu ya watu wake, na pia Yesu Kristo ni Mwombezi wa watu wake.

Je, tunatumia haya mafundisho mawili namna gani? Je, ni namna gani tunatumia onyo kwamba mtu anaweza kujidanganya? Je, ni namna gani tunaweza kutumia ahadi hii: "Kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki"? (1 Yohana 2:1). Jinsi mtu anajibu maswali haya mawili itaonyesha kama yeye kweli amezaliwa mara ya pili au la.

Kuna wale ambao hawajali kwamba wanatenda dhambi na wanazo tabia za dhambi maishani mwao. Yaani kuna wale ambao maisha yao yanaelekea njia ya dhambi na maisha yao yanaanza kuwa na tabia ya dhambi lakini wao ni kama wale ambao wanalala na hawajali mambo haya. Wao wanapenda dunia sana

na wanatenda dhambi za dunia bila kujali. Wao hawajichungi dhidi ya mawazo mabaya na matendo mabaya na wameanza tabia za dhambi.

Wakati yule ambaye amezaliwa mara ya pili anaanza kuwa hivi, Roho Mtakatifu atamwamsha kwa sababu Biblia inasema, “Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi.” Roho Mtakatifu atamwamsha huyu mtu na kumwonyesha kwamba yeye amekuwa mtu ambaye hajali na ameanza kulala katika maisha yake ya kiroho na kwa hivyo ameanza tabia za dhambi na ameanza kupenda ulimwengu na vitu vya ulimwengu. Pia, Roho Mtakatifu atamkumbusha kwamba yeye anahitaji kwenda kwake Kristo ili apate msamaha wa dhambi zake kwa sababu Kristo ni Mwombezi, na pia Kristo alikufa kwa ajili yake kuondoa ghadhabu ya dhambi zake ambazo zilikuwa juu yake. Kwa hivyo, yeye atakiri dhambi zake na ataoshwa katika damu ya Yesu Kristo (1 Yohana 1:9). Upendo wake kwa Kristo utakuwa upya na yeye sasa atapenda sana kuwa katika ushirika na Kristo na atachukia sana dhambi. Furaha ya Mungu itakuwa nguvu zake tena.

Pili, kuna wale ambao wanakufa moyo kwa sababu wanaona dhambi zao, na wanaona kwamba hawawezi kumtumikia Mungu kama vile wanavyopaswa kumtumikia. Dhamira zao zinawasumbua sana na matendo yao yanaonekana kuwa madogo sana. Wao wanawaza kwamba hawafanyi chochote kwa Ufalme wa Mungu.

Wakati mtu ako katika hali hii, anafaa kujihimiza na maneno haya ya Biblia, “Watoto wangu wapendwa, nawaandikieni haya ili msitende dhambi. Lakini kama mtu ye yote akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo Mwenye haki” (1 Yohana 2:1). Yohana hapa anatukumbusha kwamba sisi watu wa Mungu tunaye Mwombezi ambaye anaweza kutusaidia wakati tunaanguka dhambini.

**Nguvu za neno la Mungu ambazo zinawakomboa watu.**

Yule ambaye amezaliwa mara ya pili anao uwezo wa kusikia neno la Mungu na kulipokea, na pia anao uwezo wa kulitumia neno la Mungu katika maisha yake ya kila siku. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili hatakuwa mtu wa kutojali dhambi hata kama anajua kwamba yeye anaye Mwombezi. Pia, yule ambaye amezaliwa mara ya pili hatakufa moyo wakati anaanguka dhambini ingawa neno la Mungu linasema, "Ye yote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi" (1 Yohana 3:9). Yule ambaye amezaliwa mara ya pili anajua ni namna gani anaweza kutumia mafundisho ya Yohana kumsaidia katika maisha yake ya ukristo wa kila siku. Yeye ataonywa na Biblia kuhusu kutojali dhambi na kwa hivyo atajichunga sana. Pia yeye atafurahi kujua kwamba yeye anaye Mwokozi ambaye ameondoa ghadhabu ya Mungu na ambaye ni Mwombezi wake.

Ninaomba kwamba Mungu atatumia mafundisho haya kutoka kwa kitabu cha 1 Yohaana kuhakikishia kwamba wewe kweli umezaliwa mara ya pili. Ninaomba kwamba utashika onyo ambazo zinapatikana katika kitabu hiki na pia utakuwa na furaha kwa sababu ya yale ambayo tunafundishwa hapa. Ninaomba kwamba utasikia neno la Mungu kwa njia ambayo linafaa kusikizwa na kwamba utakuwa na hakikisho la wokovu wako.

# Kuwapenda wengine na upendo wa Mungu

Katika sura hii tutaona kwamba upendo wa Mungu juu yetu unatuwezesha sisi kuwapenda wengine. Mtu akiuliza, je, ni namna gani upendo wa Mungu juu ya mtu fulani unamwezesha kuwapenda wengine, jibu ni, kwa sababu yule mtu amezaliwa mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili ni kazi ambayo Mungu Roho Mtakatifu anafanya wakati yeye anamwunganisha yule ambaye amekufa kwa Kristo Yesu ili maisha ya Mungu yawe maisha yake na upendo wa Mungu uwe upendo wake.

Jambo hili tunaliona wazi katika 1 Yohana 4:7-12. Yohana anafundisha jambo hili kwa njia mbili. Kwanza Yohana anasema kwamba upendo ndiyo utu wa Mungu na yule ambaye amezaliwa mara ya pili pia atakuwa na utu wa upendo. Pili, Yohana anasema kwamba kwa sababu Mungu ni Mungu wa upendo, amemtuma Mwana wake Yesu Kristo akuje hapa ulimwenguni ili sisi wenyewe tuweze kuwa na maisha ya milele kupitia kwake. Katika sura hii tutaona haya mambo mawili.

### Utu wa Mungu ni upendo.

1. Kwanza, katika mistari 7-8, Yohana anatufundisha kwamba utu wa Mungu ni upendo. Yohana anasema katika kifungu hiki, “Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu naye anajua Mungu. Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo.” Tazama Yohana hapa anafundisha mambo mawili. Kwanza, Yohana anasema kwamba upendo umetoka kwa Mungu. Pili, katika mstari wa 8, Yohana anasema “Mungu ni upendo.” Wakati Yohana anasema “Upendo umetoka kwa Mungu,” anamaanisha kwamba utu wa Mungu ni utu wa upendo, na upendo unatoka

kwake kama tu vile joto linatoka kwa moto na mwangaza unatoka kwa jua. Mungu ni Mungu wa upendo, moyo wake ni moyo wa upendo, Mungu anapenda kwa sababu Yeye ni upendo, kama vile jua linatoa mwangaza kwa sababu jua linaangaza.

Yohana hapa anafundisha kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili, utu wa Mungu unakuwa utu wake. Wakati Mungu anamzaa mtu mara ya pili, yule mtu anapewa maisha ya Mungu, na maisha haya yanayo upendo ndani yake. Utu wa Mungu ni upendo na wakati wewe unazaliwa mara ya pili utu wake unakuwa utu wako pia.

Katika mstari wa 12, Yohana anasema hii: "Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote. Kama tukipendana, Mungu anakaa ndani yetu na upendo Wake umekamilika ndani yetu." Hapa Yohana anamaanisha kwamba wakati mtu anazaliwa mara ya pili, Mungu menyewe anakuja kwake na kukaa ndani yake. Upendo Wake Mungu unaingia moyoni mwake (Warumi 5:5). Ni lengo la Mungu kwamba upendo wake utakamilishwa ndani ya huyu mtu. Kumbuka kwamba ni upendo wa Mungu mwenyewe ambao unakuja ndani ya yule ambaye ameokoka.

Kwa hivyo, jambo la kwanza ambalo Yohana anatufundisha hapa ni kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili, upendo wa Mungu utaingia moyoni mwake kwa sababu Mungu mwenyewe anakuja na kuishi ndani yake.

2. Pili, Yohana anaendelea kusema, "Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. Huu ndio upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. Wapenzi kama Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi tupendane." (1 Yohana 4:9-11). Hapa Yohana anasema kwamba upendo wa Mungu

ulifunuliwa wakati Mungu alimtuma Mwana wake Yesu Kristo. Hili ndilo jambo Yohana anafundisha mara mbili katika mistari wa 9 na 10. Yohana anasema kwamba Mungu alimtuma Mwana wake ili Yeye, kupitia kwa kifo chake aweze kuondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu yetu. Kwa hivyo hapa Mungu alionyesha upendo wake, kwa sababu Kristo aliondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu yetu kwa kuhukumiwa badala yetu (Warumi 8:3; Wagalatia 3:13).

Hili ni jambo la kutushangaza sana. Ulikuwa upendo wa Mungu ambao ulimtuma Kristo akuje hapa ulimwenguni kufa kwa ajili ya watu wa Mungu. Ni kwa sababu ya upendo wa Mungu kwamba Kristo alilipa deni la dhambi zetu, hii yote ilikuwa kazi ya Mungu mwenyewe kuondoa ghadhabu yake.

Jinsi Kristo alifanya jambo hili limeandikwa katika 1 Yohana 3:16: "Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu kwa sababu Yesu Kristo aliutoa uhai Wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa kutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu." Kwa hivyo Yesu Kristo aliondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu yetu kwa kufa kwa ajili yetu. Kifo chake Yesu Kristo kinatuonyesha utu wa Mungu na upendo wa Mungu. Mungu ni mwenye upendo, na upendo wake unaonekana katika kifo cha Yesu Kristo.

Angalia pia ni nini Yohana anasema katika kifungu hiki, "Huu ndiyo upendo, si kwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Yohana 4:10). Yohana hapa anafundisha kwamba upendo wa Mungu ndiyo msingi wa upendo wetu. Yohana anafundisha hapa kwamba upendo unaanza kwa Mungu: Yeye ndiye chanzo cha upendo wote. Halafu yule ambaye ameokoka atakuwa na upendo ndani yake kwa sababu maisha ya Mungu yameingia ndani yake.

Kwa hivyo hapa tumeona mambo mawili kuhusu upendo wa Mungu. Kwanza, tumeona kwamba utu wa Mungu ni upendo, na kwa hivyo wakati tunazaliwa mara ya pili, sisi pia tutakuwa na utu wa upendo. Pili, Yohana anatufundisha hapa kwamba upendo wa Mungu ulifunuliwa wakati Mungu alimtuma Mwanawake Yesu Kristo aje hapa ulimwenguni ili sisi tuweze kuwa na maisha ya milele kupitia kwake.

Tazama katika 1 Yohana 4:11, Yohana anaandika, "Wapenzi, kama Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana." Hapa, wakati Yohana anasema, "imetupasa na sisi kupendana," yeye hamaanishi kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanahitaji kujaribu sana kuwapenda wengine, na kuona kama kweli wanaweza kuwapenda wengine. Yohana hamaanishi hivyo. Bali, Yohana anamaanisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anapaswa kuwa mtu wa upendo, kama tu yule mtoto ambaye amezaliwa anapaswa kuanza kupumua. Mtoto ambaye amezaliwa saa hii hahatiji yeyote kumfundisha kupumua, na hahitaji yeyote kumkumbusha kupumua; kupumua ni jambo ambalo yeye anafanya bila kuambiwa afanye.

Tunaweza kusema kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili anajua kwamba Kristo alikuja hapa ulimwenguni na kufa kwa ajili yake; na hii itamhimiza kuwapenda wengine. Pia, yule ambaye amezaliwa mara ya pili anayo maisha ya Mungu ndani yake na hii ndiyo sababu anawapenda wengine: maisha yake Yesu Kristo na kifo chake, na maisha ya Mungu ndani yake: hivi vitu viwili vitamwezesha huyu mtu kuwapenda wengine. Wakati tunazaliwa mara ya pili, tunaweza kufahamu upendo wa Mungu ambao Yesu Kristo alituonyesha wakati alikufa kwa ajili yetu, na upendo huu wa Mungu unatuwezesha kuwapenda wengine kwa upendo huo huo.

Kwa hivyo, katika sura hii ninataka kuonyesha ni namna gani upendo wa Mungu ambao ulionekana wakati Kristo alikuja hapa

ulimwenguni na kufa kwa ajili yetu unashikana na upendo wetu ambao tunawaonyesha wengine.  Mtu akimwuliza yule ambaye amezaliwa mara ya pili, “Je, ni namna gani upendo wa Mungu unakuwezesha kuwapenda wengine?” jibu ni, “Kwa sababu nimezaliwa mara ya pili.”  Kuzaliwa mara ya pili ni kazi ya Mungu Roho Makatifu wakati analeta Yesu Kristo na maisha Yake kwa yule mtu ambaye amekufa katika dhambi na makosa.  Wakati Roho Mtakatifu anamleta Yesu Kristo na maisha yake kwa mtu ambaye hajaokoka, yule mtu anazaliwa mara ya pili na kwa hivyo upendo wa Mungu sasa utakuwa ndani yake.

Upendo wa Mungu ni utu wa Mungu, na upendo wa Mungu unaonekana wakati tunamwamini Kristo ambaye alikuja hapa ulimwenguni kutuokoa kutoka kwa dhambi zetu.  Yesu Kristo alikuja hapa ulimwenguni kuondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu ya wenye dhambi, ili wale ambao wanazaliwa mara ya pili waweze kuwa na maisha ya milele.  Wakati tunazaliwa mara ya pili tunaunganishwa na upendo wa Kristo, na kwa hivyo tunajulikana kuwa watoto wa Mungu.  Ikiwa tumezaliwa mara ya pili tutapendana.

## Ni namna gani wale ambao wamezaliwa mara ya pili huwapenda wengine.

Katika sehemu ya sura hii ninataka kufundisha ni namna gani wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanawapenda wengine.  Biblia inasema, “Wapenzi, kama Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana” (1 Yohana 4:11).  Wale ambao wamezaliwa mara ya pili ni watu wa upendo.  Wale ambao wamezaliwa mara ya pili, upendo wa Mungu uko ndani yao.  Hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Sisi tunajua ya kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda ndugu” (1 Yohana 3:14).

Kuna njia mbili ambazo upendo wa Mungu utaonekana katika maisha ya kila siku ya wale ambao wamezaliwa mara ya pili.

Biblia inasema, "Hili ndilo neno mlilolisikia tangu mwanzo, kwamba imetupasa tupendane sisi kwa sisi. Msiwe kama Kaini aliyekuwa wa yule mwovu akamwua ndugu yake. Basi kwa nini alimwua? Ni kwa sababu matendo yake Kaini yalikuwa mabaya na ya ndugu yake yalikuwa ya haki. Ndugu zangu, ninyi msistaajabu kama ulimwengu ukiwachukia Sisi tunajua kwamba tumepita kutoka mautini kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda ndugu. Kila asiyempenda ndugu yake akaa mautini" (1 Yohana 3:11-14).

Tazama kwamba katika kifungu hiki, Yohana anasema, "Msiwe kama Kaini aliyekuwa wa yule mwovu akamwua ndugu yake. Ni kwa sababu matendo yake Kaini yalikuwa mabaya na ya ndugu yake yalikuwa ya haki." Yohana hapa anatueleza upendo wa yule ambaye amezaliwa mara ya pili ni wa aina gani. Je, ni kwa nini Kaini alimwua ndugu yake Abeli? Ni kwa sababu Mungu alipokea sadaka za Abeli lakini hakupokea sadaka za Kaini. Kwa kumwua ndugu yake, Kaini alikuwa mfano wa ni namna gani mtu ambaye hajazaliwa mara ya pili anavyohisi wakati anamwona mwingine akifaulu. Yohana ansema kwamba ikiwa mtu mmoja ambaye amezaliwa mara ya pili anaona kwamba mwingine ambaye pia amezaliwa mara ya pili anafaulu sana katika huduma wake kwa Mungu, yeye hatakuwa na wivu na uchungu moyoni mwake, bali atafurahia hata kama huduma wake unaonekana kuwa tu ndogo. Biblia inatufundisha kwamba Kaini alikuwa na sababu kwa nini alimwua ndugu yake: ni kwa sababu aliona kwamba ndugu yake alikuwa mwenye haki na yeye mwenyewe alikuwa mtu mwovu, na kwa hivyo alijawa na hasira. Hii ndiyo sababu alimwua ndugu yake. Yeye aliona wema wa ndugu yake na pia aliona dhambi ambayo ilikuwa ndani yake yeye mwenyewe na kwa hivyo alikuwa na hatia. Hii ndiyo sababu alimwua Abeli. Abeli hakuhitaji kusema chochote kuhusu maisha yake, kwa sababu tabia ya maisha yake ilimwonyesha Kaini kwamba yeye Kaini alikuwa mwenye dhambi, na yeye Abeli alikuwa mwenye haki. Kaini alipaswa kutubu dhambi zake na kumwomba Mungu ampe moyo mpya, lakini badala yake, alimwua Abeli kwa sababu Abeli alimkumbusha

kwamba yeye ni mwenye dhambi. Ni kama mtu ambaye anajiangalia katika kioo na kuona sura yake si mzuri hata kidogo na kwa hivyo anavunja kioo.

Biblia hapa inatufundsha kwamba hata wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanaweza kuwa kama Kaini katika jambo hili. Kwa mfano, mtu fulani ambaye amezaliwa mara ya pili anayo dhambi ambayo imebaki ndani yake, na anakumbushwa kuhusu jambo hili kila wakati anakutana na mtu fulani. Huyu mtu anapaswa kushughulikia hii dhambi ambayo imebaki ndani yake, lakini badala yake yeye atapuuza yule mwingine ambaye kila wakati anamkumbusha kuhusu hii dhambi yake. Wakati mwingine, badala ya kushughulikia dhambi yake ambayo imebaki ndani yake, yeye anaanza kusema mambo mabaya kumhusu yule ndugu yake ambaye anamkumbusha kuhusu dhambi yake.

Biblia hapa inatufundisha kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili sasa anao upendo wa Mungu ndani yake na kwa hivyo yeye hatampuuza au kusema mambo mabaya kumhusu. Yule ambaye ako na upendo wa Mungu ndani yake atafurahi wakati ndugu yake anamhudumia Mungu kwa bidii na anafaulu katika huduma wake. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili hatampuuza ndugu yake ambaye anamkumbusha kuhusu dhambi fulani ambayo imebaki ndani yake, bali ataomba Mungu kushu dhambi hii na kuitubu.

Kwa hivyo Biblia hapa inatufundisha hivi: kila mahali ambapo unaona mtu akifaulu katika maisha yake ya ukristo na katika huduma wake kwa Mungu, hakikisha kwamba unayo furaha moyoni mwako kwa sababu ndugu yako anafaulu katika mambo haya. Hakikisha kwamba unamshukuru Mungu kwa sababu ya mambo haya. Usiwe kama Kaini ambaye alikuwa na hasira kwa sababu sadaka ya Abeli ilipokelewa na Mungu.

Upendo ni unyenyekevu na upendo unafurahia wakati watu wa Mungu wengine wanafaulu katika maisha yao ya ukristo. Hii

ndiyo njia upendo wa Mungu unaonekana wakati uko ndani ya maisha ya yule ambaye amezaliwa mara ya pili.

2. Jambo la pili ambalo Yohana anasema ni hili: “Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu, kwa sababu Yesu Kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yetu. Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu. Ikiwa mtu anavyo vitu vya ulimwengu huu na akamwona ndugu yake ni mhitaji lakini asimhurumie, upendo wa Mungu wakaaje ndani ya mtu huyo? Watoto wangu wadogo, tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali kwa tendo katika kweli” (1 Yohana 3:16-18).

Katika kifungu hili, Yohana anasema mambo matatu wazi kuhusu dhambi.

Kwanza, Yohana anasema kwamba upendo unawasaidia watu katika maisha yao ya kila siku. Anasema, “Watoto wangu wadogo, tusipende kwa maneno au kwa ulimi bali kwa tendo katika kweli” (mstari wa 18). Anasema hapa kwamba wakati unaona mhitaji, usiongee tu kuhusu upendo, hakikisha kwamba unafanya kitu cha kumsaidia.

Pili, Yohana hapa anaendelea kutuambia kwamba jambo hili ni la muhimu sana. Anasema, “Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu” (mstari 16). Kristo alitupenda kwa kutoa maisha yake kwa ajili yetu. Wakati tulizaliwa mara ya pili, upendo wake ulikuwa upendo wetu. Kwa hivyo yule ambaye amezaliwa mara ya pili ako tayari kufa kwa ajili ya kuwasaidia wengine. Uwepo wa Yesu Kristo katika moyo wa yule ambaye amezaliwa mara ya pili ni uwepo wa moyo wa mtumishi. Yeye ako tayari kujitoa kwa ajili ya wengine, yeye ako tayari kufanya chochote ambacho anahitaji kufanya ili awasaidie wengine. Yeye hana moyo wa kupata fedha kutoka kwa wengine, bali ako tayari kujitoa kwa ajili ya wengine, hata kama inamgharimu maisha yake. Yeye anajua kwamba Mungu atamchunga.

Kwa hivyo kwanza Yohana anasema kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili atakuwa tayari kuwasaidia wengine katika maisha yao ya kila siku. Jambo la pili Yohana anasema hapa ni kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili atakuwa tayari kujitoa kwa ajili ya kuwasaidia wengine, hata kama itamgharimu.

Tatu, Yohana hapa anasema kwamba yule ambaye amezaliwa mara ya pili atahitaji kujitoa kwa ajili ya wengine. Yohana anasema, "Ikiwa mtu anavyo vitu vya ulimwengu huu na akamwomna ndugu yake ni mhitaji lakini asimhurumie, upendo wa Mungu wakaaje ndani ya mtu huyo?" (mstari wa 17). Yohana anasema hapa kwamba wale ambao wako na vitu vya dunia hii wanapaswa kuwa tayari kugawanya vitu hivi na madugu zao. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili hawazi tu juu ya nini anaweza kupata, bali anajua kwamba kila kitu anacho ni cha Mungu na si chake, na kwa hivyo Mungu anaweza kutuamrisha kutumia vitu vyake kwa ajili ya watu wa dunia. Mungu ni upendo na wakati tunazaliwa mara ya pili sisi pia tunakuwa watu wa upendo. Upendo wa Mungu unatawala jinsi tunatumia mali yetu.

Kwa hivyo sisi sote ambao tumezaliwa mara ya pili tunapaswa kuwa wale ambao wanawapenda wengine katika maisha ya kila siku na si kwa maneno tu. Tunapaswa kuwa wale ambao wako tayari kutoa hata maisha yao kwa ajili ya wengine, kama tu Kristo alivyotoa maisha Yake kwa ajili yetu. Tunapaswa kukumbuka kwamba kila kitu tunacho ni cha Mungu na tunapaswa kukitumia kwa kuwapenda wengine. Tukumbuke kwamba sisi ni watu wa Mungu, sisi ni watoto wake, sisi tuko na utu wake. Huu ndiyo upendo.

Ninaomba kwamba Mungu atatupatia njia mpya ya kufahamu upendo wake ambao ulidhihirishwa wakati Yeye alimtuma Mwana wake aje hapa ulimenguni kufa kwa ajili ya watu wake.

Wakati tunawaza juu ya upendo wa Mungu katika Kristo, tunapaswa kuomba kwamba tutajua kwa hakika kwamba kweli tumezaliwa mara ya pili kwa sababu ya upendo wa Mungu.

"Wapenzi na tupendane, kwa kuwa upendo watoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na Mungu naye anamjua Mungu" (1 Yohana 4:7).

# Sehemu ya Tano

## Je, ni namna gani tunaweza kuwasaidia wengine ili wazaliwe mara ya pili?

*"Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni. Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele. Maana, 'Mwili wote ni kama majani na utukufu wote wa binadamu ni kama ua la majani, majani hunyauka, lakini neno la Mungu ladumu milele.' Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu.*

*Kwa hivyo, wekeni mbali nanyi uovu wote na udanganyifu wote, unafiki, wivu na masingizio ya kila namna. Kama watoto wachanga, waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya kiroho yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu, ikiwa kweli mmeonja ya kwamba Bwana ni mwema".*

1 Petro 1:22-2:3

# Waambieni watu wote habari njema ya Yesu Kristo

Biblia inafundisha kwamba kazi ya kuwazaa wenye dhambi mara ya pili ni kazi ya Mungu pekee na hakuna yeyote mwingine ambaye anaweza kufanya kazi hii (1 Yohana 5:1). Kuna wale ambao wakati wanafahamu hii, wanahimizwa sana kuenda nje na kuhubiri neno la Mungu kwa wote, kwa sababu wamefahamu kwamba ni Mungu pekee ambaye anawaokoa watu. Lakini pia, kuna wale ambao wanaacha kazi ya kuhubiri neno la Mungu wakati wanafahamu kwamba ni Mungu ambaye anawaokoa wenye dhambi. Wao wanawaza, “Ikiwa Mungu anawaokoa wenye dhambi na kazi yote ya kuwaokoa wenye dhambi ni Yake, mimi sina haja ya kuenda nje na kuhubiri neno la Mungu. Mungu atawaokoa wale ambao amewachagua.”

Lakini haya ni mawazo mabaya. Ni kweli kwamba ni Mungu ambaye anawaokoa wenye dhambi na ni Yeye ambaye atachagua ni nani ataokoa na namna gani. Lakini sisi tunapaswa kuomba Mungu kwamba atatupatia ujasiri na uwezo wa kuwahubiria watu wote neno la Mungu.

Katika sura hii, ninataka kuangalia jambo hili: ni nini tunapaswa kufanya ili tuwasaidie wengine wazaliwe mara ya pili? Katika kitabu hiki tumeona kazi ya kumzaa mtu mara ya pili ni kazi ya Mungu, lakini pia tumeona kwamba mtu akitaka kuzaliwa mara ya pili yeye ana mambo ambayo anapaswa kufanya, na kama hatafanya mambo hayo, basi yeye hatazaliwa mara ya pili. Je, ni namna gani tunaweza kuwasaidia wale ambao wanataka kuzaliwa mara ya pili ili wao wafanye yale ambayo wanahitaji kufanya ili wazaliwe mara ya pili?

Jibu la Biblia la swali hili ni rahisi na wazi. Biblia inasama kwamba tunahitaji kuwaambia wote habari njema kumhusu Yesu Kristo kutoka kwa moyo wa upendo na maisha ya huduma. Hili ndilo jambo ambalo Paulo alifundisha, “Kwa maana hatujihubiri sisi wenyewe ila tunamhubiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana na sisi ni watumishi wenu kwa ajili ya Yesu” (2 Wakorintho 4:5). Watu wa Mungu wanapaswa kumhubiri Kristo, kwamba Yeye ni Bwana na wao ni watumishi wake.

Kuwa watumishi inamaanisha kuwa watu wanyenyekevu na kuwa kiwango moja na watu wote wa dunia. Wale ambao wanataka kuonekana kwamba wao ni watu wa kiwango cha juu kuliko wengine na ni watu wa kiburi na majivuno hawafanyi kazi ya Mungu kwa njia inayofaa.

Katika kifungu cha 1 Petro 1:22-25, tunaona ni namna gani yule ambaye amezaliwa mara ya pili anawashuhudia watu wa ulimwengu ukweli kuhusu Yesu Kristo. Hapa tunafundishwa ni namna gani tunapaswa kuhubiri habari njema ya Yesu Kristo kwa wale ambao hawajaokoka.

Kifungu hiki kinasema, “Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni. Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele. Maana, ‘Mwili wote ni kama majani na utukufu wote wa binadamu ni kama ua la majani, majani hunyauka, lakini neno la Mungu ladumu milele.’ Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu.”

Kwanza, Petro anasema, “Basi kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli kwa njia ya Roho kwa kuwapenda ndugu zenu kwa upendo wa kweli, pendaneni kwa dhati kutoka moyoni” (mstari 25). Hapa Petro anamaanisha kwamba hawa watu ambao anawaandikia wamezaliwa mara ya pili. Hii ndiyo maana ya

"mmejitakasa nafsi zenu." Wao walizaliwa mara ya pili kwa kulitii ukweli wa Mungu, yaani neno la Mungu. Wakati mtu anatii ukweli wa Mungu, yeye anakuwa na imani ndani ya Kristo.

Hii inamaanisha kwamba upendo kwa wengine unazaliwa ndani ya yule ambaye amezaliwa mara ya pili. Hii ndiyo sababu Petro hapa anasema, "Ninyi mmezaliwa mara ya pili kwa sababu mmetii neno la Mungu, sasa pendaneni kwa dhati kutoka moyoni."

Halafu katika mstari wa 23 anasema, "Kwa maana mmezaliwa upya, si kwa mbegu ile iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika, kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele." Mstari huu ni muhimu sana kwa kutueleza ni namna gani tunaweza kuwasaidia wengine kuzaliwa mara ya pili. Petro hapa anasema, "Mmezaliwa upya...kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu." Yaani, Petro hapa anasema kwamba ile mbegu ambayo Mungu anatumia kuwazaa wenye dhambi mara ya pili ni mbegu ya neno la Mungu. Hii ndiyo njia ambayo Mungu anatumia kuwazaa wenye dhambi mara ya pili.

### Je, neno la Mungu ni nini?

Kabla ya kuona ni namna gani tunaweza kuwasaidia wengine wazaliwe mara ya pili, tunahitaji kufahamu neno la Mungu ni nini. Katika Biblia, "neno la Mungu" linamaanisha mambo tofauti tofauti. Ulimwengu uliumbwa na neno la Mungu (Waebrania 11:3). Yesu Kristo mwenyewe anaitwa neno la Mungu (Yohana 1:1,14). Amri Kumi za Mungu pia zinaitwa neno la Mungu (Marko 7:13). Ahadi ambazo Mungu aliwapatia watu wa Israeli zinaitwa neno la Mungu (Warumi 9:6).

Katika kifungu hiki, wakati Petro anaongea kuhusu neno la Mungu anamaanishi jambo lingine. Kwanza, Petro anasema, "Mmezaliwa upya...kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele" (mstari 23). Neno la Mungu liko hai kwa sababu liko na uwezo wa

Mungu kuwapatia maisha mapya. Na neno la Mungu linadumu kwa sababu baada ya kuzaa maisha ndani ya mtu, linamhudumisha milele.

Katika kifungu hiki Petro ananukuu Isaya 40:6-8 kueleza kwamba neno la Mungu linadumu milele: "Mwili wote ni kama majani na utukufu wote wa binadamu ni kama ua la majani, majani hunyauka na ua lake hupukutika, lakini neno la Mungu linadumu milele" (1 Petro 1:24-25). Neno la Mungu si kama majani au maua. Majani na maua yanaishi kwa nuda kidogo na halafu yanapita. Lakini neno la Mungu si hivi. Yale maisha ambayo neno la Mungu yanazaa yatadumu milele kwa sababu neno lenyewe ambalo lilizaa maisha haya linadumu milele.

Kwa hivyo Petro hapa anatuambia ni nini anamaanisha wakati anaongea kuhusu "Neno la Mungu." Petro anasema, "Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu" (mstari 25). Habari njema ambayo inahubiriwa kwa wenye dhambi kila wiki ndiyo ile mbegu ambayo haiharibiki, bali ni neno ambalo linadumu hata milele. Hili ndilo neno ambalo Mungu analitumia kuwaokoa wenye dhambi kutoka kwa dhambi zao na kutoka kwa ghadhabu ya Mungu.

Habari njema, ambayo tunahubiria wenye dhambi wote ni hii: Mwana wa Mungu alikufa kwa ajili ya wenye dhambi, alikufa kwa niaba yetu. Yeye alikufa msalabani kulipa deni la dhambi zetu. Yeye aliishi maisha bila dhambi hapa ulimwenguni ili yeye aweze kuwa haki yetu. Yeye alikufa juu ya msalaba kuondoa dhambi zetu na kuondoa ghadhabu ya Mungu. Yeye alifufuka ili ashinde kifo na ili sisi tuweze kupata maisha ya milele na furaha katika uwepo wake. Na kwa sababu ya maisha yake na kifo chake na kufufuka kwake, wale ambao watakuja kwake kupitia kwa imani watapata wokovu kutoka kwa dhambi zao zote bila malipo yoyote. Hii ni habari njema ambayo tunahitaji kuwahubiria wenye dhambi wote. Hii ndiyo habari njema ambayo imehubiriwa kwa miaka 2,000, na hata leo hii ndiyo habari njema ambayo inahubiriwa kwa

wenye dhambi wote. Ni jambo la kutuhuzunisha kwamba kuna mamilioni hapa ulimwenguni ambao hawajasikia habari hii.

Hii yote inamaanisha kwamba ikiwa mtu atazaliwa mara ya pili, yeye kwanza anahitaji kusikia mahubiri ya neno la Mungu ambayo yanawaeleza watu ujumbe wa injili ya Yesu Kristo. Wao watazaliwa mara ya pili kupitia "Kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele," yaani ujumbe wa injili (1 Petro 1:23).

Kwa hivyo kazi ya Mungu na jukumu la wale ambao wamezaliwa mara ya pili yanaambatana hivi:

Kwanza, Mungu anamwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili kupitia kwa mbegu ya neno la Mungu, yaani ujumbe wa injili.

Pili, yule ambaye amezaliwa mara ya pili anawahubiria wengine neno la Mungu, na Mungu anatumia mahubiri hayo kuwawezesha wengine kuzaliwa mara ya pili.

Mungu anawawezesha watu kuzaliwa mara ya pili kupitia kwa habari kuhusu Kristo ni nani na ni nini amefanya juu ya msalaba na katika kufufuka kwake.

Mungu anawapatia maisha mapya kwa wale ambao wamekufa katika dhambi kupitia kwa maneno ya yule ambaye amezaliwa mara ya pili wakati yeye anaongea kuhusu ujumbe wa injili.

Kwa ufupi tumeona katika sura hii kwamba wale ambao wamekufa katika dhambi zao wanazaliwa mara ya pili wakati watu wa Mungu wanahubiri neno la Mungu. Wakati sisi tunahubiri na kuongea ujumbe wa injili, Mungu anatumia neno lake kufungua macho ya wale ambao hawajaokoka ili waweze kuona wokovu ambao uko ndani ya Yesu Kristo, na anafungua masikio ya wale ambao hawajaokoka ili waweze kusikia neno la Mungu na kuokoka.

Hii inamaanisha kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanaweza kumhudumia Mungu kwa kuhubiri neno lake kwa wote ambao hawajaokoka. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Kwa mapenzi Yake yeye mwenyewe alituzaa kwa Neno la kweli, kusudi tuwe kama mazao ya kwanza katika viumbe Vyake vyote” (Yakobo 1:18). Yakobo anasema hapa kwamba mtu anazaliwa mara ya pili “kwa Neno la Mungu.” Pia, hii ndiyo sababu Biblia inasema, “Ninyi ni taifa teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu la Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu” (1 Petro 2:9). Mungu alitutoa kutoka kwa giza na alituleta katika nuru yake kupitia kwa neno la Mungu, yaani ujumbe wa injili (1 Petro 1:23,25). Sasa wakati tunaingia katika ufalme huu wa nuru, je, ni nini tunapaswa kufanya? Je, ni kwa nini Mungu ametuleta katika ufalme wa nuru? Petro anasema, “Mlioitwa ili kutangaza sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu” (1 Petro 2:9). Tumeletwa katika nuru ili tuishi maisha matakatifu na ya furaha na kuwahubiria wote neno la Mungu ili wengine pia wazaliwe mara ya pili. Na wakati wao wanazaliwa mara ya pili, wao pia wanaingia katika nuru na kuishi maisha matakatifu na ya kumtukuza Mungu. Kwa hivyo furaha yetu inakuwa kamili.

### Mfano wa wakristo wa Yerusalemu.

Katika kitabu cha Matendo ya Mitume tunasoma kwamba watu wa Mungu walikaa katika mji wa Yerusalemu. Wao walipaswa kuenda “Uyahudi kote na Samaria hadi mwisho wa dunia” (Matendo ya Mitume 1:8), lakini wao walikaa tu mji wa Yerusalemu. Kwa hivyo Mungu alimwinua Stefano kuwa shahidi wa nguvu sana (Matendo ya Mitume 6:10), hadi maadui wa Mungu walilazimishwa kumwua (Matendo 7:60).

Wakati hawa maadui walimwua Stefano, wakristo wote katika mji wa Yerusalemu waliteswa na walilazimishwa kutoroka Yerusalemu: “Siku ile kukatukia mateso makuu dhidi ya kanisa

huko Yerusalemu, waamini wote isipokuwa mitume wakatawanyika wakakimbilia Uyahudi na Samaria” (Matendo ya Mitume 8:1). Sasa wakati tunasoma Matendo ya Mitume 8:4, tunasoma maneno haya: “Kwa hivyo wale waliotawanyika wakalihubiri neno la Mungu kila mahali walipokwenda” (Matendo ya Mitume 8:4). Watu hawa wa Yerusalemu hawakuwa wahubiri; wao walikuwa wakristo wa kawaida tu, na walikuwa maelfu (Matendo ya Mitume 2:41). Baada ya kulazimishwa kutoroka manyumbani mwao, wao walienda kila mahali na kuhubiri neno la Mungu.

Hili ni jambo la kutushangaza. Wao walikuwa watu ambao waliteswa na maadui wa Mungu na walipoteza manyumba zao na kulazimishwa kutoroka manyumba zao. Lakini wakati walienda kila mahali, wao hawakulalamika na kulia-lia kuhusu majaribu yao, bali walihubiri neno la Mungu kila mahali.

Watu wa Mungu wote wanahitaji kupenda injili ya Mungu kama vile hawa watu wa Yerusalemu waliipenda, na pia tunahitaji kuwa na rehema na upendo kwa wale ambao hawajaokoka kwa sababu wao hawana msamaha wa dhambi na kwa hivyo hawana wokovu. Tunapaswa kuhakikisha kwamba hata kama tuko na mateso mengi na majaribu mengi sana, hatulalamiki na kulia-lia kuhusu majaribu yetu, bali tutaendelea kuhubiri neno la Mungu.

Hawa wakristo wa Yerusalemu walijaribiwa sana lakini walienda kila mahali na kuhubiri neno la Mungu. Hata leo tuna sehemu ya dunia ambapo watu wa Mungu wanajaribiwa na kuteswa sana lakini wao bado wanaendelea kuhubiri neno la Mungu, na kwa sababu ya ushuhuda wao, wengi wanazaliwa mara ya pili.

Je, ni namna gani sisi tunaweza kuwa kama hawa wakristo wa Yesusalemu ili sisi pia tuendelee kuhubiri neno la Mungu hata ule wakati tunateswa na maadui wa Mungu? Jibu la swali hili linapatikana katika maneno haya ya Petro: “Kwa hiyo, wekeni

mbali ninyi uovu wote na udanganyifu wote, unafiki, wivu na masingizio ya kila namna. Kama watoto wachanga, waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya kiroho yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu" (1 Peto 1:1-2).

Petro hapa anasema kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili ni kama watoto wachanga. Kwa kusema hii, Petro anamaanisha kwamba wao wako na njaa ya neno la Mungu kama vile mtoto mchanga anakuwa na njaa ya maziwa. Anasema hapa kwamba wale ambao wamezaliwa mara ya pili wanapaswa kutamani sana yale mafundisho ya ukweli. Wao wanafaa kupenda kutaka kile chakula ambacho hakina uchafu wowote.

Kwa hivyo Petro anatuambia katika kifungu hiki kwamba tumezaliwa mara ya pili kupitia kwa neno la Mungu. Halafu Petro anasema kuwamba tunahitaji kutamani neno la Mungu kila siku kama vile watoto wachanga wanavyotamani maziwa. Petro anasema kwamba tunahitaji kutamani neno la Mungu ili tukue katika imani yetu, kama tu vile mtoto mchanga anatamani maziwa ili akue kimwili. Neno la Mungu ni chakula cha yule ambaye ameokoka: "Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu" (Mathayo 4:4).

Petro hapa anasema ikiwa yule ambaye amezaliwa mara ya pili atakuwa bila uovu wote na udanganyifu wote na unafiki, wivu na masingizo, yeye anahitaji kutamani neno la Mungu kila siku. Pia ikiwa yule ambaye amezaliwa mara ya pili anataka kuwa na moyo wa kuhubiri neno la Mungu hata kama anajaribiwa na kuteswa, basi anafaa kutamani neno la Mungu kama vile mtoto mchanga anatamani maziwa.

Katika kifungu hiki Petro anaendelea kusema, "ikiwa kweli mmeonja ya kwamba Bwana ni mwema" (1 Petro 2:3). Hili ni jambo muhimu sana wakati tunataka kuwahubiria wengine neno la Mungu. Je, wewe mwenywe umeonja kwamba Bwana ni

mwema? Siulizi kwama umewaza juu ya Bwana Yesu Kristo. Siulizi kama unajua mambo fulani kumhusu Kristo. Ninauliza kama umezaliwa mara ya pili na kujua kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi. Yule ambaye amezaliwa mara ya pili na anajua moyoni mwake kwamba Mungu ni mwema na Mungu ni Mungu wa upendo na rehema, basi yeye atakuwa na moyo wa kuwahubiria neno la Mungu wenye dhambi wote kila wakati.

*“Kwa hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii kwa rehema za Mungu, hatukati tamaa. Tumekataa mambo ya siri na ya aibu, wala hatufuati njia za udanganyifu, tukichanganya Neno la Mungu na uongo. Kinyume cha hayo kwa kudhihirisha kweli waziwazi na kujitambulisha wenyewe kwenye dhamira ya kila mtu mbele za Mungu. Hata nayo Injili yetu kama imetiwa utaji, ni kwa wale tu wanaopotea. Kwa habari hiyo, mungu wa dunia hii amepufusha akili za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu. Kwa maana hatujihubiri sisi wenyewe ila tunamhubiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana na sisi ni watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa Mungu, Yeye aliyesema, ‘Nuru na ing’ae gizani,’ ameifanya nuru Yake ing’ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo. Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu”.*

2 Wakorintho 4:1-7

# "Ninawatuma kufungua macho yao."

Katika sura hii ninataka kuongea kuhusu kazi ya uinjilisti, yaani ile kazi ambayo wakristo wote wanafanya wakati wanawaelezea marafiki wao na watu wa jamii zao ujumbe wa injili. Hii ni kazi ambayo mamilioni ya watu wanafanya kila siku katika manyumba zao na maafisi. Hii ni kazi ambayo inafanywa na yule ambaye anamweleza rafiki yake ujumbe wa injili wakati wao wawili wanaongea kuhusu mambo ya dini; hii ni kazi ambayo mwanamke fulani anafanya wakati anamweleza jirani yake ni kwa nini yeye ameokoka. Kwa hivyo katika sura hii, ninataka kufundisha kuhusu kazi hii ya uinjilisti.

Katika kitabu hiki tumeona mara mingi mafundisho ya Petro wakati yeye alisema, "Mmezaliwa upya....kwa neno la Mungu lililo hai na linalodumu hata milele" (1 Petro 1:23). Petro anaeleza kwamba, "Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu" (1 Petro 1:25). Yaani, Mungu anamwezesha mtu kuzaliwa mara ya pili kupitia kwa mahubiri ya ujumbe wa injili. Ujumbe huu ni habari njema kwamba Mungu alimtuma Mwana wake hapa ulimwenguni kuishi maisha makamilifu, na kufa kwa ajili ya wenye dhambi, na kuondoa ghadhabu ya Mungu ambayo ilikuwa juu ya watu wake, kuondoa hatia ya dhambi zao na kuwafanya watu wake kuwa wenye haki na kuwapatia watu wake furaha ya milele ndani ya Yesu Kristo kupitia kwa imani pekee na si kwa matendo yao mema.

Wale ambao wamezaliwa mara ya pili, wamezaliwa mara ya pili kupitia kwa kusikia ujumbe wa injili, hakuna yeyote ambaye amezaliwa mara ya pili bila kusikia ujumbe wa injili. Biblia inasema, "Basi, imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa Neno la Kristo" (Warumi 10:17). Kwa hivyo wakati tunajiuliza swali hili, "Ni nini tunapaswa kufanya kuwasaidia wengine

kuzaliwa mara ya pili?" tunapaswa kujibu kwamba tunahitaji kuwaambia ujumbe wa injili kutoka kwa moyo wa upendo na maisha ya huduma.

Kwa hivyo katika sura hii ninataka kufundisha zaidi kuhusu kuwahubiria wengine ujumbe wa Mungu kutoka kwa moyo wa upendo na maisha ya huduma.

Katika Biblia tunasoma, "Kwa habari yao, mungu wa dunia hii amepofusha akili za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu" (2 Wakorintho 4:4). Biblia hapa inatufundisha kwamba wale ambao hawajaokoka ni vipofu. Wao hawawezi kumwona Kristo kuwa mwenye utukufu wote, na kuwa hivyo hawataki kumpokea kuwa Mkuu wao na Mwokozi wao. Kazi ya Mungu inahitaji kufanyika katika mioyo yao. Mungu anahitaji kufungua macho yao na kuwapatia maisha ili wao waweze kumwona na kumpokea Kristo kuwa Mwokozi wao na Bwana wao. Kazi hii ya Mungu ni kuwazaa mara ya pili.

Hii ndiyo sababu Biblia inasema, "Kwa kuwa Mungu, Yeye aliyesema, 'Nuru na ing'ae gizani,' ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo" (2 Wakorintho 4:6). Hapa tunaona tiba ya upofu ambayo tulisoma katika mstari wa 4. Hapa tunasoma kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Mungu ambaye mwanzoni aliumba nuru, anaumba nuru moyoni mwa yule ambaye amezaliwa mara ya pili. Nuru hii si kama nuru ya jua, bali ni "nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo," yaani, "nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu" (mstari wa 4). Mungu anawezesha moyo wa yule ambaye hajazaliwa mara ya pili kuona uzuri na ukweli na thamani ya Yesu Kristo, yaani utukufu wa Yesu Kristo.

Wakati yule ambaye hajazaliwa mara ya pili anamwona Kristo jinsi alivyo, yeye anampokea. Biblia inasema kwamba wale

ambao wanampokea Kristo, Yeye huwapatia haki ya kuwa watoto wa Mungu (Yohana 1:12). Hili ni jambo ambalo tunatamani kwa watoto wetu wote: tunatamani kwamba Mungu atafungua macho yao ili wao waweze kuona utukufu wa Yesu Kristo na kumpokea ili waweze kuzaliwa mara ya pili. Tunatamani kwamba nuru ya Mungu itang’aa moyoni mwao ili waweze kumwona na kumpokea Kristo. Tunatamani wao wazaliwe mara ya pili.

Paulo aliandika, “Kwa maana hatujihubiri sisi wenyewe ila tunamhubiri Yesu Kristo kuwa ni Bwana na sisi ni watumishi wenu kwa ajili ya Yesu” (2 Wakorintho 4:5). Kazi yake Paulo ilikuwa kumhubiri Kristo kutoka kwa moyo wa upendo na maisha ya huduma. Mahubiri yake yanaitwa injili, na yeye anasema, “Hata nayo Injili yetu kama imetiwa utaji, ni kwa wale tu wanaopotea” (2 Wakorintho 4:3). Wale ambao hawajaokoka hawawezi kuona ujumbe wa injili; wao ni vipofu. Pia wao hawawezi kusikia ujumbe wa injili kwa sababu hawana masikio ya kuusikia. Kwa hivyo, ni nini tunahitaji kufanya ili tuwasaidia watu kama hawa waweze kuzaliwa mara ya pili? Jibu ni kwamba tunahitaji kuwahubiria injili kwa moyo wa upendo na maisha ya huduma.

Ikiwa wale ambao hawajazaliwa mara ya pili wamekufa katika dhambi na makosa na hawawezi kusikia mahubiri ya ujumbe wa injili, je, kuna faida gani kwa watu wa Mungu kuwahubiria neno lake?

Tunapaswa kuwahubiria neno la Mungu kwa sababu Mungu anatumia mahubiri ya neno lake kuwaokoa wale ambao wamekufa katika dhambi na makosa. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 26, tunasoma kwamba Paulo alikuwa mbele ya Mfalme Agripa. Paulo alimwambia Agripa ni namna gani yeye aliokoka, na ni namna gani Mungu alimwita katika huduma wake. Alisema kwamba wakati yeye alikutana na Kristo katika barabara

ya Dameski na kuongea naye Kristo: “Nikauliza, ‘Ni nani wewe, Bwana?’ Naye Bwana akanajibu, ‘Ni Mimi Yesu unayenitesa. Lakini sasa inuka usimame, kwa miguu yako, kwa sababu nimekutokea kwa kusudi hili ili kukuweka utumike na kushuhudia juu ya mambo ambayo umeyaona na yale nitakayokutokea kwayo. Nitakuokoa kutoka kwa watu wako na watu Mataifa ambao ninakutuma kwao, uyafungue macho yao ili wageuke kutoka gizani waingie nuruni na kutoka kwenye nguvu za shetani, wamgeukie Mungu ili wapate msamaha wa dhambi na sehemu miongoni mwa wale waliotakaswa kwa kuniamini Mimi’” (Matendo ya Mitume 26:15-18).

Katika kifungu hiki, tunaona ni kazi gani sisi wanadamu tunaweza kufanya ili tuwasaidia wengine kuzaliwa mara ya pili. Yesu Kristo alimwambia Paulo, “Ninakutuma kwao, uyafungue macho yao ili wageuke kutoka gizani waingie nuruni na kutoka kwenye nguvu za shetani, wamgeukie Mungu ili wapate msamaha wa dhambi na sehemu miongoni mwa wale waliotakaswa kwa kuniamini Mimi” (Matendo ya Mitume 26:16-18).

Tumeona katika 2 Wakorintho 4:4 kwamba wale ambao hawajaokoka ni vipofu hadi Mungu afungue macho yao ili waweze kuona, yaani hadi Mungu awawezeshe kuzaliwa mara ya pili. Na hapa Kristo alimwambia Paulo, “Ninakutuma kwao, uyafungue macho yao.” Yaani Biblia inatufundisha kwamba Mungu anafugua macho ya wale ambao hawajaokoka ili waweze kuona ukweli na utukufu wa Mungu, na Mungu anafanya kazi hii kwa kuwatumia watu wake kuwahubiria habari njema kutoka kwa mioyo ya upendo na maisha ya huduma.

Hii ndiyo sababu kila wakati ninaomba, “Ee Mungu, utupatie tamaa kuwa watumishi wako ili tuhubiri neno lako kwa wale ambao hawajazaliwa mara ya pili, ili wao waweze kuona utukufu wa Mungu na kuokoka.” Msomaji, ninakuambia, “Nenda nje na uyafungue macho ya wale ambao hawajaokoka.”

Usiache kufanya kazi hiyo kwa sababu wewe huna uwezo wa kufungua macho ya wale ambao hawajaokoka. Ni kweli kwamba ni Mungu pekee ambaye anaweza kufungua macho ya wale ambao hawajazaliwa mara ya pili (2 Wakorintho 4:6). Lakini wewe unaweza kuwahubiria wengine ujumbe wa injili. Hii ndiyo njia Mungu anatumia kuwazaa wenye dhambi mara ya pili: kupitia kwa mahubiri ya neno lake ambalo ni ujumbe wa habari njema katika Yesu Kristo.

**Himizo kwa wahubiri.**

Katika sehemu hii ya sura hii, ninataka kukuhimiza kufanya kazi hii ya kuwahubiria wengine ujumbe wa injili kwa kukufundisha mambo machache.

***1. Fahamu kwamba Mungu hutumia vyombo vya udongo.***

Paulo aliandika hii: "Kwa kuwa Mungu, Yeye alisema, 'Nuru na ing'ae gizani,' ameifanya nuru Yake ing'ae mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu wa Mungu katika uso wa Kristo. Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu" (2 Wakorintho 4:6-7). Paulo hapa anatukumbusha kwamba sisi wanadamu ni wadhaifu kama vyombo vya udongo, lakini sisi tunayo hazina hii ndani yetu, yaani, ingawa sisi ni watu wadhaifu, sisi tunalo neno la Mungu ambalo Mungu analitumia wakati anawazaa wenye dhambi mara ya pili.

Tazama kwamba sisi wanadamu ni vyombo vya udongo: sisi si watu wenye nguvu na uwezo, sisi ni watu wa dhaifu. Sisi si hazina, neno la Mungu ni hazina; sisi wanadamu si dhahabu au fedha, sisi ni udongo. Lakini sisi tunayo hazina ya Mungu, yaani neno la Mungu.

Yule ambaye anajiwazia kuwa mtu mdhaifu na ni mtu ambaye hana uwezo sana amefahamu ukweli. Yule ambaye anajiwazia

kuwa mtumishi wa Mungu wenye nguvu sana na mwenye uwezo sana hajafahamu mafundisho ya Biblia na hajijui: yeye amejidanganya. Sisi wanadamu ni wadhaifu kama udongo, sisi hatuna uwezo kwa kumwokoa yeyote. Wakati Mungu anamwokoa mtu, anatumia mahubiri ya watu wake. Ingawa watu wake ni wadhaifu, neno lake ni hazina na Mungu analitumia kuwaokoa wenye dhambi.

Hii ndiyo sababu wakati Paul anapoongea kuhusu yeye mwenyewe na mhubiri mwingine ambaye aliitwa Apolo, alisema, "Kwani, Apolo ni nani? Naye Paulo ni nani? Ni watumishi tu ambao kwa kupitia kwao mliamini. Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye aliyekuza. Hivyo mwenye kupanda mbegu na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke Yake ndiye akuzaye" (1 Wakorintho 3:5-7).

Je, ni kwa nini Mungu anawatumia wale ambao ni wadhaifu, yaani wale ambao ni kama vyombo vya udongo? Paulo anasema, "Lakini tunayo hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa Mungu wala si kwetu" (2 Wakorintho 4:7). Mungu anataka kwamba utukufu wake ujulikane katika kazi ya wokovu. Yeye anataka kwamba wote wajue kwamba ni Yeye ambaye anawaokoa watu kutoka kwa dhambi zao kwa uwezo wake, na si wanadamu. Kwa hivyo ikiwa wewe unajiwazia kuwa mdhaifu na mtu ambaye hana uwezo mwingi ya kuwaeleza wenye dhambi neno la Mungu, wewe ndiye mtu ambaye Mungu atatumia kwa kazi yake. Yeye hatatumia yule ambaye anataka kuonekana kuwa mwenye uwezo nyingi na nguvu nyingi. Mungu atatumia yule ambaye ni mdhaifu na anaonekana kuwa mdhaifu ili uwezo wake wote ujulikane wakati mtu anaokoka.

Kwa hivyo, usikufe moyo bali jihimize ikiwa wewe ni mkristo wa kawaida tu na yule ambaye ni mdhaifu. Mungu anawatumia watu kama wewe kwa kazi yake ya kuhubiri ujumbe wa injili yake.

***2. Tumia vitabu na vijitabu.***

Kutumia vitabu na vijitabu ni njia nzuri ya kuwaeleza wengine injili ya Yesu Kristo. Jiwazie, "Kila wakati ninataka kuwaeleza watu injili ya Yesu Kristo, ninataka kuwaeleza watu ule ujumbe ambao Mungu anatumia kuwaokoa wenye dhambi." Hakikisha kwamba kila siku uko na vijitabu ambavyo unaweza kuwapatia watu. Pia hakikisha kwamba unaomba kila siku kwamba Mungu atakutumia kuwaeleza wengine neno lake. Omba kwamba Mungu atakutumia kufungua macho ya wale ambao wako katika dhambi zao.

***3. Fahamu kwamba Mungu anatumia njia nyingi na watu wengi kumwokoa mwenye dhambi.***

Kumbuka kwamba Mungu anaweza kuwatumia watu wengi kumshuhudia mtu mmoja. Pengine wewe umeongea na mtu fulani kumhusu Kristo, halafu baada ya masaa machache mwingine anakuja na kumpatia kijitabu kuhusu wokovu, na halafu baada ya masaa machche yeye anaweza kusikia mahubiri ya injili kwa radio. Pengine umeongea na mtu kuhusu injili ya Kristo na unawaza kwamba hakuna chochote ambacho kilitendeka moyoni mwake, lakini inaweza kuwa kwamba wengine pia wameongea naye na Mungu atatumia maneno ya ninyi nyote kumwokoa (1 Wakorintho 15:58).

***4. Hakikisha kwamba wewe ni mtu ambaye anawasaidia wengine bila kujijali.***

Yesu Kristo alisema, "Wapendeni adui zenu, watendeeni mema, wakopesheni bila kutegema kurudishwa mlichokopesha" (Luka 6:35). Watu wa Mungu wanapaswa kuwa wale ambao wanawasaidia wangine na ambao wako tayari kujitoa. Wale ambao wanajijali tu kwa maisha yao wanasema kwamba Yesu Kristo siyo Mwokozi wa rehema na upendo, na yeye siyo Mwokozi muhimu.

Ikiwa unawajua wale ambao hawajaokoka, hakikisha kwamba unawapatia vitabu vya ukristo bila kujijali. Pia kuwa tayari kuwasaidia watu kupata Biblia. Ikiwa mtu hana Biblia na anataka kuisoma, ukiweza, msaidie kupata moja. Kuna watu wengi ambao wameokoka kwa sababu wamesoma Biblia nyumbani mwao.

***5. Hakikisha kwamba unawajali watu.***

Wakati unakutana na mtu usiwe tu yule ambaye anaongea naye kuhusu Kristo na kumwacha. Hakikisha kwamba unajali yeye ni nani na anakaa wapi na afanya wapi, na mambo kama haya. Ikiwa mtu anajua kwamba wewe unajali mambo yake yeye atakuwa tayari kukusikia wakati unaongea naye kumhusu Kristo na wokovu.

***6. Waalike watu kanisani.***

Wakati unawashuhudia watu wa jamii yako na rafiki zako, hakikisha kwamba unawaalika waje kanisani nawe. Pengine, wao hawajui ukristo ni nini na ni namna gani watu wa kanisa lako wanamwabudu Mungu, lakini wakija kanisani, wataona ni namna gani mnafanya ibada yenu. Kumbuka pia kwamba mahubiri ya neno la Mungu yako na nguvu nyingi. Wakati mwingi Mungu anatumia mahubiri ya neno lake kuwaokoa wenye dhambi. Biblia inasema, "Kwa kuwa katika hekima ya Mungu, ulimwengu kwa hekima yake haukumjua Yeye, ilimpendeza Mungu kuwaokoa wale waaminio kwa upuzi wa lile neno lililohubiriwa" (1 Wakorintho 1:21).

***7. Hakikisha kwamba umejaza mji wako na mahubiri ya injili.***

Maadui wa Mungu waliwaambia mitume wa Kristo, "Tuliwaonya kwa nguvu msifundishe kwa jina hili, lakini ninyi mmeijaza Yerusalmeu yote mafundisho yenu" (Matendo ya Mitume 5:28). Hili ni jambo ambalo sisi sote tunahitaji kufanya. Tunahitaji

kuwapatia wote vijitabu vya ukristo na tunahitaji kuhakikisha kwamba wakristo wote wanaongea na rafiki zao na wafanyikazi wenzao kuhusu ujumbe wa Biblia. Kwa njia hiyo watu wa Mungu wanaweza kujaza mji yao na mafundisho ya Biblia.

***8. Tumia vipawa vyako.***

Kumbuka kwamba kila mmoja wetu anavyo vipawa tofauti tofauti na wewe hunahaja ya kumwiga mwingine ambaye anavyo vipawa tofauti nawe. Kila mkristo anahitaji kuwa mtumishi (Wagalatia 5:13), lakini kuna wale ambao wana vipawa vya kuhudumu (Warumi 12:7). Kila mkristo anahitaji kuwa na moyo wa rehema, lakini kuna wale ambao wanao kipawa cha rehema (Warumi 12:8). Kila mkristo anahitaji kuwahubiria na wengine kumhusu Kristo (1 Petro 2:9), lakini kuna wale ambao wana kipawa cha kufundisha na kuhubiri neno la Mungu (Warumi 12:7).

Biblia inafundisha kwamba watu wa Mungu wote wanapaswa kufanya kazi ya Ufalme wake pamoja. Wengine wamepewa vipawa fulani na wengine vipawa vingine. Hakikisha kwamba unajua vipawa vyako ni gani na hakikisha kwamba unavitumia vipawa vyako kwa utukufu wa Mungu. Hakikisha kwamba unakua katika ukristo wako na kwamba vipawa vyako pia vinakua. Usijaribu kuwa kama wengine ambao wako na vipawa tofauti na vyako: wewe tumia tu vipawa vyako.

***9. Soma vitabu ambavyo vinakufundisha kuhusu kuhubiri neno la Mungu.***

Kuna vitabu vingi ambavyo vimeandikwa kuwasaidia watu wa Mungu kujifunza ni namna gani wao wanaweza kuwahubiria rafiki zao kuhusu ujumbe wa injili. Kumbuka kwamba vitabu hivi vimeandikwa kwa faida yako ili uweze kumhudumia Mungu kwa kuhubiri neno lake.

***10. Omba Mungu akupe ujasiri.***

Wakati tunasoma Agano Jipya, tunaona kwamba wakati watu wa Mungu waliomba kwa ajili ya kazi ya kuhubiri neno la Mungu, mara mingi waliwaombea wale ambao walikuwa wanafanya kazi ya kuhubiri, si wale ambao walisikia neno la Mungu. Paulo pekee anawaombea wale ambao watasikia mahubiri wa neno la Mungu, "Ndugu zangu, shauku ya moyo wangu na maombi yangu kwa Mungu ni kwa ajili ya Waisraeli kwamba wataokolewa" (Warumi 10:1). Hapa Paulo anawaombea wale ambao watasikia mahubiri ya neno la Mungu. Lakini mahali pengine katika Agano Jipya tunasoma maombi kwa wale ambao walikuwa na jukumu la kuhubiri ujumbe wa injili. Kwa mfano, "Hatimaye, ndugu, tuombeeni ili kwamba Neno la Bwana lipate kuenea kwa haraka na kuheshimiwa kila mahali" (2 Wathesalonike 3:1), na, "Pia tuombeeni na sisi ili Mungu atufungulie mlango wa kunenea, ili tupate kuitangaza siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake pia mimi nimefungwa" (Wakolosai 4:3). Paulo anaandika, "Niombeeni na mimi pia, ili kila nifunguapo kinywa changu, nipewe maneno ya kusema niweze kutangaza siri ya Injili kwa ujasiri, ambayo mimi ni balozi wake katika vifungo. Ombeni kwamba nipate kuhubiri kwa ujasiri kama inipasavyo" (Waefeso 6:19-20).

Hakikisha kwamba unaomba kwamba wewe mwenyewe utakuwa na ujasiri wa kuhubiri neno la Mungu kila wakati utapata nafasi. Hakikisha pia kwamba utawaombea watu wa jamii yako na washiriki wa kanisa lako na wachungaji wa kanisa lako kwamba wao pia watakuwa na ujasiri. Tumeona hapa juu kwamba hata mtume Paulo alihitaji maombi ili awe na ujasiri, na yeye alikuwa mtume! Ikiwa yeye alihitaji maombi, sisi bila shaka tunayahitaji.

**Kuhubiri neno la Mungu kwa ujasiri.**

Wakati unaomba kwa kanisa lako, kumbuka maneno haya kutoka kwa Biblia, "Walipokwisha kuomba, mahali pale walipokuwa

wamekutanika pakatikiswa, nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri” (Matendo ya Mitume 4:31). Mungu akitubariki namna hii, sisi sote tutakuwa na ujasiri na furaha na tutahubiri neno la Mungu kila mahali. Hii ndiyo njia sisi wenyewe tulizaliwa mara ya pili, wakati tulisikia mahubiri ya neno la Mungu, na hii ndiyo njia wengine pia watazaliwa mara ya pili.

“Kwa maana mmezaliwa upya...kwa neno la Mungu lilillohai na linalodumu hata milele...hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu” (1 Petro 1:23-25).

# Kuzaliwa Upya na nchi mpya

Yesu Kristo alisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili" (Yohana 3:7). Maneno haya yanatuonyesha bila shaka taabu ya ulimwengu leo. Mwanadamu hawezi kuwa na amani na haki, na yeye hawezi kushinda mambo kama kuchukia na kujijali hadi yeye abadilishwe ndani ya moyo wake.

Watu wa ulimwengu wanajaribu kufanya mambo mengi kuhakikisha kwamba maisha yao hapa ulimwenguni yatakuwa maisha ya amani na furaha na bila taabu yoyote, lakini wao wameshindwa. Kila taifa liko na sheria kuhakikisha kwamba watu wa lile taifa wanaweza kuishi bila mateso na taabu, lakini hata sheria imeshindwa. Hii ni kwa sababu moyo wa mwanadamu ni moyo wa dhambi, na hadi mtu azaliwe mara ya pili, moyo wake utaendelea kuwa moyo wa dhambi na kuzaa matunda ya dhambi na kuharibu kiumbe chote.

Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili." Yesu Kristo alijua ni kwa nini watu wa ulimwengu wanafanya dhambi. Alijua kwamba wao wanafanya dhambi si kwa sababu ya mazingira yao au kwa sababu wamefundishwa na wengine kufanya dhambi, bali kwa sababu mioyo yao ni mioyo ya dhambi. Hii ndiyo sababu tunawadanganya wengine na kuwatukana wengine na kukosa kufanya majukumu yetu na kuwachukia wengine na kusema uongo na kujijali na kupenda pesa na kukosa kumheshimu Mungu.

Taabu ya sisi wanadamu ni kwamba kila dhambi ambayo tunafanya, tunafanya kwa sababu sisi ni wenye dhambi mioyoni. Taabu ya dhambi inapatikana ndani yetu. Kristo alisema, "Mti mwema huzaa matunda mazuri na mti mbaya huzaa matunda mabaya. Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya wala mti

mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri" (Mathayo 7:17-18). Pia, Yesu Kristo alisema, "Kinywa cha mtu huyanena yale yaliyojaza moyo wake" (Mathayo 12:14). Kristo hapa anasema kwamba mti fulani utazaa matunda mabaya kwa sababu mti wenyewe ni mbaya. Ikiwa mtu anapata matunda mabaya kutoka kwa ule mti, anajua kwamba ni kwa sababu mti huo ni mbaya. Vile vile, mtu anatenda matendo mabaya kwa sababu yeye ni mtu mbaya. Sisi sote tunafanya dhambi kwa sababu sisi sote ni wenye dhambi; tunazaa matendo mabaya kwa sababu mioyoni mwetu sisi ni watu wabaya. Hii ndiyo sababu tunafanya dhambi.

Wakati tunafahamu jambo hili tunafahamu ni kwa nini Kristo alisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili." Mtu akikataa kukubali kwamba moyo wake ni moyo wa dhambi na kwamba hii ndiyo sababu yeye anatenda dhambi, basi yeye atakataa kupokea mafundisho ya Yesu Kristo kwamba "Huna budi kuzaliwa mara ya pili." Mwanadamu ni mwenye dhambi kutoka ndani mwake. Haya ndiyo mafundisho ya Yesu Kristo. Yesu Kristo alipenda sana wanafunzi wake na Yeye alijua kwamba wanafunzi wake waliwahurumia watoto wao. Lakini Kristo alisema, "Ikiwa ninyi basi mlio waovu mnajua jinsi ya kuwapa watoto wenu vitu vizuri" (Mathayo 7:11). Yaani, aliwaambia wanafunzi wake, "Ninyi ni waovu." Mafundisho ya Kristo yanaambatana na mafundisho ya watumishi wengine wote katika Biblia. Nabii Yeremia aliandika, "Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu kupita kiasi. Ni nani awezaye kuujua?" (Yeremia 17:9).

Pia, Paulo aliandika kuhusu watu wote kwamba wao wanaishi, "Katika ubatili wa mawaza yao. Watu hao akili zao zimetiwa giza na wametengwa mbali na uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga wao na ugumu wa mioyo yao" (Waefeso 4:17-18). Paulo hapa anasema kwamba wanadamu wote wana mioyo ya dhambi, yaani mioyo migumu. Hii ndiyo hali ya kila mtu hapa ulimwenguni: "Hakuna mtu anayeishi mwenye haki mbele zako" (Zaburi 143:2).

Hii ndiyo sababu Yesu Kristo alisema kwamba tiba ya hali hii ya kiroho ni kuzaliwa mara ya pili: “Huna budi kuzaliwa mara ya pili.”

Kazi yake Yesu Kristo hapa ulimwenguni ilikuwa kuwazaa wenye dhambi mara ya pili. Yeye aliishi maisha bila dhambi yoyote hapa ulimwenguni. Yeye alikufa kwa ajili ya wenye dhambi. Yeye alichukua ghadhabu ya Mungu juu yake. Yeye alilipa deni la dhambi zetu na alitunununulia uzima wa milele. Yeye alihakikisha ahadi zote za Mungu. Yeye alifufuka kutoka kwa wafu. Yeye alishinda kifo na shetani. Yeye sasa anaketi kwa mkono wa kuume wa Mungu Baba na anatawala ulimwengu. Yeye ni mwakilishi wetu. Siku moja Yeye atarudi na kuwabariki watu wake ambao walikuwa chini ya laana ya Mungu kabla ya wao kuokoka. Kristo alifanya haya yote ili sisi tuweze kuzaliwa mara ya pili. Wale ambao watazaliwa mara ya pili, kwa hakika watapata hizi baraka zote. Wakati tunazaliwa mara ya pili tunapata baraka zote ambazo Kristo ametayarisha.

Kwa hivyo Kristo anasema kwamba watu wote wa ulimwengu wanahitaji kuzaliwa mara ya pili. Mtu hawezi kubadilika hadi yeye azaliwe mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili ni msingi wa kuwa mtu mpya na kuanza kuishi maisha mapya.

Pengine mtu atasema, “Ninajua watu ambao ni watu wa dini sana lakini wao ni watenda mabaya katika maisha yao. Wao ni watu wa dini lakini wao hawaishi maisha mapya bali wanaishi maisha ya dhambi.” Yesu Kristo pia alijua watu kama hawa. Lakini hii haimaanishi kwamba kuzaliwa mara ya pili haina faida. Kristo alisema kwamba wale ambao ni watu wa dini sana lakini wanaishi maisha ya dhambi ni wanafiki. Yeye aliwaambia watu kama hawa, “Mnasafisha nje ya kikombe na kisahani, lakini ndani mmejaa unyang’anyi na kutokuwa na kiasi” (Mathayo 23:25). Pia, Yeye aliwaambia watu kama hawa, “Mnafanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, ambayo yanapendeza kwa nje lakini ndani yamejaa mifupa ya wafu na kila aina ya uchafu” (Mathayo 23:27).

Kristo alikutana watu wengi ambao walidai kwamba wao ni watu wa dini lakini kwa ukweli wao walikuwa watu wa dhambi. Jambo hili halikumshangaza. Kuna watu wengi ulimwenguni kama hawa, lakini hii haimaanishi kwamba hata kama mtu amezaliwa mara ya pili, yeye bado anaweza kuishi maisha maovu kabisa. Bali inamaanisha kwamba wao kwa ukweli hawajazaliwa mara ya pili. Yeye alisema kwamba watu wa dini ambao wanaishi maisha ya dhambi kabisa ni "Uzao wa nyoka" (Mathayo 12:34). Maneno haya ya Yesu Kristo yanatufundisha kwamba yule ambaye hajazaliwa mara ya pili ni mwenye dhambi mkuu na ako katika hali mbaya sana ya kiroho kwa sababu yeye ni mwenye dhambi kutoka ndani mwake. Yeye hahitaji kubadilisha tabia ya maisha yake hapa na pale, yeye anahitaji kubadilishwa kutoka kwa ndani mwake, yeye anahitaji kuzaliwa mara ya pili. Ni kweli kwamba kuna wengi ambao wanadai wao wameokoka ambao wanaishi maisha ya dhambi kama tu watu wa dunia. Lakini hii haimaanishi kuzaliwa mara ya pili haina maana, inamaanisha mtu huyu hajazaliwa mara ya pili na anahitaji kuzaliwa mara ya pili!

Pengine unaona kwamba wewe uko na mambo mabaya mengi katika maisha yako ambayo yanahitaji kubadilishwa. Pengine rafiki zako hawaoni mambo haya kwa sababu haya ni mambo ya siri, lakini unajua kwamba wewe si mtu mwema mbele za Mungu, bali wewe ni mtu wa dhambi na unatenda dhambi nyingi. Unajua kwamba unahitaji maisha yako yanahitaji mabadiliko kwa sababu bila kufanya hii hutaingia mbinguni. Unajua kwamba ukisimama mbele za Mungu katika hali yako ya sasa, bila shaka utahukumiwa jahanum milele. Unajua kwamba unahitaji kubadilishwa kutoka ndani mwako. Unajua kwamba haitoshi kubadilisha tabia ya maisha yako hapa na pale kidogo kidogo, bali unahitaji kubadilishwa kamili kutoka kwa moyo wako.

Pengine, wakati unaangalia maisha ya watu wa dunia, unaona kwamba kuna taabu kubwa sana ndani yao. Unaona kwamba wengi wanadai wao ni watu wa dini na watu wa Mungu, lakini

wakati unachunguza maisha yao kwa uangalifu na hekima unajua kwamba wao kweli si watu wa Mungu, bali ni watu wa dhambi. Unajua kwamba kwa ukweli wao wako na upendo wa dunia na vitu vya dunia mioyoni mwao. Unajua kwamba wao si wanyenyekevu bali ni watu wa kiburi na majivuno na wanapenda sana kuheshimiwa na watu wa dunia. Moyoni mwako unajua kwamba watu hawa wanahitaji kubadilishwa. Unajua kwamba haitoshi kubadilisha tabia ya maisha yao hapa na pale, bali wanahitaji kubadilishwa kutoka kwa mioyo yao, wanahitaji kubadilishwa kutoka ndani mwao.

Kama wewe ni mtu kama huyu, basi unahitaji kufahamu vizuri mafundisho ya Biblia kuhusu kuzaliwa mara ya pili. Unahitaji kufahamu kwamba kuna njia moja tu kwa mtu kubadilika kabisa na kuwa mtu mpya na kuishi maisha matakatifu ya kweli na hii ni kuzaliwa mara ya pili. Hakuna njia nyingine ya kubadilisha mtu. Unaweza kujaribu kubadilisha tabia ya maisha yako, lakini wewe bado utakuwa mwenye dhambi, na mwishowe utashindwa. Pengine utakuwa mtu wa tabia mpya kwa muda kidogo, lakini kwa sababu wewe ni mwenye dhambi kutoka kwa moyo wako, utarudi kwa maisha ya dhambi. Wewe unahitaji kuomba Mungu akubadilishe kutoka kwa ndani, yaani, unahitaji kuomba Mungu akuzae mara ya pili.

Siku moja Yesu Kristo atarudi na ulimwengu wote utakuwa ulimwengu mpya. Ufalme wa Mungu utakuja ukiwa umekamilika. Yesu Kristo atakuwa hazina ya watu wake na atawatosheleza watu wake kikamilifu na milele. Dunia hii itakuwa dunia mpya, itakuwa dunia ambayo imekamilike na ni mzuri bila dhambi yoyote na ni makosa yoyote. Lakini si watu wote ambao watasherekea dunia mpya. Yesu Kristo alisema, “Amin, amin, nakuambia, mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mbingu asipozaliwa mara ya pili” (Yohana 3:3). Yesu Kristo ndiye njia na kweli na uzima (Yohana 14:6).

Tukitaka uzima, tunahitaji kuja kwake. Bila kuja kwake hatuwezi kupata uzima huu sasa au milele. Mungu mwenyewe anawapatia watu uzima wa milele, na uzima huu uko ndani ya Mwana wake (1 Yohana 5:11). Yule ambaye anaye Mwana anao uzima (1 Yohana 5:12). Tunaweza kutegemea neno lake wakati Yeye alisema, "Mnataka kuja Kwangu ili mpate uzima" (Yohana 5:40). Ukija kwake Kristo, utakuwa na uzima wa milele wa kweli.

**Vitabu hivi vinaweza kupatikana katika kanisa la:**

Injili Bible Church,
P.O. Box 20447,
00200 City Square,
Nairobi,
Kenya.
injili.bible@gmail.com
Simu (0723) 570222
www.clik-africa.org

*Dhambi ni Hatari*

*Je, Umezaliwa Mara ya Pili*

*Utakatifu*

*Kutembea na Mungu*

*Kwa nini Yesu Kristo alikufa msalabani*

*Ufafanuzi wa Injili ya Mathayo*

*Ufafanuzi wa Injili ya Marko*

*Ufafanuzi wa Injili ya Luka*

*Ufafanuzi wa Injili ya Yohana*

*Mchungaji na Kazi Yake*

*Kimbia utoroke ulimwengu huu wa dhambi*

*Ulafi na Ukristo wa Ukweli*

*Hatari ya Kuupenda Ulimwengu*